

# UP-ATA-NISHO

## NJIA YA KUKAMILISHA UREJESHWAJI NA MUNGU

ADRIAN EBENS

# UP-
# ATA-
# NISHO

## NJIA YA KUKAMILISHA UREJESHWAJI NA MUNGU

ADRIAN EBENS

FATHER
OF LOVE
fatheroflove.info

Adrian Ebens, 2021
Hakimiliki © 2021, Adrian Ebens
Haki ya kimaadili ya mwandishi imethibitishwa.
Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kuzalishwa tena kwa faida ya kibiashara, ikijumuisha kusambazwa kwa njia yoyote ile, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodi au vinginevyo, bila kibali cha maandishi cha awali cha mchapishaji na wenye hakimiliki. Tafadhali kumbuka kuwa mwandishi amekoleza wino sehemu za mistari ili kusisitiza jambo Fulani lililokusanywa kutoka kwenye maandiko hayo.
Isipokuwa imeonyeshwa vinginevyo, nukuu za Maandiko zimetolewa katika Biblia Mpya ya King James Version. Hakimiliki © 1982 na Thomas Nelson, Inc. Imetumiwa kwa ruhusa.
Nukuu za Maandiko zinazotokana na NIV zimetoka katika Biblia Takatifu, New International Version, hakimiliki ©1973, 1978, 1984, 2011 naBiblica, Inc.® Imetumiwa kwa ruhusa.
Nukuu za Maandiko zinazotokana na YLT zimetoka katika Biblia Takatifu, Young’s Literal Translation, hakimiliki © 1898, na Robert Young, ambayo sasa iko hadharani.
Nukuu za Maandiko zinazotokana na Apostolic Polyglot zimetoka katika Apostolic Bible Polyglot, hakimiliki © 1995, na Charles Lynn VanderPool, Sr. Haki zote zimehifadhiwa.
Nukuu za Maandiko zinazotokana na Habari Njema zimetoka katika Biblia Habari Njema, Hakimiliki © 1976, 1992, na American Bible Society. Haki zote zimehifadhiwa.
Viungo vyote vya tovuti na maudhui yaliyonukuliwa ni ya sasa kuanzia Desemba 2021.
Kitabu hiki na machapisho mengine yote ya Father of Love yanapatika na kutoka kwenye tovuti yetu fatheroflove.info ili kuagiza nakala za ziada tafadhali tuma barua pepe kwa adrian@life-matters.org
ISBN: 978-0-6488114-8-0

Kitabu hiki kimeandikwa na Adrian Ebens
Kimeandaliwa na Danutasn Brown
Kimethibitishwa na Lorelle Ebens
Jalada limetengenezwa na Shane Winfield/Advent Design
Picha ya Jalada na Josh Imerbin/Shutterstock.com
Aina 10.5/14 Palatino Linotype

Kimechapishwa nchini Australia

# Yaliyomo


1. Katika Kutafuta ........ 5

2. Muktadha Wa Wanamatengenezo ........ 14

3. Haki Ya Mungu Na Adhabu ........ 19

4. Usaliti Uliofichwa Wa Adamu ........ 25

5. Nimekutukuza Duniani ........ 34

6. Kiti Cha Uovu ........ 39

7. Nyoka Aliyeinuliwa ........ 48

8. Kupiga Mwamba ........ 58

9. Upatanisho Wa Mwanadamu ........ 63

10. Dhambi Ilipozidi, Neema Ilikuwa Nyingi Zaidi ........ 73

11. Mauaji Ya Wasio Na Hatia ........ 82

12. Pazia La Mwili Wake ........ 92

13. Muktadha Wa Kisa Cha Ibrahimu Na Isaka ........ 106

14. Imani Ya Ibrahimu ........ 117

15. Danieli Na Usaliti Wa Kuchukiza Wa Pembe Ndogo ........ 130

16. William Miller, Kila Siku Na Kosa La Uharibifu ........................... 137

17. Utakasaji Wa Patakatifu .................................................................. 146

18. Ulinganisho Kati Ya Upatanisho Wa Waprotestanti Na Waadventista ................................................................................... 154

19. Patakatifu Pa Mbinguni.................................................................. 163

20. Hukumu Na Kuondolewa Kwa Dhambi....................................... 174

21. Kuvunja Nira Ya Maagano Mawili................................................. 186

22. Kuufikia Utu Uzima—Msalaba Ni Jambo La Sasa........................ 199

23. Maana Ya Damu Katika Patakatifu ................................................. 209

24. Adhabu Yetu Sote ........................................................................... 218

25. Kurejea Jangwani ............................................................................ 232

26. Kuleta Uasi Katika Ukamilifu Wake ............................................... 246

27. Hakuna Chronos Tena..................................................................... 255

28. Mwanangu Mpendwa ..................................................................... 263

29. Huduma Ya Upatanisho ................................................................. 269

30. Ujumbe Wa Malaika Wa Kwanza................................................... 276

31. Umeanguka Babeli ........................................................................... 284

32. Moyo Wa Shukrani .......................................................................... 290

SURA YA 1

# KATIKA KUTAFUTA UPATANISHO

*"Nitapatanishwaje na Mungu?"* Swali hili linaonyesha shauku ya ndani ya mabilioni ya nafsi za wanadamu ambazo zimesafiri katika giza la ulimwengu huu ulioanguka.

Hisia zilizokusanywa za hatia, inayozidi kukua ndani ya fahamu za mioyo ya wanadamu ambao wameasi dhidi ya Muumba wao, inasababisha nafsi kutamani msamaha na upatanisho.

Baba yetu aliye mbinguni ameandika kanuni za ufalme wake katika mbao za moyo wa mwanadamu. Hisia za mema na mabaya ambayo hutuchoma katika dhamiri zetu tunaposema uongo, kuiba, na kuua hutukumbusha kwamba tunawajibika kwa mtu aliye mkuu kuliko sisi wenyewe.

Fundisho la Kikristo la upatanisho limejaribu kutufafanulia utaratibu wa jinsi tunavyoweza kupata kuachiliwa kwa nafsi zetu zenye hatia na amani pamoja na Muumba wetu na wanadamu wenzetu.

Hiki ndicho mhubiri maarufu wa Kikristo Billy Graham anachokisema kuhusu maana ya upatanisho katika muktadha wa Kikristo:

*…uhakikisho unategemea kazi iliyokamilika ya Yesu Kristo. Yesu alipokufa msalabanNoliyachukua maovu yetu, akistahimili ghadhabu ya Mungu, na akapaza sauti, "Imekwisha!" (Yohana 19:30). Kwa hili, alimaanisha kwamba upatanisho kamili wa dhambi zetu zote - zilizopita, za sasa na zijazo - umefanywa. Kazi yake ya ukombozi sasa imekamilika, deni lote la dhambi limelipwa kikamilifu*.[1]

Mtazamo huu unakitazama kifo cha Yesu kuwa ni kutosheleza ghadhabu ya Mungu; Yesu anachukua nafasi yetu na anapokea adhabu tunayostahili ili tuweze kuwekwa huru. Lakini watu wengi ulimwenguni wana maswali kuhusu kisa hiki. Mungu ana ghadhabu juu ya nini, na kumtuma Mwana Wake afe kunatoshelezaje ghadhabu hiyo? Kifo cha Kristo hulipaje deni la dhambi ambazo wanadamu wanaendelea kufanya leo?

Katika kiini cha upatanisho ni kisa cha Yesu Kristo ambaye alihukumiwa kifo kupitia uovu wa viongozi wa kidini wa taifa lake na kutundikwa juu ya msalaba wa Warumi. Watu walimuua Kristo; watu walimtaka auawe. Je, Baba yake pia alitaka afe? Je, Yesu alijiweka mwenyewe ili afe?

Maana ya kifo chake juu ya Msalaba na jinsi ambavyo hili hupelekea katika msamaha na amani kwa nafsi iliyo na hatia haiko wazi kama mtu anavyoweza kufikiria.

Alipokuwa akizungumza na mmoja wa viongozi wa Kiyahudi ambaye alivutiwa na huduma ya Kristo, Yesu alionyesha sehemu muhimu ya fumbo kwa ajili ya upatanisho.

*"Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye." Yohana 3:14-15*

Yesu alimwelekeza msikilizaji wake kwenye kisa kuhusiana na Musa na wana wa Israeli mara tu walipotoka Misri. Watu walikuwa wakilaumu na kumnung'unikia Mungu na Musa juu ya magumu yao

[1] https://billygraham.org/story/how-to-be-sure-of-your-salvation/

waliyoyawazia kule jangwani, bila kujali ukweli kwamba Mungu alikuwa amewapa mahitaji yao yote. Mungu amekuwa akiwalinda kutokana kwenye majanga na pia hatari za viumbe wa jangwani.

Ulinzi wa Mungu uliondolewa kwa sababu ya ubinafsi wa kutokuwa na shukrani na nyoka wakaingia kati ya watu na kuanza kuwauma. Kilichofuata kinaonekana kuwa cha kushangaza sana.

> *Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu. BWANA akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa. Watu wakamwendea Musa, wakasema, Tumefanya dhambi kwa sababu tumemnung'unikia Mungu, na wewe; utuombee kwa BWANA, atuondolee nyoka hawa. Basi Musa akawaombea watu. Bwana akamwambia Musa, "Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi." Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi. Hesabu 21:5-9*

Musa aliagizwa kutengeneza sanamu ya shaba ya kitu kile kile ambacho Mungu alikituma kuwauma na kuwaua watu kwa ajili ya uasi wao - nyoka mwenye sumu kali. Kisha watu waliamriwa kutazama kielelezo hiki cha kile kilichokuwa kinawaua na kwa kumwangalia yule nyoka wa shaba, wakitumaini neno la Mungu, wangeishi.

Kwa kustaajabisha, Yesu alimwambia Nikodemo kwamba kwa namna hiyo hiyo Musa alipomwinua yule nyoka wa shaba nyikani, kuinuliwa kwa Yesu kungewafanya wote ambao wangemtazama kwa imani, wakimwamini, kuishi.

Ni hadithi ya ajabu sana ambayo kwayo tunaweza kuweka msingi wa jinsi mwanadamu anavyoweza kupata amani na Mungu na kuwa na uzima wa milele. Je, Yesu alikuwa akijilinganisha na nyoka, ambaye kimsingi anamwakilisha Shetani? Kwa nini Mungu alimwomba Musa

atengeneze sanamu ya nyoka waharibifu kisha akawataka watu waitazame kwa imani sura ya kile kilichokuwa kinawaangamiza ili wapone? Kwa nini asitengeneze sanamu ya mponyaji au ya kile kinachoiangamiza nyoka? Kwa nini si sanamu ya mwana-kondoo au njiwa; hiyo haingekuwa na maana zaidi? Je, unawezaje kuponywa ukitazama sanamu ya kitu hicho hicho kinachokuua? Kwa nini Yesu alijilinganisha na kitu kilichokuwa kinawaangamiza - nyoka?

Maswali haya yanatumika kusisitiza hoja kwamba kuna fumbo katika kiini cha mchakato wa jinsi mtu anavyoweza kupata msamaha na upatanisho.

Utafiti huu unatatizwa zaidi na mambo mengine ambayo Yesu anayasema kuhusiana na njia ya wokovu. Yesu alipoulizwa na mtu jinsi gani angeweza kupata uzima wa milele, Yesu alitoa jibu ambalo huenda tusingelitazamia.

> *Na tazama, mwana-sheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Akamwambia, Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako. Akamwambia, Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi. Luka 10:25-28*

Kwa nini Yesu alimwelekeza mtu huyu kwenye torati na kumuuliza maana yake? Yesu hasemi chochote kwa mtu huyo kuhusu kufa kwa ajili ya dhambi zake na kwamba ikiwa angeamini dhabihu ya Yesu kama malipo ya dhambi zake basi angeokolewa. Yesu anakubaliana tu na taarifa ya mtu huyo kwamba tunapaswa kumpenda Mungu kwa mioyo yetu yote na jirani zetu kama sisi wenyewe. Je, ni kwa sababu Yesu anazungumza na mtu ambaye hajui kuhusu mchakato wa wokovu na anajaribu tu kumwelekeza katika njia ifaayo? Kwa nini Yesu hakuzungumza kuhusu dhabihu yake na haja ya kuamini juu ya dhabihu hii kwa ajili ya wokovu?

Usiku kabla ya Yesu kukamatwa na kusulubishwa, alikuwa akiomba kwa Baba yake. Jambo moja aliloomba kiuhalisia hugonga uelewa

uliozoeleka kama unavyoelezewa katika Ukristo kuhusiana na upatanisho.

> *"Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye." Yohana 17:4*

Je, Yesu anawezaje kusema kwamba amemaliza kazi ambayo Baba yake alimpa usiku kabla ya kufa Msalabani? Ikiwa kuamini dhabihu ya Yesu Msalabani kama mbadala wa dhambi zetu ni kiini cha imani ya Kikristo, basi Yesu anamaanisha nini kwa hili? Je! Alisema hivi kwa kutarajia siku iliyofuata? Je! Hangepaswa kuomba, "Tuko karibu kufika; sehemu kubwa tumekwisha imaliza, Baba."?

Haya ni baadhi ya maswali yanayofanya somo la upatanisho kutokuwa rahisi kuliko tunavyoweza kufikiria. Haishangazi, mwanatheolojia mmoja, Leon Morris, ambaye aliandika mengi juu ya somo la upatanisho, anakiri kwa kushangaza kuhusu waandishi wa Agano Jipya na maneno yao kuhusu wazo la upatanisho:

> *Waandishi wa Agano Jipya hawarudii hadithi iliyozoeleka. Kila mmoja anaandika kwa mtazamo wake. Lakini kila moja inaonyesha kwamba ni kifo cha Kristo na si mafanikio yoyote ya kibinadamu ambayo huleta wokovu. Lakini hakuna hata mmoja wao anayeweka nadharia ya upatanisho*.[2]

Anaendelea kusema:

> *Nadharia za upatanisho ni jeshi kwa vile wanadamu katika nchi mbalimbali na katika zama mbalimbali wamejaribu kuleta pamoja hoja mbalimbali za mafundisho ya kimaandiko na kuzifanyia kazi katika nadharia ambayo itasaidia wengine kuelewa jinsi ambavyo Mungu amefanya kazi ili kutuletea wokovu*.[3]

Na hatimaye anahitimisha:

---

[2] https://www.monergism.com/thethreshold/articles/onsite/atonementmorris2.html
[3] Ibid

*Lakini sisi ni wadhambi wenye akili ndogo na upatanisho ni mkubwa na mkubwa zaidi. Hatupaswi kutarajia kwamba nadharia zetu zitawahi kuuelezea kikamilifu. Hata tunapoziweka pamoja, hatutaweza zaidi ya kuanza kufahamu kidogo ukubwa wa tendo la kuokoa la Mungu*.[4]

Je, Biblia haisemi utaratibu kamili wa upatanisho? Je! ni fumbo kiasi kwamba haikuweza kuandikwa vya kutosha katika Maandiko? Ushahidi unaounga mkono kile Leon Morris anachokipendekeza ni kwamba Ukristo umegawanyika juu ya mchakato wa upatanisho na jinsi ya kuuelezea.

Kuna nadharia kadhaa za upatanisho ambazo zimeendelezwa kwa muda tangu Kristo alipokaa duniani. Wazo lililotawala fikira za Kikristo baada ya Mitume kufa, na kuendelezwa na mababa wa kanisa la kwanza lilikuwa ni nadharia ya ukombozi.

*Kimsingi, nadharia hii ilidai kwamba Adamu na Hawa waliuza ubinadamu kwa Ibilisi wakati wa Anguko; kwa hiyo, ilihitaji kwamba Mungu amlipe Ibilisi fidia ili atukomboe kutoka katika makucha ya Ibilisi. Hata hivyo, Mungu alimdanganya Ibilisi ili akubali kifo cha Kristo kuwa fidia, kwa kuwa Ibilisi hakutambua kwamba Kristo hangeweza kufungwa katika vifungo vya kifo. Ibilisi alipokubali kifo cha Kristo kuwa fidia, nadharia hiyo ilikata kauli kwamba, haki ilitimizwa na Mungu akaweza kutuweka huru kutoka katika vifungo w vya Shetani*.[5]

Lengo la nadharia hii ni, bila shaka, fidia iliyolipwa ili kuwakomboa wanadamu. Inaonyesha mtazamo wa Mungu kama anayefanya biashara na shetani na hata kumdanganya ili kuwaokoa wanadamu. Mungu anaeleweka kuwa mtu mwerevu, mwenye hila ambaye humpita mpinzani wake kwa werevu. Augustine, akiandika kuhusiana na hili, alisema:

[4] Ibid

[5] https://en.wikipedia.org/wiki/Ransom_theory_of_atonement

*Mkombozi alikuja na mdanganyifu akashindwa. Mkombozi wetu alifanya nini kwa mtekaji wetu? Kwa ajili ya malipo yetu aliweka mtego, Msalaba wake, kwa damu yake kama chambo. Yeye [Shetani] angeweza kweli kumwaga damu hiyo; lakini hakustahili kuinywa. Kwa kumwaga damu ya Mtu ambaye hakuwa mdeni wake, alilazimika kuwaachilia wadeni wake*.[6]

Je, hivi ndivyo Mungu anavyotenda? Je, hii ni haki? Je, hushughulikia masuala yote yanayohusika katika jinsi ubinadamu ulivyoanguka na kwa nini Yesu alipaswa kuja? Wakristo wengi leo wanakubali kwamba mtazamo huu una matatizo na mfinyu sana. Wazo la fidia linakaziwa lakini mfumo wa fidia unatia shaka. Bila kujali matatizo hayo, wazo hilo lilikuwa maarufu katika makanisa mengi hadi karne ya kumi na moja wakati Askofu Mkuu wa Canterbury, Anselm, alipoanzisha ile iitwayo nadharia ya kuridhisha ya upatanisho.

Anselm alizaliwa huko Burgundy ya juu kwenye mpaka wa Ufaransa na Italia. Katika umri wa miaka kumi na tano, alitamani kuingia kwenye monasteri lakini baba yake alikataa kumruhusu. Baada ya mama yake kufariki, baba yake Anselm alizidi kuwa mtu wa kidini jambo ambalo Anselm aliliona kuwa kali sana. Muda mfupi baadaye, aliondoka nyumbani kutafuta njia yake ulimwenguni. Baba yake alipokufa, alitafakari ikiwa angerudi kuchukua milki ya baba yake au kujiunga na nyumba ya watawa na kuwa mtawa. Akachagua la mwisho.[7]

Anselm alifaulu katika shughuli za kielimu na alipanda vyeo hadi akawa Askofu Mkuu wa Canterbury. Anselm alipambana na wafalme wa Uingereza na kufukuzwa mara mbili wakati wa mabishano aliyoyaendesha. Anselm alikuwa na falsafa ya Uplatoni Mpya katika mtazamo wake wa ulimwengu ambayo ina maana kwamba aliyaendea Maandiko kupitia mfumo wa falsafa ya Kigiriki kama

[6] https://www.newadvent.org/cathen/02055a.htm
[7] https://en.wikipedia.org/wiki/Anselm_of_Canterbury

wasomi wengi wa Kikristo kabla na baada yake. Haishangazi kwamba tunapata mada ifuatayo katikati ya dhana za Anselm za upatanisho.

> *Katika karne ya kumi na moja Anselm, Askofu Mkuu wa Canterbury, alitoa kitabu kidogo kiitwacho Cur Deus Homo? ("Kwa nini Mungu alifanyika Mwanadamu?"). Ndani yake aliweka mtazamo wa mababa wa awali wa fidia iliyolipwa kwa Shetani. Aliona dhambi kuwa ni kudhalilisha ukuu wa Mungu.* ***Sasa mtawala anaweza kuwa tayari katika nafasi yake binafsi kusamehe tusi au jeraha, lakini kwa sababu yeye ni mtawala hawezi.*** *Jimbo limevunjiwa heshima kichwani mwake. Utoshelevu unaofaa lazima utolewe.* ***Mungu ndiye Mtawala mkuu wa wote, na haifai kwa Mungu kuondoa kasoro yoyote katika ufalme wake****. Anselm alidai kwamba dhambi ya matusi ambayo imetolewa kwa Mungu ni kubwa sana hivi kwamba ni mmoja tu ambaye ni Mungu anayeweza kutoa uradhi.*[8]

Inavutia kutafakari jinsi Anselm anavyofikia hitimisho hili. Wanaonekana kuwa wametolewa kutoka kwenye mantiki ya nadharia ya kisiasa, badala ya Maandiko. Je, kweli Mungu hawezi kusamehe kwa sababu ya cheo chake kama Mkuu wa Nchi? Mungu, katika kuzungumza na Musa, alidhihirisha wazi tabia yake kuhusu rehema na msamaha:

> *BWANA akapita mbele yake, akatangaza, BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne. Kutoka 34:6-7*

Hakuna dokezo la Mungu kutoweza kusamehe bila kuridhika fulani kwa ukuu Wake uliotukanwa. Juu ya Msalaba, Kristo anaonyesha kwa namna ya juu kabisa uwezo wa Mungu wa kuwasamehe wale

---

[8] Leon Morris – Theories of atonement

wanaomkosea. Tunapozingatia uzoefu wa Anselm na baba yake mwenyewe na migogoro yake na wafalme wa Uingereza, ni rahisi kuona mfano wa uzoefu wake mwenyewe kwa Mungu.

> *Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Yakobo 1:23-24*

Hadithi ya Anselm inatumika kutukumbusha kwamba wanadamu wanajaribiwa sana kuelekeza tabia zao wenyewe kwa Mungu ili kutakasa na kutoa udhuru kwa imani zao, maamuzi na tabia zao. Hii ndiyo sababu kuu ya fumbo la upatanisho. Wanadamu wanaona Mungu anatenda kama ambavyo wangefanya. Uelekezaji huu ni wa asili na rahisi pale ambapo haturuhusu Maandiko kujitafsiri yenyewe. Kupitia mfumo wa Uplatoni Mpya, Anselm alikuwa huru kuwasilisha matamanio yake mwenyewe kwa Baba yetu wa mbinguni na kusaidia kuimarisha ndani ya Ukristo mtazamo wa Mungu kama mtawala mkali na asiyesamehe ambaye ukuu wake uliokosewa lazima uridhishwe. Kwa vyovyote yeye si wa kwanza, na kuna Maandiko mengi ambayo yanaweza kuonekana kutoa uthibitisho wa mawazo yake.

Anselm ni mtu muhimu sana katika kuzingatia somo la upatanisho, kwa maana wanamatengenezo wa Kiprotestanti walikuza na kuboresha mawazo yake katika nadharia kuu ya upatanisho iliyopo leo inayoitwa Mbadala wa Adhabu.

SURA YA 2

# MUKTADHA WA WANAMATENGENEZO

Muda mfupi baada ya wakati wa Anselm, karibu 1200-1300 A.D., ilikuwa kilele cha nguvu za Kanisa Katoliki. Papa alitawala Ulaya yote, akiamuru wafalme na kutangaza ni nani aliyekwenda mbinguni na nani alikwenda kuzimu. Haki hii ya kutawala inaeleweka vyema kwa maneno yao wenyewe.

> *Papa Innocent III (1198-1216, labda mwenye nguvu zaidi ya Papa wote) aliteua maaskofu wote; alileta kwenye mahakama yake sababu zote, kuanzia mambo mazito ya falme kuu hadi mahangaiko ya faragha ya raia mnyenyekevu. Alidai falme zote kama zake, wafalme wote kama vibaraka wake; na akaanzisha kwa mkono usio na huruma miiko ya kuwatenga watu wote waliopinga utashi wake wa kipapa...*
>
> *Innocent wa Tatu alithibitisha "kwamba mamlaka ya papa yalizidi sana mamlaka ya kifalme kama vile jua linavyoufanya mwezi." Wala hangeweza kupata maneno ya kufafanua kazi zake zenye kutisha, isipokuwa zile za Yehova kwa nabii wake Yeremia: "angalia, nimekuweka leo juu ya mataifa na juu ya falme, ili kung'oa, na kubomoa, na kuharibu, na kuangamiza."*

> *“Tunatangaza,” asema Boniface VIII (1294-1303), katika fahali wake Unam Sanctam, “hufafanua, na kuitamka kuwa ni muhimu kwa wokovu kwa kila kiumbe cha kibinadamu kuwa chini ya Papa wa Kiroma.” Utii huu unatangazwa katika fahali ili kupanua mambo yote. “Upanga mmoja,” asema Papa, “lazima uwe chini ya mwingine, na mamlaka ya muda lazima yawe chini ya nguvu za kiroho; kutoka hapo, ikiwa nguvu ya kidunia itapotea, lazima ihukumiwe na roho.” Hayo ni machache ya “maneno makuu” ambayo yalisikiwa yakitoka katika Mlima wa Vatikani, ile Sinai mpya, ambayo, kama ile ya kale, iliyozungukwa na vitisho vikali, ilikuwa imejiinua yenyewe katikati ya mataifa yaliyostaajabu na kutishwa ya Jumuiya ya Wakristo. (J.A. Wylie, History of Protestantism)*

Huu ulikuwa Ukristo tofauti kabisa na ule uliokuwepo wakati wa Mitume, kutokana na uhusiano wa kanisa na nguvu na mamlaka. Katika kipindi cha kanisa la kwanza hapakuwa na mwelekeo wa jinsi ya kutawala mataifa kwa sababu Ukristo ulikuwa katika wachache na ulikuwa unateswa duniani. Wanatheolojia wa Kikristo wa awali walijali zaidi jinsi ya kuishi katika ulimwengu wa kipagani.

Lakini kufikia miaka ya 1300 Ulaya yote ilikuwa imefanywa kuwa "Wakristo" na chini ya udhibiti kamili wa watawala wa kanisa huko Roma, na kwa hiyo Mapapa walizingatia jinsi ya kutawala na kushikilia taratibu za kidini. Ulazima huu wa kuweka akili za wanadamu katika ufahamu sawa na wa watawala wao, ili “kulinda amani,” waonekana katika mwanatheolojia mkuu wa kipindi hicho, Thomas Aquinas, aliyekuwa mashuhuri miaka 100 hivi baada ya Anselm, akitetea kuchomwa moto kwa wazushi. –wakiwa hai.[9]

Katika kanisa la kwanza, kukomesha uzushi halikuwa suala kwa sababu rahisi kwamba hapakuwa na taratubu za kidini. Hapo awali kulikuwa na maoni mbalimbali kuhusu jinsi ya kuyaelewa Maandiko, na uhuru mkubwa kwa kila mmoja kujiamulia mwenyewe. Hii ni

---

[9] https://www.heretication.info/_heretics.html

tofauti kabisa na hali ya uhuru wa dhamiri wakati wa kilele cha Ukristo wa Kiroma uliojikita katika sehemu kuu, ambapo Maandiko hayakupatikana katika lugha ya kawaida na makuhani walionwa kuwa ndio pekee walioweza kuyasoma na kuyafasiri. Kwa mabadiliko haya ya Ukristo, uzushi ulikuja kuonekana kuwa tishio zaidi na zaidi.

Katika karne ya sita wakati Justinian alipokabidhi mamlaka ya Kaisari kwa papa wa Kirumi, alitunga sheria dhidi ya wazushi zilizohitaji kufukuzwa ofisini lakini maisha yao yalindwe. Kwao, Justinian alisema, "kuwepo kunatosha."[10]

Wakati nguvu ya kuvuta ya upendo wa Kristo inapoondolewa kutoka kwa mwanadamu, nguvu pekee iliyobaki ni ile ya nguvu na tishio la kifo. Kanisa lilipozidi kuwa juu ya mafundisho ya imani na siasa badala ya Maandiko, huduma, na kuwafikiria wengine kuwa bora kuliko wewe mwenyewe, kifo kwa wapinzani kilizidi kuwa kitu cha kawaida.

Takwimu zinatofautiana sana kuhusu ni watu wangapi waliuawa kama wazushi wakati wa zama za giza, lakini jambo ninalotaka kulileta kutokana na hili ni kwamba Upapa uliwasilisha kwa uwazi wazo kwamba uzushi lazima uadhibiwe kwa kifo.

Katika mauaji ya Waldensia na Albigensia; katika moto wa Smithfield; katika mahakama ya Kihispania miongoni mwa wengine wengi, tunaona uso wa mwanadamu ukionyeshwa kwenye uso wa Mungu na kuabudiwa kama Mungu.

Ni muhimu kuelewa kwamba fundisho la upatanisho lililoanzishwa na wanamatengenezo katika karne ya 16 lilikuwa katika muktadha wa mauaji ya maelfu mengi ya "wazushi" ambayo yalikuwa yameenea kwa miaka mia tatu iliyotangulia.
Wanamatengenezo walishutumu unyanyasaji wa Mapapa na kupinga ukatili wao lakini watoto wengi wanapogundua ni nani

[10] Ibid

anayewatukana wazazi wao, wanatambua kabisa kwamba sio jambo rahisi kuondoa kutoka kwenye tabia yako kile ulichojifunza ukiwa mtoto chini ya masomo yao.

Martin Luther aliwahimiza wakuu wa Ujerumani kukomesha uasi wa wakulima kwa nguvu baada ya awali kuonyesha huruma kwa kazi ya wakulima.

> *Martin Luther mwanzoni anaonyesha huruma fulani kwa shida ya wakulima. Yeye, mwenyewe, katika Mawaidha yake kwa ajili ya Amani mwaka wa 1525, alishutumu mtazamo wa "kiburi" wa watawala. Ni pale tu vikosi vya wakulima wanapochinja idadi na wasindikizaji wake, na hili linazua ghasia kama "hati ya umwagaji damu ya Weinsberg", ambapo mwanamatengenezo anabadilisha pande. Sasa anajitenga sana na waasi. Kwa maandishi yake "Dhidi ya Makundi ya Mauaji ya Wakulima wa Uporaji", anawahimiza wakuu walipize kisasi kikatili. "Lazima wakatwe vipande vipande, wakasongwe, wakachomwe visu, kwa siri na hadharani, na wale ambao wanaweza, kama vile ambavyo mtu lazima amuue mbwa mwenye kichaa." Luther anachagua kutumia "uhuru wa Mkristo" kwa mambo ya kiroho na si kwa eneo la kiulimwengu*.[11]

Haiwezekani kwa mtu anayeamini kwamba wakulima waliofanya mauaji wanapaswa kukatwa vipande vipande, kusongwa na kuchomwa visu kama mbwa mwenye kichaa asilete mawazo haya katika kuelewa jinsi Mungu anavyoshughulika na tabia ya dhambi.
John Calvin alitaka Michael Servetus mjanja auawe kwa kuunga mkono mafundisho ya uzushi. Calvin alimwandikia William Farel kuhusu suala hilo:

> *Natumaini kwamba hukumu ya kifo angalau itatolewa juu yake; lakini nilitaka ukali wa adhabu uweze kupunguzwa*[12]

Calvin aliomba Servetus akatwe kichwa, badala ya kuchomwa moto akiwa hai, ili kujaribu kupunguza ukali wa adhabu. Kwa mara

---

[11] https://www.dokumentarfilm.com/en/luther-and-the-peasants-war
[12] https://en.wikipedia.org/wiki/Michael_Servetus

nyingine tena, Calvin anafunua mawazo yake kuhusu jinsi Mungu anavyoshughulika na wale wanaoonwa kuwa waovu. Je, tunahusianishaje hili na maneno ya Yesu?

> *"lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:44-45*

Luther na Calvin wote walikuwa muhimu katika kuunda fundisho la upatanisho ambalo lina ushawishi mkubwa zaidi leo -Mbadala wa Adhabu[13]. Zilikuwa bidhaa za wakati wao. Ni ukweli usiopingika kwamba watu husoma Biblia kupitia mtazamo wa utamaduni na malezi yao. Ndani ya muktadha wa kile kilichokuwa kikitukia katika zama za Kati, Luther na Kalvini waling'aa gizani, na kwa ajili ya hili sote tunapaswa kushukuru, hata hivyo, katika kutafuta kwetu ukweli hatuwezi kuruhusu shukrani zetu kwao zitupofushe tusione mapungufu yao. Wangetamani tusonge mbele katika nuru ambayo wameanzisha.

Hebu sasa tuchunguze fundisho la Mbadala wa Adhabu kama kituo chetu kinachofuata katika utafutaji wetu wa kuelewa upatanisho.

---

[13] https://en.wikipedia.org/wiki/Penal_substitution

SURA YA 3

# HAKI YA MUNGU NA ADHABU

Ingawa Anselm alizungumza juu ya fidia katika kutosheleza haki ya Mungu, wanamatengenezo walizungumza juu ya adhabu. Martin Luther anaihuisha nadharia hiyo kwa njia ifuatayo:

> *Akiwa Mwana-Kondoo asiye na doa wa Mungu, Kristo hakuwa na hatia. Lakini kwa sababu alizichukua dhambi za ulimwengu kutokuwa na dhambi kwake kulitiwa unajisi na dhambi ya ulimwengu. Dhambi zozote ambazo mimi, wewe, sisi sote tumefanya au tutafanya, zinapaswa kuwa dhambi za Kristo au tutaangamia milele ... Baba yetu wa mbinguni mwenye huruma ... kwa hiyo alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni na kumwambia: "Wewe sasa ndiye Petro, mwongo; Paulo, mtesaji; Daudi, mzinzi; Adamu, muasi; mwizi msalabani, Wewe, Mwanangu, lazima ulipe uovu wa ulimwengu." Sheria inanguruma: "Sawa. Ikiwa Mwanao anachukua dhambi za ulimwengu, sioni dhambi mahali pengine popote*

*isipokuwa kwake. Atakufa Msalabani." **Na sheria inamwua Kristo. Lakini tunabakia huru**.*[14]

Luther anadai sheria ya Mungu inadai wanadamu waadhibiwe kwa sababu watu wote wamefanya dhambi, na Kristo anaingia mahali pa mwanadamu ili kupokea adhabu hiyo ili mwanadamu "abakie huru". Ubinafsishaji wa sheria unaonyesha ugumu wa pendekezo hili. Badala ya kusema Baba ananguruma na Baba anamuua Kristo, Luther anasema kwamba sheria ndiyo inayofanya hivyo.

Wazo la Baba kumwadhibu Kristo limeibua wasiwasi mwingi kutoka kwa wasomi. Kwa mfano, John Scott anapinga wazo hilo kwa kusema "Hatupaswi kamwe kumfanya Kristo kuwa mlengwa wa adhabu ya Mungu."[15] Ili kuepuka shtaka hilo, Mbadala wa Adhabu hutegemea sana fundisho la Utatu ili kuruhusu tofauti ambayo Mungu alichukua adhabu juu yake mwenyewe katika nafsi ya Mungu Mwana.

*Dhana muhimu za kitheolojia kuhusu mbadala wa adhabu hutegemea fundisho la Utatu. Wale wanaoamini kwamba Yesu mwenyewe alikuwa Mungu, katika kupatana na fundisho la Utatu, wanaamini kwamba Mungu alijichukulia adhabu hiyo badala ya kuweka adhabu hiyo kwa mtu mwingine. Kwa maneno mengine, fundisho la muungano na Kristo linathibitisha kwamba kwa kuchukua adhabu juu yake Yesu anatimiza matakwa ya haki si kwa mtu wa tatu asiyehusika bali kwa wale wanaohusishwa naye*.[16]

Mbadala wa Adhabu unatafuta kuosha mikono yake juu ya athari mbaya za haki inayodai malipo kupitia fundisho la Utatu. Lakini sio wote wanaoshawishika ya hitaji la hoja hii. Kwa wengine ukweli halisia wa utawala wa Mungu unamaanisha kwamba Mungu ana hasira dhidi ya wale wanaovunja sheria yake na anadai adhabu - hivyo ndivyo Alivyo, Atawaadhibu wenye dhambi kama vile Papa anavyowaadhibu wazushi.

---

[14] Martin Luther, Commentary on St Paul's Epistle to the Galatians
[15] John Scott, The Cross of Christ, (Leicester, UK:InterVarsity, 1986), page 151
[16] https://en.wikipedia.org/wiki/Penal_substitution

*Nadharia yoyote ya upatanisho inayotosheleza kibiblia lazima ijumuishe wazo la upatanishaji, ni kusema, kutuliza ghadhabu ya haki ya Mungu dhidi ya dhambi.* ***Chanzo cha ghadhabu ya Mungu ni haki yake ya kulipiza kisasi, na hivyo kutuliza ghadhabu kimsingi ni suala la kuridhika kwa haki ya Mungu****. Je, madai ya haki ya kimungu yanatimizwaje? Kuzungumza Kibiblia, utoshelevu wa haki ya Mungu hasa hutukia, si kama alivyofikiri Anselm, kupitia fidia bali kupitia adhabu*.[17]

Charles Spurgeon anaielezea bila hofu yoyote. Angalia kwa makini muunganiko wa upendo na haki katika mchakato wake wa mawazo.

*…lazima tupime ukombozi mkuu kwa ukali wa haki ya kimungu"Mungu ni upendo," mwenye upendo daima; lakini pendekezo langu linalofuata haliingiliani hata kidogo na madai haya.* ***Mungu ni mwenye haki kali, mkali asiyebadilika katika shughuli zake na wanadamu****. Mungu wa Biblia si Mungu wa fikira za baadhi ya watu, Ambaye hufikiria dhambi kidogo sana hivi kwamba anaipita bila kudai adhabu yoyote kwa ajili yake….*

*Jifunzeni, marafiki zangu, kumwona Mungu kuwa mkali katika uadilifu wake kana kwamba hana upendo, na bado ni mwenye upendo kana kwamba si mkali. Upendo wake haupunguzi haki yake, wala haki yake hata katika kiwango kidogo, haileti ukinzani juu ya upendo wake. Mambo hayo mawili yameunganishwa pamoja kwa uzuri katika upatanisho wa Kristo. Lakini, zingatia, hatuwezi kamwe kuelewa utimilifu wa upatanisho hadi tuwe tumefahamu kwanza ukweli wa Kimaandiko wa haki kuu ya Mungu.*

*Kamwe hapakuwa na neno baya lililonenwa, wala mawazo mabaya yaliyofikiriwa, wala tendo ovu lililofanywa, ambalo Mungu hatapata adhabu kutoka kwa mtu fulani au mwingine. Atapata kuridhika kutoka kwako, ama sivyo kutoka kwa Kristo. Ikiwa huna upatanisho wa kuleta kwa njia ya Kristo, ni lazima uongoze daima kulipa deni*

---

[17] William Lane Craig, atonement and the Death of Christ, (Baylor University Press, 2020), page 195

*ambalo huwezi kulipa, katika taabu ya milele; kwani hakika Mungu ni Mungu, ni rahisi kupoteza Uungu Wake kuliko kuiacha dhambi moja kwenda bila kuadhibiwa, au chembe moja ya uasi bila kulipizwa kisasi. Unaweza kusema kwamba tabia hii ya Mungu ni mbaya, kali, na ya kikatili. Siwezi kusaidia kuhusiana na unachosema juu yake; hata hivyo ni kweli. Huyo ndiye Mungu wa Biblia.*[18]

Maneno *ukali, katili* na *yasiyobadilika* kwa kawaida hayahusiani na neno upendo. Spurgeon anatualika katika mchakato wa fumbo na vipingamizi hivi vya kimantiki kwa kupendekeza kwamba haki yake inaonekana kana kwamba Yeye si mwenye upendo na wakati huo huo anapenda kana kwamba hakuwa mkali. Ili kukubali kanuni hizi zinazokinzana, lazima ujisalimishe kwenye wazo la fumbo. Unalazimika kuachana na mchakato wako wa kimantiki na ukubali mzozo huo kama kizuizi cha akili yako. Tunakumbushwa kwamba Paulo anatuagiza tujaribu mambo yote (1 Wathesalonike 5:21) na kwa hiyo hatutakiwi kuacha mantiki kwa ajili ya fumbo wakati Biblia haisemi hivyo waziwazi.

> *Je, Biblia inaunga mkono wazo hili la haki isiyobadilika-badilika ambayo lazima iadhibiwe na kwamba Mungu amekusudia sana kuwa na haki hiyo hivi kwamba Angemwadhibu Mwanaye wenyewe ili aridhike?*

Ingawa liko nje ya upeo wa kitabu hiki, matumizi hayo ya kimafumbo ya mantiki hupata ukubali kwa mtu ambaye tayari amekubali ukinzani wa kimantiki wa Utatu. Kukubali kwamba watu watatu wana uwezo wote kwa wakati mmoja na bado wao si watu watatu wenye uwezo wote lakini mtu mmoja mwenye uwezo wote kunahitaji ukinzani wa kimantiki uliowekwa upya kama fumbo ambalo lazima likubalike. Kama tulivyosema hapo awali, fundisho la Mbadala wa Adhabu linakaa kwa urahisi zaidi

[18] Charles Spurgeon, Particular Redemption

katika kifua cha Utatu na inaweza kuonekana kwamba kipengele hicho cha fumbo katika zote mbili kinatumika kushinikiza akili ya kimantiki katika utii. Ulazimishaji kama huo unapaswa kuzua shaka iwapo njia ya ukweli inatuhitaji tutembee katika mwelekeo huu.

Je, taswira ya yule ambaye ni rahisi kwake kupoteza taji yake ya kimungu kuliko kuacha dhambi moja iende bila kuadhibiwa inakufanya ujisikie kuwepo katika uwepo Wake? Kwamba kosa lolote, hata liwe dogo jinsi gani, linahitaji damu? Je, Baba yetu wa mbinguni anatenda kwa njia hii? Je, hii kweli ni tabia Yake? Je, Biblia inaunga mkono wazo hili la haki isiyobadilika-badilika ambayo lazima iadhibiwe na kwamba Mungu amekusudia sana kuwa na haki hiyo hivi kwamba Angemwadhibu Mwanaye mwenyewe ili aridhike?

Kuna sauti nyingi zinazolia "Hapana" kwa wazo hili la adhabu, lakini inaonekana kuna wachache wanaohoji kanuni za mfumo wa haki unaohitaji adhabu hii. Badala ya kuchimba ndani zaidi kile ambacho Maandiko yanakisema na kumwuliza Mungu kama hivi ndivyo Yeye alivyo, watu wengi wanaochukizwa na dhana hii ya upatanisho huacha Ukristo na kuiacha imani.

Lakini je, hizi nadharia kali za upatanisho zinatoka kwa Mungu, au zinatoka kwa mwanadamu?

Je, inawezekana kwamba kutokana na ukweli kwamba hakuna kanuni iliyo wazi ya upatanisho ambayo imesimama peke yake ndani ya fikira za Kikristo kwamba ubinadamu umetengeneza upatanisho kupitia mitazamo yake wenyewe ya haki iliyorithiwa kutoka kwa Adamu na kuvuviwa na yule mwovu? Je, nabii wa injili hakutabiri juu ya tukio hili?

> *Hakika alichukua uchungu wetu na kuyachukua mateso yetu, lakini tulimwona kuwa ameadhibiwa na Mungu, amepigwa na yeye na kuteswa. Isaya 53:4 ( NIV)*

Je, tunaweza kuwazia kwamba Mungu alimwadhibu Mwanaye ili kukidhi haki yake ya kimungu wakati kwa hakika sisi ndio tuliomwadhibu?

*Sisi sote kama kondoo tumetanga-tanga, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, na BWANA ameleta juu yake, adhabu yetu sisi sote. Isaya 53:6 (YLT)*

Wakati King James anatafsiri Isaya 53:6 kama Mungu akiweka juu ya Mwanaye maovu yetu sisi sote, Tafsiri ya Young's Literal inatoa ufahamu katika mtazamo mwingine. Je, ni Mungu aliyedai malipo au ni mwanadamu? Je, Mungu aliruhusu tamaa yetu ya adhabu kukutana na Mwanaye ili tuweze kuona asili yetu mbaya ya kweli ikitenda kazi? Je! ni Mungu aliyemhukumu mwanadamu au ni mwanadamu aliyemhukumu Mungu?

SURA YA 4

# USALITI ULIOFICHWA WA ADAMU

Katika kuzungumza juu ya Baba Yake, Yesu anaonyesha kauli ya ulimwengu wote bila mipaka au kizuizi.

> *"Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote;" Yohana 5:22*

Neno hakimu hubeba maana ifuatayo kama inavyoonyeshwa katika Strong's Concordance:

> *Kutofautisha ipasavyo, yaani, kuamua (kiakili au kimahakama); kwa maana ya kujaribu, kuhukumu, kuadhibu:—kulipiza kisasi, kuhitimisha, kulaani, kulaani, kuamuru, kuamua, kuthamini, kuhukumu, kwenda (kushtaki kwenye) sheria, kuamuru, kuita katika swali, hukumu kwa, kufikiria.*

Yesu anatuambia kwamba Mungu haamui ama kiakili au kihukumu kujaribu, kulaani au kumwadhibu mtu yeyote. Hakuna mtu katika ulimwengu wote ambaye anamjua Baba kuliko Yesu; kwa hakika, Yesu anatuambia kwamba anamjua Baba kwa kiwango sawa na vile ambavyo Baba anamjua Yeye.

*"Kama vile Baba anijuavyo mimi, vivyo hivyo nami namjua Baba…" Yohana 10:15*

Je, ingewezekanaje kwa Baba asimhukumu mtu yeyote? Kuna mistari mingi ya Biblia inayoonekana kupingana na yale aliyosema Yesu. Katika kutafuta kusuluhisha hili akilini mwangu hapo awali, nilihitimisha kwamba Yesu Mwenyewe ndiye atakayewahukumu na kuwaadhibu wale wanaoipinga injili. Lakini kisha tunagundua kauli nyingine ya hukumu kutoka kwa Yesu sura chache baadaye.

*"Ninyi mwahukumu kwa kufuata mambo ya mwili; mimi simhukumu mtu." Yohana 8:15*

Hili ndilo neno lile lile la hakimu kama tulivyopata katika Yohana 5:22. Yesu anatuambia waziwazi kwamba yeye hahukumu au kumwadhibu mtu yeyote. Nilipochambua kwa mara ya kwanza ukweli wa maandishi haya mawili yalichokuwa yanakisema, nilipata hali mbaya ya utambuzi. Ikiwa Mungu hamhukumu mtu yeyote na hata Mwanawe hamhukumu, basi hukumu inafanyaje kazi na uovu unashughulikiwa vipi? Inaonekana haiwezekani kabisa kutafsiri mistari hii kumaanisha Mungu na Mwanawe hawahukumu au kumwadhibu mtu yeyote hata kidogo.

Mistari ifuatayo inatufungulia dirisha la ukweli mpya kabisa tunapowazia hukumu na adhabu.[19]

*"Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi.* ***Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa;*** *na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa.' Mathayo 7:1-2*

*[Upendo] hauvunji heshima kwa wengine, hautafuti ubinafsi, haukasiriki upesi, hautunzi kumbukumbu ya makosa. 1 Wakorintho 13:5 ( NIV)*

[19]Kwa maelezo ya kutosha juu ya sura hii angalia kitabu AS YOU JUDGE kinachopatikana katika fatheroflove.info

> *Na mtu akiyasikia maneno yangu, asiyashike,* ***mimi simhukumu; maana sikuja ili niuhukumu ulimwengu,*** *ila niuokoe ulimwengu. Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye;* ***neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*** *Yohana 12:47-48*

Mtume Paulo anatufunulia hukumu inatoka wapi na ilianzia wapi hapa duniani.

> *Wala kadiri ya yule mtu mmoja aliyefanya dhambi si kadiri ya kile kipawa; kwa maana hukumu ilikuja kwa njia ya [ilitoka kwa] mtu mmoja [Adamu] ikaleta adhabu; bali karama ya neema ilikuja kwa ajili ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki. Warumi 5:16 (KJV).*

Tukiitazama Warumi sura ya tano kwa makini, inafunua kwamba hukumu inatoka kwa Adamu na si kwa Mungu.

| **Warumi 5** | **Matendo ya Mwanadamu na matokeo** | **Matendo ya Mungu na matokeo** |
|---|---|---|
| Fungu 15 | Lakini haikuwa kama lile kosa ... | .. vivyo hivyo na karama |
| Fungu 15 | Kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake mmoja wengi walikufa... | ... Zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika neema yake Mwanadamu mmoja Yesu Kristo kimezidi kwa ajili ya wengi. |
| Fungu 16 | Wala kadiri ya Yule mmoja aliyefanya dhambi, .... | *... si kadiri ya kile kipawa*: |
| Fungu 16 | ... kwa maana hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhabu | ... Bali karama ya neema ilikuja kwa ajili ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki. |
| Fungu 17 | Ikiwa kwa kukosa kwake mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja; ... | ... Zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki watatawala katika uzima kwa Yule mmoja, Yesu Kristo. |
| Fungu 18 | Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu ... | ... Kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. |
| Fungu 19 | Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, ... | ... Kadhalika kwa kutii kwake mtu mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki. |
| Fungu 20 | Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana ... | ... Na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi: |
| Fungu 21 | Ili kwamba kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, ... | ... Vivyo hivyo kwa njia ya haki neema itawale hata uzima wa milele kwa Kristo Bwana wetu. |

Tafsiri nyingi hutafuta kuwasilisha wazo la kwamba Adamu alijiletea hukumu ya Mungu juu yake mwenyewe kupitia matendo yake lakini usomaji sahihi wa kifungu unaonyesha kwamba Adamu ndiye aliyehukumu. Na ni nani aliyemhukumu?

> *Adamu akasema, Huyo mwanamke* ***uliyenipa awe pamoja nami*** *ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Mwanzo 3:12*

Kama vile ambavyo hakuna mtu anayekuja kwa Baba isipokuwa kupitia kwa Mwana, ndivyo Mwana wa Mungu alivyokuja kwa Adamu kwenye bustani na kumuuliza amefanya nini. Adamu alikuwa amekimbia kutoka mbele za Mungu akiogopa kwamba angeadhibiwa kwa kula tunda hilo. Adamu alifikiria kwamba kwa sababu Mungu alisema utakapokula tunda hilo utakufa, hiyo ilimaanisha kwamba Mungu alikuwa anakuja kumuua. Kwa kuamini kwamba Mungu alikuwa amemhukumu na kumlaani, Adamu analipiza kisasi na kumlaumu Mungu katika utu wa Mwana Wake kwa ajili ya matukio ambayo yalikuwa yametukia. Adamu alifikiri kwamba angekufa, alijaribu kuhamisha kile alichofikiri kuwa ni kuuawa kiangukie kwa Mwana wa Mungu na kwa mke wake.

Aya tuliyosoma hivi punde inatuletea kielelezo cha upatanisho wa kibinadamu. Adamu alimhukumu Hawa, ambaye alikuwa na hatia, kwa sehemu yake ya kumletea Adamu tunda. Lakini Adamu basi alimhukumu asiye na hatia, Mwana wa Mungu. Hapa kuna kuzaliwa kwa Mbadala wa Adhabu ndani ya jamii ya wanadamu. Udhihirisho kamili wa upatanisho huu unaonekana Msalabani. Watu wawili kando ya Kristo walikuwa na hatia kama Hawa, lakini katikati palikuwa na kusulubishwa kwa asiye na hatia. Hili ndilo wazo lililoongozwa na roho ya kishetani ambalo Shetani alikuwa nalo muda wote la kumwua Mwana wa Mungu. Kama tutakavyogundua katika sura zinazofuata, upatanisho wa kibinadamu kwa kawaida huhitaji kifo cha wasio na hatia pamoja na mwakilishi wa wenye hatia. Hii ndiyo dhambi iliyofichwa ndani kabisa ya moyo wa Adamu.

> *Ikiwa nimeyafunika makosa yangu kama Adamu, Kwa kuuficha uovu wangu kifuani mwangu. Ayubu 31:33*

Simulizi ya Mwanzo haionyeshi tamanio la Adamu la kuweka hukumu ya kifo juu ya Mwana wa Mungu na mke wake, ingawa ni wazi kwamba Adamu anataka kuwalaumu wote. Tunaona ushahidi wa uzao ndani ya Adamu wa kumlaumu mkewe katika wanawake 137 wanaouawa kila siku na wenzi wao wa kiume.[20]

Nabii Hosea anatuambia uovu wa Adamu ulivyokuwa.

> *Nao Kama vile Adamu walikiuka agano, ndipo waliponitenda kwa hiana. Hosea 6:7 (YLT).*

Neno la hiana lina anuwai ya maana zifuatazo katika Kiebrania:

> *H898 Bâgad: Mzizi wa awali; kufunika (na vazi); kwa njia ya mfano kutenda kwa siri; kwa maana ya kupora: - tenda kwa hila (kwa hiana, bila uaminifu), chukiza, ukiukaji (-au), (ondoka), msaliti (mchuuzi, -ly, mwanadamu), asiye mwaminifu (-ly, mtu), X sana.*

Adamu alivunja agano la milele na Mungu. Alitenda kwa hiana kwa Mungu lakini aliuficha usaliti huu wa uuaji ndani kabisa ya moyo wake. Kufunikwa kwa majani ya mtini kulikuwa ishara ya jaribio lake la kufunika kitu kibaya zaidi kuliko kujisikia vibaya kwa kula tunda la mti huo.

Adamu hakujua kabisa hisia zake kwa Mungu, na pili, mke wake. Kwa jinsi zilivyofichwa, zisingejulikana kweli mpaka zidhihirike. Mungu alitaka kumwonyesha Adamu ukubwa wa hila yake kwa kuruhusu mmoja wa wanyama Wake wa thamani atolewe dhabihu. Mungu hakutamani kufanya hivi (Zaburi 40:6) lakini ilikuwa ni hatua ya dharura iliyokithiri kumtahadharisha Adamu juu ya uovu wa kutisha uliokuwa umefichwa ndani. Dhabihu ilikuwa kioo ndani ya kifua cha Adamu; ilikusudiwa kumwonyesha nia yake ya kweli dhidi ya Mwana wa Mungu.

[20] https://www.bbc.com/news/world-46292919

*Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi; Warumi 5:12*

Mstari huu unaeleweka kwa Wakristo kumaanisha kwamba kifo kilipitia kwa Adamu, na kwa hiyo watu wote, kwa sababu Mungu alihumkumu na kumwadhibu Adamu kwa kula matunda ya mti huo. Ukweli ni kwamba Adamu alidhani kwamba Mungu angemhukumu na kumuua. Yesu anatuambia kwamba Yeye wala Baba yake hawahukumu mtu yeyote. Kwa hiyo, Adamu alitenda dhambi dhidi ya ukweli wa tabia ya Mungu. Mungu alimwambia Adamu angeangamia kwa kuchagua njia ambayo ilitilia shaka upendo wa Mungu, kwani hii ingemtenganisha Adamu na chanzo. Dhambi ya Adamu ya kutaka kubadili kile alichoelewa ni adhabu kwa Mwana wa Mungu, badala ya kushikilia tumaini la wema wa Mungu, ilisababisha kifo kije ulimwenguni. Njia hii ya kufikiria imepita kwa kila mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu:

***Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui** tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake,.....Warumi 5:10*

*Na ninyi, mliokuwa **hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu**, kwa matendo yenu mabaya...Wakolosai 1:21*

Adamu alimhukumu Mwana wa Mungu (asiye na hatia) na mkewe (mwenye hatia) kifo wakiwa wameketi kwenye kiti cha enzi cha hukumu cha Shetani.
Dhambi ya Adamu ilidhihirishwaje? Kaini alipomuua Habili.

Tunda la mwili wa Adamu halingeweza kufichwa. Kaini alichukuliwa mimba katika hali ya awali ya dhambi ya Adamu. Uovu uliokuwa kifuani mwake ulidhihirishwa katika maisha ya Kaini. Kile ambacho hakikuonekana kwa Adamu kilionekana kwa Kaini. Habili alijazwa na Roho wa Kristo na kuakisi tunda la toba ya Adamu iliyokua, huku Kaini akiendelea kukuza asili ya kimwili ya baba yake kupitia kukataa kwake kutubu.

Tunaona kwamba Paulo hasemi *kwa mwanamke mmoja dhambi iliingia ulimwenguni*; ilikuja kupitia kwa Adamu sio Hawa. Wakati Hawa alipokula tunda, alidanganywa na nyoka. (1 Timotheo 2:14). Adamu kwa makusudi alichukua tunda na akapanda uadui(chuki) wa mtu wa kimwili. (Warumi 8:7).

Uovu uliofichika wa Adamu ulikuwa uadui/chuki dhidi ya Mungu. Ili kuficha uadui huu, Adamu alidhihirisha hukumu yake iliyofichika ya kuhukumu kwa Mungu. Kwa Adamu, ilionekana kwamba Mungu alitaka kumuua, badala ya yeye kutaka kumuua Mungu. Huu ni mchakato unaotambulika kisaikolojia ambao wanadamu walioanguka hutumia kupotosha na kukandamiza mawazo na hisia zisizohitajika.

> *Uelekezaji wa kisaikolojia ni utaratibu wa kujilinda ambapo nafsi ya mwanadamu hujilinda dhidi ya msukumo au sifa zisizo na fahamu (zote chanya na hasi) kwa kukataa uwepo wa hisia hizo ndani yao wenyewe huku ukizihusisha na wengine*.[21]

Ikiwa tunaelewa mchakato huu kwa usahihi, fundisho la Mbadala wa Adhabu ni tunda lililokuzwa kikamilifu la mwanadamu kuelekeza ghadhabu yake ya kuhukumu kwa Mungu. Adamu ndiye aliyekuwa mchokozi huku Mwana wa Mungu kwa upole alichukua mapigo yaliyowekwa juu Yake, si mapigo ya adhabu ya Mungu bali ya wanadamu.

Hukumu ya adhabu inayodai kifo kuma inavyotoka kwa mwanadamu badala ya Mungu pengine litakuwa wazo geni kwa msomaji. Ikiwa dhambi ni ya udanganyifu na imefichwa, hii haipaswi kukushangaza. Ikiwa dhambi ingeshughulikiwa kwa urahisi sana, wanadamu wangekuwa na upatanisho na Mungu zamani sana. Hatimaye, baada ya takriban milenia sita iliyojaa damu, Roho wa Mungu akifika ndani ya mioyo ya wanadamu hatimaye anaweza kutuonyesha kile ambacho kweli kinatendeka ndani yetu. Hatungeweza kamwe kugundua hili sisi wenyewe. Tumejidanganya

[21] https://en.wikipedia.org/wiki/Psychological_projection

sana kutambua hilo. Lakini sasa ujumbe huu unatuita kutubu usaliti wetu tuliorithi na uliokuzwa dhidi ya Mungu na Mwanawe.

Hebu tuweke wazi. Hofu ya Adamu kwa Mungu, ambayo wanadamu wote wamerithi kwa sababu ya dhambi, ilisababisha ndani yetu kiwewe kibaya kiakili. Katika kujilinda, mwanadamu anaweka dhambi yake iliyofichwa kwenye tabia ya Mungu na kumfanya Mungu kuwa mwenye kasoro ya tabia. Hili hutufanya tuamini upatanisho hufanyika kwa hitaji la Mungu la damu, wakati kwa kweli ni hitaji letu la damu.

Ikiwa huu ndio ukweli, basi inafuata kwamba upatanisho kwa mwanadamu unapatikana katika mambo mawili.

1. Ufahamu uliorejeshwa wa tabia ya Mungu.

2. Ufahamu wa kweli wa tabia mbaya ya mwanadamu ya kuhukumu ambayo inaongoza kwenye toba katika nuru ya ukweli wa tabia ya Mungu.

SURA YA 5

# NIMEKUTUKUZA DUNIANI

Maneno ya Yesu kwa Filipo ni ya kina na rahisi katika kujibu swali lake la kumwonyesha Baba.

> *Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Yohana 14:8-9*

Yesu anamhakikishia Filipo kwamba ndani ya muda ambao alikuwa amemjua Kristo, tabia ya Baba ilifunuliwa kwake kikamilifu. Yesu hakuzuia chochote bali ukuu wote wa tabia tukufu ya Mungu ulifunuliwa kwake. Kwa hivyo Yesu aliweza kuomba hivi usiku kabla ya kusulubishwa kwake:

> *"Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika." Yohana 17:6*

Neno jina katika Kigiriki hapa linazungumzia tabia. Yesu hakuwafundisha tu wanafunzi jinsi ya kutamka jina la Baba, hapana,

aliwafunulia tabia ya Baba yake kwa sababu hii ndiyo iliyohitajika ili kuanzisha sehemu ya kwanza ya upatanisho.
Maisha ya Yesu yaliyoandikwa katika Injili nne za Agano Jipya yanafunua mtu ambaye ni mzuri sana. Daima kufikiria wengine, kuonyesha huruma, rehema na wema. Imara katika imani; daima kusema ukweli. Bila woga mbele ya dhoruba za wanadamu na asili huku akisamehe kabisa udhaifu wa watu. Mtazamo wake wa upendo kwa Petro, hata wakati Petro alipokuwa akilaani kwa kukana kumjua, hutuacha katika mshangao wa vipengele vya thamani vya tabia yake.

Katika matukio mawili Yesu alisafisha hekalu akifunua ukubwa wa uaminifu-mshikamanifu kwa ibada Yake kwa Baba Yake, lakini Hakuwahi kumpiga mtu yeyote kwa tendo la jeuri wala Hakumwua mtu kamwe. Ukweli huu unahitaji kupata fursa ya kuingia ndani ya mioyo na akili zetu. Hii ni njia nyembamba sana ya kuipita, kwa sababu tukikubali ukweli ulio wazi kwamba Kristo hakuwahi kuua mtu yeyote akiwa hapa duniani, na tukikubali maneno yake kwamba kile alichoonyesha kwa kweli ni tabia yenyewe ya Baba yake, basi tunaachwa bila udhuru wowote wa tabia zetu za kulaani na za jeuri ambazo zinajaribiwa kuona adhabu na hata kifo kikiwapata wale waliotukosea au wale tunaowapenda.

> *Ikiwa Kristo hakuwahi kudhihirisha haki iliyomfanya aue mtu yeyote hapa duniani, basi haiwezekani kufikiria kwamba Baba yake angefanya hivi.*

Ikiwa unaweza kuona kwamba maisha ya Kristo duniani ni udhihirisho kamili wa tabia ya Mungu, basi hii inaathiri moja kwa moja uelewa wako wa upatanisho. Ikiwa Kristo hakuwahi kudhihirisha haki iliyomfanya aue mtu yeyote hapa duniani, basi haiwezekani kufikiria kwamba Baba yake angefanya hivi. Mawazo haya yanazua maswali mengi nje ya upeo wa kitabu hiki. Kwa utangulizi wa somo la tabia ya Mungu isiyo na jeuri tafadhali soma

kitabu cha Acts of our Gentle God kinachopatikana katika fatheroflove.info. Kwa uchambuzi wa kina wa somo hili tafadhali soma kitabu cha Agape kinachopatikana pia katika *fatheroflove.info.*

Ikiwa katika kiini cha upatanisho Mungu anatafuta kumfunulia mwanadamu ukweli wa tabia yake ya upendo kupitia kwa Mwanawe, basi tunaweza kupata nuru safi ya ukuu katika maombi ya Yesu usiku uliotangulia kifo Chake.

> *"Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye." Yohana 17:4*

Nguzo kuu ya Mbadala wa Adhabu ni kwamba adhabu tuliyostahili iliwekwa kwa Kristo katika mateso na kifo chake. Hii inatangazwa, na fundisho hilo, kuwa kazi kuu ambayo Kristo alikuja kuifanya. Kristo anaharibu nguzo hii kwa ombi rahisi kwamba alikuwa amekamilisha kazi ambayo Baba yake alimpa usiku kabla ya kifo chake.

Kristo alimtukuza Baba yake katika ufunuo alioutoa wa tabia yake. Kazi hii ilikamilika kabla Kristo hajafa Msalabani. Ni kweli kwamba katika sala ya Yesu ya kuwasamehe wale waliokuwa wanamuua ilitolewa alama ya mshangao mtukufu kwa uzuri wa tabia ya Mungu, lakini Yesu anasisitiza kwamba kazi hii ilikuwa tayari imekamilika usiku uliopita.

Kristo alipojitoa kikamilifu kwa mapenzi ya Baba yake na kujitoa kumwokoa mwanadamu kwa gharama yoyote, alidhihirisha upendo wa Baba yake kikamilifu. Kusulubishwa kwa Kristo kulikuwa muhimu kwa misingi ambayo wanadamu walihitaji kuona ukifunuliwa ule uovu uliokuwa umefichwa ndani ya Adamu na kurithiwa na wazao wake wote. Tulihitaji kuona Msalaba ili kuona jinsi tulivyo viumbe wa kutisha, na kukiri wenyewe hatia ya mauaji ya Mwana wa Mungu.

> *"Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa*

*ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza." Zekaria 12:10*

Kila wakati tunapohisi hasira ndani yetu tukitamani madhara kwa mtu mwingine, tuna hatia ya damu ya Kristo. Yohana anatuambia kwamba anayemchukia ndugu yake ni muuaji. ( 1 Yohana 3:15 ). Kristo anatuambia kwamba kwa kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mmenitendea Mimi. (Mathayo 25:40).

Unapochunguza maneno ya Yesu katika Injili ili kugundua ufafanuzi wake wa Msalaba, unapata tu maneno haya:

*Akawaambia wote, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate." Luka 9:23*

Yesu anafafanua Msalaba kama kujinyima kila siku. Kupigiliwa misumari kwa Yesu kwenye msalaba wa mbao lilikuwa dhihirisho kuu la kujikana kwake, lakini hili pekee sio Msalaba wa kweli. Msalaba wa kweli wa Kristo unajumuisha kujikana kwake katika historia yote ya mwanadamu.[22]

*Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale. Isaya 63:9*

Kila siku Kristo anateseka kwa mateso ya kusulubiwa; kila siku watu wanamchoma kwa maneno yao ya kulaani na matendo yao ya jeuri. Kama vile ambavyo mzazi yeyote angejeruhiwa sana kwa kulazimishwa kutazama mateso na kifo cha watoto wake, ndivyo Kristo, kwa kiwango kikubwa zaidi, anateseka na kuchomwa katika kutazama watoto wake wakiumizana na kuangamizana wao kwa wao.

---

[22]Kwa uchunguzi zaidi juu ya mada hii tazama kitabu Cross Examined and Cross Encountered kinachopatikana katika fatheroflove.info

> *Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu;* ***kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao****, na kumfedhehi kwa dhahiri. Waebrania 6:6*

Paulo alielewa ukweli huu aliposema "Nimesulubishwa pamoja na Kristo." (Wagalatia 2:20, KJV). Hakusema alisulubishwa kama Kristo, akimaanisha tukio moja huko nyuma, bali na Kristo kama alivyotangaza "Nakufa kila siku." (1Wakorintho 15:31 ).

Wengi wanapiga kelele katika giza la usiku "Uko wapi wewe Mungu katika saa yangu ya uhitaji!" Ukweli ni kwamba Yeye yuko pale pale gizani akiteseka katika kila kitu unachokihisi, akitumaini kwamba utamgeukia na kumwamini ili akusaidie kupitia bonde lako la kukata tamaa. Pasipo imani haiwezekani kwake kuingia katika gereza letu la vivuli linalotawaliwa na nguvu za giza. Ni lazima tuwe watu wa kumwalika kwa imani kuleta nuru yake ili kutusaidia.

Ulimwengu wa Kikristo umepofushwa kuhusiana na Msalaba wa kweli wa Kristo kwa mbao za msalaba na miiba ya Kalvari. Inashangaza kwamba ubinadamu katika hekima yake ya kishetani unaweza kuchukua nembo ya nuru safi na bado kuitumia kuficha ukuu wa kweli wa Msalaba. Msalaba wa kweli unaang'aa sana kwa ubinadamu kuuthamini. Kujikana nafsi kwa Mungu kwa zaidi ya miaka 6000 ni kukubwa sana kuelewa. Upendo huu unashutumu kabisa ubinafsi wetu lakini hautokani na uso wa uungu wenye kukunjamana bali ni mwonekano mwororo wa upendo wenye subira. Baba yetu hurundika makaa ya moto yenye upendo juu ya vichwa vya wenye hatia, ili wenye hatia waone ukweli wa tabia yake (Warumi 12:20); si kwa ajili ya kuwadhuru au kuwaangamiza.

Je, tunaamini maneno ya Yesu kwamba Alimaliza kazi ya Baba Yake usiku uliotangulia kufa kwake? Ukifanya hivyo ni lazima ubadilishe kwa kiasi kikubwa mitazamo yako ya upatanisho, kwa kuwa Baba yetu mwema hakutamani kamwe dhabihu au kafara kwa ajili ya dhambi. ( Zaburi 40:6 ). Sisi ndio tuliotamani hivyo, kupitia urithi wa laana wa mababu zetu hadi kwa Adamu.

SURA YA 6

# KITI CHA UOVU

Katika kuzungumza na viongozi wa taifa la Kiyahudi, Yesu anazungumza ukweli wa ndani zaidi wa mtu wa mwilini:

> *"Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo." Yohana 8:44*

Kwa asili, mwanadamu aliyeanguka ana asili ya inayotokana na Shetani. Misukumo yetu ya asili hutimiza matamanio ya Shetani. Paulo anathibitisha ukweli huu anaposema:

> *…ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga,* ***roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi****; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa* ***tabia yetu watoto wa hasira*** *kama na hao wengine. Waefeso 2:2-3*

Shetani alikuwa muuaji tangu mwanzo. Alitamani kuabudiwa kama Baba, wakati huo huo akichukua nafasi ya Mwana wa Mungu. (Isaya 14:12-14). Shetani alifanya kazi kwa usiri, baba wa kweli wa sanaa

zote za udanganyifu, akitafuta kuangusha utawala wa Mwana wa Mungu.

Kutokana na ukweli kwamba wanadamu wa kimwili huakisi tamaa za Shetani tunaweza kugundua kupitia hadithi za Biblia, njia za Shetani za utendaji katika vita vyake na serikali ya mbinguni zikithibitisha kuwa kweli maneno ya Paulo kwamba "Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani. (1 wakorintho 10:11, KJV).

Kisa cha Absalomu katika kukitafuta kiti cha enzi cha baba yake, hata kufikia kiwango cha kumuua, kinaakisi kabisa tamaa ya baba yake Ibilisi. Ni somo gani ambalo Absalomu alianzisha katika nyua za milki ya baba yake?

> *Tena Absalomu huondoka asubuhi na mapema, na kusimama kando ya njia ya lango; kisha ikawa, mtu ye yote aliyekuwa na neno, lililokuwa halina budi kufika kwa mfalme ili kuhukumiwa, Absalomu humwita mtu huyo kwake, na kumwuliza, Wewe u mtu wa mji gani? Naye akasema, Mtumwa wako ni mtu wa kabila fulani ya Israeli. Naye Absalomu humwambia, Tazama, maneno yako ni mema yenye haki; lakini hapana mtu aliyeagizwa na mfalme kukusikiliza. Tena Absalomu husema,* ***Laiti mimi ningewekwa kuwa mwamuzi katika nchi hii, ili kila mtu mwenye neno au daawa aje kwangu, nimpatie haki yake!*** *Tena ikawa hapo alipokaribia mtu ye yote kumsujudia, hunyosha mkono wake, na kumshika, na kumbusu. Hivyo ndivyo Absalomu alivyowatendea Israeli wote, waliomwendea mfalme ili wapate hukumu; na hivyo Absalomu akawadanganya watu wa Israeli. 2 Samweli 15:2-6*

Kitu ambacho Absalomu alikitumia kuingia ndani ya mioyo ya taifa na kukifikia kiti cha ufalme kiliitwa Haki. Jina Absalomu maana yake ni baba wa amani, lakini siri iliyo chini ya jina hili ilikuwa tabia ya chuki na vita. Absalomu alitaka baba yake amwadhibu Amnoni, kaka yake wa kambo, ambaye alimnyanyasa kingono dada ya Absalomu, Tamari. Kwa sababu mfalme Daudi hakutekeleza hukumu dhidi ya

Amnoni kulingana na matakwa ya Absalomu, Absalomu alimdharau baba yake na akaazimia kushughulika na Amnoni mwenyewe.

> *Mfalme akamwambia, Kwa nini aende nawe? Lakini Absalomu akamsihi sana, naye akamwacha Amnoni na wana wote wa mfalme waende naye. Kisha Absalomu akawaamuru watumishi wake, akasema, Angalieni basi, moyo wake Amnoni utakapofurahiwa kwa mvinyo;* ***nami nitakapowaambia, Mpigeni Amnoni, ndipo mwueni, msiogope; si mimi niliyewaamuru? Iweni hodari, iweni na ujasiri.*** *Basi watumishi wa Absalomu wakamfanyia Amnoni kama alivyoamuru Absalomu. Ndipo wakaondoka wana wote wa mfalme, wakapanda kila mtu nyumbu wake, wakakimbia. 2 Samweli 13:27-29*

Absalomu alimuua Amnoni kwa haki aliyoona inafaa. Haielekei sana kwamba tamaa ya Absalomu ya kulipiza kisasi ilitegemea tu kulipiza kisasi kwa dada yake. Amnoni alikuwa mwana mzaliwa wa kwanza wa Daudi na kwa hiyo alikuwa wa kwanza katika mstari wa kiti cha enzi. Mwana wa pili wa Daudi Danieli au Chileab inaonekana kutoweka katika historia na kusababisha wengine kufikiri kwamba alikufa akiwa mtoto.

Matarajio ya Absalomu ya kiti cha enzi yalikuwa nia ya ndani zaidi. Ingawa sasa alikuwa karibu na kiti cha enzi, hofu yake kwamba anaweza kutengwa kwa sababu ya kisasi chake, pamoja na tamaa yake ya mamlaka ilimsukuma kutwaa kiti cha enzi kwa nguvu. Ili kufikia lengo hili alijiwekea lengo la kuteka mioyo ya ufalme wa Israeli kama vile Shetani alivyofanya kati ya malaika wa mbinguni, akitafuta kuwavuta upande wake ili kutwaa kiti cha enzi cha Mungu kwa nguvu.

Daudi alihuzunika juu ya kile mwanawe Amnoni alichomfanyia binti yake lakini hakuwa na wazo lolote la kumuua. Kushindwa kwa Daudi mwenyewe kimaadili na Bathsheba kulifunika hitaji la Daudi la kuchukua hatua. Hapo awali Daudi alikuwa ametoa haki ya kweli ndani ya milki yake (2 Samweli 8:15), lakini kutotenda kwa Daudi kulimchochea Absalomu kuchukua hatua yake mwenyewe.

Baada ya Absalomu kumuua Amnoni, Daudi alimfukuza kutoka katika mji mkuu hadi hatimaye, kupitia ombi la Yoabu, jemadari wake, Absalomu akarudi.

Baada ya kurejea, somo ambalo Absalomu alianzisha kwenye akili za watu wa taifa lilikuwa somo la haki na usimamizi wa sheria. Uchochezi kwake kwa somo hili kuliweka shaka juu ya usimamizi wa Mfalme Daudi wa serikali ya Israeli. Kiti cha enzi cha Absalomu kilitengenezwa kwa kufanya upotovu wa sheria.

> *Je! Kiti cha udhalimu kitashirikiana nawe, atungaye madhara kwa sheria? Zaburi 94:20 (KJV).*

Mauaji ya Absalomu kwa Amnoni yanaonyesha asili ya kutokuwa na huruma ya mawazo yake juu ya haki. Aliachanisha kanuni ya rehema na haki, akizifanya kutopatana baina ya kanuni hizi mbili.

Katika njama za Absalomu, tunaona tamaa za baba yake muuaji, Shetani. Alitaka kumwondoa Kristo, Mwana mzaliwa wa kwanza wa Baba na kuchukua nafasi yake. Bila shaka, Mungu hakuwa mzembe kama Daudi ili kusimamia haki katika milki Yake, lakini kushughulika kwa Mungu na hila za Shetani kulihitaji muda ili ukweli ufichuliwe. Kama Absalomu, Shetani alianzisha kwenye ufalme wazo tofauti la haki; haki inayodai adhabu kali na kifo bila msamaha. Shetani alitengeneza sheria ya Mungu kwa udanganyifu kwa namna ya kutenganisha tabia ya Mungu kutoka kwenye utawala na usimamizi Wake; akitengeneza utupu katika akili za viumbe wa mbinguni ambao aliujaza mwenyewe kwa mamlaka yake mwenyewe na wazo la haki, hivyo kuunda kiti cha uovu.

> *…uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na* ***nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao,****....Matendo ya Mitume 26:18 (KJV)*

Paulo anafunua kwamba kutoka katika nguvu za Shetani ni kuja katika uwezekano wa msamaha wa dhambi. Ufalme wa Shetani uliotiwa giza ulijengwa juu ya kutosamehe na adhabu. Mungu

anajidhihirisha kuwa ni mwenye rehema, mwenye neema, na mvumilivu katika tabia. (Kutoka 34:5-6). Tamanio la Mungu ni kuonyesha rehema na ukweli; Shauku ya Shetani ni kuadhibu na kuangamiza.

Sheria ya Mungu ni sheria ya uzima na uhuru. (Yakobo 2:12; Mithali 13:14). Kwa vile Baba ndiye pekee ambaye kwa asili ana hali ya kutokufa na Mwanawe alimiliki hali hii ya kutokufa kwa upendo na heshima ya Baba yake, malaika wengine wote walipewa uzima huu kupitia Mwana wa Mungu, muda baada ya muda.[23]

Lusifa aliifanya sheria iwe kama kanuni ambayo malaika wanapaswa kuitii na kwamba wale wasiotii wanapaswa kuadhibiwa. Hii ndiyo aliyoiita haki. Hii ilikuwa tofauti na haki ya Mungu. Kumbuka kwa makini aya ifuatayo.

> *Haki na hukumu ndio makao ya kiti chako cha enzi: fadhili na kweli zitakutangulia. Zaburi 89:14 (KJV)*

Andiko hili la Biblia ni muundo wa sentensi wa Kiebrania. Sentensi ya pili ni upanuzi wa ile ya kwanza. Inarejelea kanuni za sehemu ya kwanza kwa njia iliyokuzwa. Kando na hili, alama za uandishi wa Kiingereza pia hutoa kanuni hii. Nukta pacha baada ya neno kiti cha enzi humanisha kwamba kinachofuata huelezea kile kilicho kabla ya nukta pacha.

1. Haki na hukumu ndio maskani ya kiti chako cha enzi

   *Ni Sawa na*

2. Rehema na kweli zitakutangulia

[23]Kwa maelezo zaidi juu ya hili tazama kitabu Divine Risk sura ya 1 mpaka 6 kinachopatikana katika fatheroflove.info

Kile ambacho hiki inachokisema ni kwamba haki inaonyeshwa kama rehema na hukumu inaonyeshwa kama ukweli. Haki ya Mungu inamaanisha kufanya lililo sahihi. Kwa Mwenyezi Mungu lililo sahihi ni kurehemu.[24] Wale wanaokataa kutii baada ya maonyo ya mara kwa mara watavuna walichokipanda.

Mungu alipomfunulia Musa jina/tabia yake, hatusomi chochote kuhusu kuua.

> *BWANA akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la BWANA. BWANA akapita mbele yake, akatangaza, BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne. Kutoka 34:5-7*

Je, Mungu alitimiza ombi la Musa na kumfunulia tabia yake yote? Baba yetu mpendwa anataja rehema kama sifa yake ya kwanza ikifuatiwa na fadhili. Kisha anaitaja subira, kuwa na wingi wa wema na ukweli na kuwa mwenye rehema kwa maelfu ya vizazi na mwenye kusamehe uovu na dhambi.

*Baba yetu hataji chochote kuhusu malipo ya dhabihu kwa ajili ya dhambi. Hakuna kutajwa kwa Mbadala wa Adhabu katika kile Alichokisema. Inasema tu kwamba Yeye husamehe*

Baba yetu hataji chochote kuhusu malipo ya dhabihu kwa ajili ya dhambi. Hakuna kutajwa kwa Mbadala wa Adhabu katika kile Alichokisema. Inasema tu kwamba Yeye husamehe.

---

[24]Kwa maelezo zaidi juu ya hili tazama kitabu Divine Risk sura ya 9 mpaka 14 pamoja na kitabu As You Judge sura ya 3 hadi 13 vyote hupatikana katika fatheroflove.info

Mwenyezi Mungu hamhesabii yeyote kuwa mwenye hatia ya makosa kwa sababu neno hatia liliwekwa na wafasiri. Mungu huruhusu kila mtu kupokea matokeo ya matendo yake mwenyewe na atatoa rehema kwa wale wanaoiomba huku wakikabili matokeo yao. Inasema kwamba Mungu huwapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne. Inamaanisha nini kuwapatiliza watoto maovu ya baba zao? Neno hili kwa Kiebrania linamaanisha:

> *(Qal) kuzingatia, kutazama, kuhudumia, kutafuta, kutazama, kutafuta bure, haja, kukosa, kupungukiwa, kutembelea, kupatiliza, kuadhibu kupita katika ukaguzi, kukusanya, namba, kuteua, kukabidhi, kuweka kama malipo, amana - Brown Driver Briggs*

Baba yetu wa mbinguni hutazama na kuona jinsi dhambi za kizazi kimoja zinavyoathiri kizazi kijacho. Ingawa anaendelea kuonya awezavyo juu ya hatari za kuchukua njia ya dhambi, Hawalazimishi watu upande wowote. Mungu hapatilizi tu au kupuuza maovu ya waovu bali pia hufanya hivi kwa wafuasi wa Mungu. Daudi alipofanya uzinzi na kupanga mauaji ya Uria, Mungu hakumwondolea Daudi kifo cha wanawe wanne bali alimpa neema ya kuvumilia matokeo ya uchaguzi wake mbaya.

Biblia inarudia tena na tena kanuni hii ya watu kuadhibiwa na matokeo ya asili ya uchaguzi wao mbaya:

> *BWANA hujulikana kwa hukumu anayoifanya;* ***mtu mbaya amenaswa katika kazi ya mikono yake mwenyewe****. Zaburi 9:16*

> *Tazama, huyu ana utungu wa uovu, Amechukua mimba ya madhara, amezaa uongo. Amechimba shimo, amelichimba chini sana, Akatumbukia katika handaki aliyoifanya!* ***Madhara yake yatamrejea kichwani pake, Na dhuluma yake itamshukia utosini****. Zaburi 7:14-16*

> *Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Wagalatia 6:7-8*

Mungu alifunua tabia yake yote kwa Musa. Hasemi lolote kuhusu kuwaua wale wanaomtenda dhambi. Kanuni hii hii imewekwa katika Amri Kumi ambazo ziliandikwa kwa kidole cha Mungu na kusemwa naye ili watu wote wasikie kwenye Mlima Sinai.

> *"Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu."* *Kutoka 20:3-6*

Kizazi au aina ya watu wanaoamua kumchukia Mungu na njia zake watakabiliana na matokeo ya asili ya makosa yao wenyewe. Kukataa kuja katika ukweli wa neno la Mungu huwaacha wale wanaokataa hili kwa utendaji wa Shetani. Shetani anapoanza kuwadhuru na kuwaangamiza wale wanaompinga Mungu, wale wanaoathiriwa hufikiri kwamba ni Mungu anayewaadhibu kwa wivu. Mungu si mwenye wivu bali Anaonekana kuwa na wivu machoni pa wale wanaotembea katika njia ya uasi. Hivyo, Mungu anatuonya kwamba tukiabudu miungu au mawazo ya uwongo, Ataonekana kuwa na wivu. Neno amin "Mimi… ni Mungu mwenye wivu" liliwekwa na wafasiri na si sehemu ya aya hiyo.

Ni jambo la kuhuzunisha sana kwa Baba yetu kuruhusu watoto wake waasi waende mikononi mwa Shetani na kuangamizwa. Lakini kwa vile Yeye anaheshimu uchaguzi huru wa wote, Hatawazuia wale ambao wameazimia kuasi.

Shetani ndiye mwanzilishi wa hukumu na kifo. Kiti chake cha enzi kimejengwa juu ya kuunda upya sheria ya Mungu katika chombo kinachoongoza kwenye adhabu na kifo.

Kama vile Absalomu alivyoiba mioyo ya Israeli kwa kuhangaikia kwake haki ya kuadhibu, vivyo hivyo Shetani ameudanganya

ulimwengu wote kwa uwongo huo huo. Wakatoliki, Waprotestanti na vikundi vingine vyovyote vinavyorejelea haki ya Mungu kuwa inayodai kifo kwa kweli bila kujua wanadhihirisha haki mbovu ya Shetani kwa Baba mwenye rehema, mpole, na mwenye neema kwa wote walio hai.

Kupitia haki yake ya uwongo, Shetani karibu amefanikisha kile alichokusudia kufanya - kuweka kiti chake cha enzi juu ya nyota za Mungu na wanadamu wote. (Isaya 14:12-14).

Ingawa Mungu hakutaka dhabihu kwa ajili ya dhambi, Shetani aliwasadikisha malaika wengi na jamii yote ya kibinadamu kuhusu kanuni zake za haki. Kwa sababu hii, mpango wa uokoaji wa Mungu kwa wanadamu ulipaswa kuzingatia ukweli kwamba ufahamu wetu wa uongo wa haki, ulioelekezwa kwa Mungu, ulimaanisha kwamba hakuwezi kuwa na msamaha wa dhambi bila kumwaga damu.

Haikuwa na maana kuwaambia wanadamu wamesamehewa dhambi zao. Kwanza, Adamu alificha mbegu ya dhambi ndani kabisa ya nafsi yake hivi kwamba hakuelewa kabisa alichohitaji kuungama. Pili, hadi wanadamu walipoona kwamba dhambi zao zimeadhibiwa, ama wao wenyewe au mbadala, hawangeamini katika msamaha wa Mungu kama vile Kaini alivyokataa kuukubali.

> *Kaini akamwambia Bwana Mungu, kosa langu ni kubwa mno hata siwezi kusamehewa. Mwanzo 4:13 (Tafsiri ya Kiingereza ya Brenton LXX)*

Ili kumwokoa mwanadamu, ilimbidi Mungu atukomboe kutoka kwenye ufalme wa Shetani ambao ndani yake hakukuwa na msamaha bila adhabu na kifo. Kwa hiyo, Kristo alipaswa kufanywa dhambi kwa ajili yetu, ili tuweze kuamini katika msamaha wa Mungu. Kristo lazima ainuliwe ili kukidhi haki ya nyoka, ili tuweze kumtazama Kristo Msalabani na kuamini kwamba tunaweza kuponywa.

SURA YA 7

# NYOKA ALIYEINULIWA

Katika sura ya kwanza tuliibua maswali kadhaa kuhusiana na maneno ya Yesu akijilinganisha na kuinuliwa kwa nyoka juu ya mti. Bila kushughulikia suala la mfumo wa haki wa uwongo wa Shetani, ingekuwa vigumu sana kujibu vya kutosha katika sura hiyo. Sasa tumeshughulikia mfumo wa haki wa Shetani, tuko tayari kuchunguza kisa hiki.

Kisa cha nyoka aliyeinuliwa nyikani kina ufunguo muhimu wa kuelewa somo la upatanisho.

> *Wakasafiri kutoka mlima wa Hori kwa njia ya Bahari ya Shamu; ili kuizunguka nchi ya Edomu, watu wakafa moyo kwa sababu ya ile njia. Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu. Hesabu 21:4-5*

Wana wa Israeli walilalamika juu ya hali yao na hawakumlaumu Musa peke yake bali Mungu mwenyewe kwa kupuuza mahitaji yao

na kuwaacha wafie jangwani. Watu walimruhusu Shetani kupofusha macho yao kwa ulinzi wa upendo wa Mungu na maombi ya daima na uongozi mzuri wa Musa. Roho hii ya manung'uniko ilimruhusu Shetani kuvunja ukuta wa ulinzi wa Mungu.

*Achimbaye shimo atatumbukia ndani yake, na atakayebomoa ukuta ataumwa na nyoka. Mhubiri 10:8*

Israeli walikuwa wamejichimbia kwenye shimo la wasiwasi usio na sababu na lawama zisizo na msingi. Kumlaumu Mungu kwamba hawajali lilikuwa shitaka la uwongo dhidi ya tabia yake na kwa hiyo ilikuwa ni ibada ya sanamu. Ni muhimu kuelewa kwamba wazo lolote la uongo kuhusu Mungu hufanyiza ibada ya sanamu. Dhana yoyote mbaya ya tabia ya Mungu ni sanamu ya mawazo yetu wenyewe.

Mungu alikuwa akiwalinda Israeli kutokana na hatari za jangwani. Alikuwa ameandaa nguzo ya wingu wakati wa mchana ili kuwakinga na joto la jua na nguzo ya moto wakati wa usiku ili kuwakinga na baridi. Aliwalisha mana kila siku na kwa wazi aliwalinda dhidi ya wanyama wa mwituni na viumbe wenye sumu katika jangwa. Mwishoni mwa jangwa lao, Musa aliwaambia:

*Kwa maana BWANA, Mungu wako, amekubariki katika kazi zote za mkono wako. Anajua kutembea kwako katika jangwa hili kuu. Miaka hii arobaini BWANA, Mungu wako, amekuwa pamoja nawe;* ***hamjapungukiwa na kitu****. Kumbukumbu la Torati 2:7*

Pia tunaambiwa:

*Malaika wa BWANA hufanya kituo, Akiwazunguka wamchao, na kuwaokoa. Zaburi 34:7*

Israeli walipoacha kumcha Mungu na kumshutumu kwa kutojali, Hangeweza kuwalinda na Shetani kama Alivyokuwa amefanya hapo awali.

*Basi Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma watu; na watu wengi wa Israeli walikufa. Hesabu 21:6*

Tafsiri zote nilizokagua zinasema kwamba Mungu alituma nyoka kati ya watu. Unaposhikilia wazo kwamba haki ya Mungu inadai adhabu inayopelekea kwenye kifo, basi inaleta maana kamili kuamini kwamba Mungu aliwaadhibu Waisraeli kwa kutokuwa na shukrani na mashtaka ya uwongo dhidi yake. Adhabu ya wengi ilikuwa kifo.
Waisraeli waliona kwamba Mungu ndiye aliyewatuma nyoka wawaadhibu, wakakiri kwa Musa kwamba walikuwa wametenda dhambi na wakamsihi Musa amwombe Mungu awaondoe nyoka hao.

> *Watu wakamwendea Musa, wakasema, Tumefanya dhambi kwa sababu tumemnung'unikia Mungu, na wewe; utuombee kwa BWANA, atuondolee nyoka hawa. Basi Musa akawaombea watu. Hesabu 21:7*

Mungu hamwambii Musa kuwaambia watu kwamba si Yeye aliyetuma nyoka kwa sababu watu hawangeelewa hili. Walijua walikuwa wamemtenda Mungu dhambi, na katika akili zao wenyewe ilikuwa na maana kamili kwamba Mungu angewaadhibu na hata kuwaua baadhi yao kwa hasira kwa sababu ya dhambi zao. Hii ndiyo haki waliyoielewa; hivi ndivyo upatanisho ulivyomaanisha kwao.

Unapotazama maana ya neno la Kiebrania la kutuma katika wakati uliotolewa, tunaona yafuatayo:

> Piel Tense
>
> 1c1) kuachilia au kuondoka au kutoka au nje, kukataa, kutoa, kutupwa nje
>
> 1c2) kuachilia, kuweka huru
>
> 1c3) kupiga (matawi)
>
> 1c4) kushuka
>
> 1c5) kupiga

Je, Mungu aliwatuma moja kwa moja ili kuwadhuru Waisraeli? Au je, Mungu aliwaacha huru nyoka kwa kutowazuia tena wasiingie katika

kambi ya Israeli? Hatupaswi kukisia maana ya kutumika hapa kwa sababu Paulo anatuambia kilichotokea:

> *…wala tusimjaribu Kristo, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaangamizwa na **nyoka**;[G3789] wala kulalamika, kama baadhi yao walivyonung'unika, wakaangamizwa na **Mwangamizaji**. [G3644] 1Wakorintho 10:9-10*

Neno la Kigiriki ambalo Paulo anatumia kumaanisha nyoka linatumiwa katika sehemu nyingine nyingi kurejelea Shetani.

> *Basi yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka [G3789] wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani,… Ufunuo 12:9*

> *Akamshika yule joka, yule nyoka wa kale [G3789] ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga kwa muda wa miaka elfu moja. Ufunuo 20:2*

Juu ya hili, ufafanuzi wa Nguvu wa neno mwangamizaji (mharabu) katika mstari unaofuata unamaanisha "nyoka mharibifu, mwenye sumu kali." Tunazingatia pia maneno ya Yesu kuhusu tabia Yake.

> *Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa…. Luka 9:56*

Haya yote yanaelekeza kwa nguvu kwenye wazo kwamba Mungu aliwaacha nyoka waende huru kutoka kwenye kizuizi na kisha Shetani akawatumia kuwadhuru na kuwaua Waisraeli. Israeli walifikiri kuwa ni Mungu aliyekuwa akiwaua kupitia nyoka wakati kwa hakika ni Shetani aliyechukua udhibiti wa nyoka kwa sababu Israeli walikuwa wametoboa ukuta wa ulinzi wa Mungu kupitia kutokuwa na shukrani, mashtaka ya uongo, na ibada ya sanamu kuhusu tabia ya Mungu.

Ili kukidhi mawazo ya watu, Mungu alimpa Musa maagizo ya ajabu sana.

> *Kisha BWANA akamwambia Musa, "Tengeneza nyoka ya moto [H8314], ukaiweke juu ya mti; na itakuwa ya kwamba kila mtu aliyeumwa, aitazamapo, ataishi." Basi Musa akafanya nyoka ya*

*shaba, akaiweka juu ya mti; na ndivyo ilivyokuwa, ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipomtazama yule nyoka wa shaba, aliishi. Hesabu 21:8-9*

Mungu alimwambia Musa atengeneze sanamu ya shaba ya nyoka waliokuwa wakiwauma, na kuiweka juu ya mti, kisha awaalike watu wamtazame yule nyoka wa shaba na wangeishi.

Tendo hili lilikuwa la kawaida miongoni mwa mataifa ya kipagani kama inavyoonekana katika kisa cha Wafilisti walipolichukua sanduku la Israeli na kwa sababu hiyo wakapata mapigo ya panya na kupigwa na bawasiri.

*Kwa nini Mungu anatumia utaratibu wa kipagani kuwaponya Waisraeli? Kwa sababu bado walikuwa wametawaliwa na mawazo ya kipagani ya haki na urejeshwaji.*

*Basi, hilo sanduku la BWANA lilikuwamo katika nchi ya Wafilisti muda wa miezi saba. Nao Wafilisti wakawaita makuhani na waaguzi, wakasema, Tulifanyieje sanduku la BWANA? Tuonyesheni jinsi tuwezavyo kulirudisha mahali pake. Nao wakajibu, Mkilirudisha hilo sanduku la Mungu wa Israeli, msilirudishe kitupu; lakini msikose kumpelekea na matoleo ya kosa; hivyo mtapona, tena mtafunuliwa ni kwa sababu gani mkono wake haukuondolewa kwenu. Ndipo wakauliza, Na hayo matoleo ya kosa yatakuwa ya namna gani, hayo tutakayompelekea? Nao wakajibu, Na yawe majipu ya dhahabu matano, na panya wa dhahabu watano, sawasawa na idadi ya mashehe wa Wafilisti; kwa kuwa tauni moja ilikuwa juu yenu nyote, na juu ya mashehe wenu. Kwa hiyo mtafanyiza sanamu za majipu yenu, na sanamu za panya wenu waiharibuo nchi; nanyi mtamtukuza huyo Mungu wa Israeli; huenda ataupunguza uzito wa mkono wake juu yenu, na juu ya miungu yenu, na juu ya nchi yenu. 1 Samweli 6:1-5*

Kwa nini Mungu anatumia utaratibu wa kipagani kuwaponya Waisraeli? Kwa sababu bado walikuwa wametawaliwa na mawazo ya kipagani ya haki na urejeshwaji.

Kinachovutia kuhusu neno linalotumiwa kwa nyoka wa moto ni kwamba linapatikana mahali pengine kurejelea malaika.

> *Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu. Juu yake walisimama **maserafi**; [H8314] kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka. Isaya 6:1-2*

Je, ni bahati kwamba neno lile lile la nyoka wa moto pia linatumiwa kurejelea maserafi wanaosimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu? Ni malaika yupi aliyefanyika nyoka ambaye wakati fulani alisimama kwenye chumba cha enzi cha Mungu? Kwa wazi, hili hurejelea kwa Shetani. Kwa nini Musa anaombwa kufanya ishara ya Shetani na kufuata desturi za kipagani za mataifa mengine ili kutoa njia ya ukombozi kwa Waisraeli walioumwa? Kwa sababu mawazo yao ya upatanisho yalidai aina hii ya ibada ili watu waamini kwamba Mungu angewasamehe na kuwakubali.

Muunganiko wa Shetani na Upagani unaohusiana na kuinuliwa kwa nyoka ina nyanja nyingine ya uthibitisho. Hii inahusiana na chuma ambacho kilitumika kumfanya nyoka - shaba.

Shaba haikuwa chuma kilichoumbwa na Mungu. Haikuwa kitu ambacho unaweza kuchimba kutoka kwenye ardhi. Shaba ilitengenezwa na mmoja wa wazao wa Kaini.
Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; akajenga mji akauita Henoko, kwa jina la mwanawe.

> *Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; akajenga mji akauita Henoko, kwa jina la mwanawe. Henoko akamzaa Iradi, Iradi akamzaa Mehuyaeli; Mehuyaeli akamzaa Methushaeli; Methushaeli akamzaa Lameki. Lameki akajitwalia wake wawili, jina*

*la wa kwanza ni Ada, na jina la wa pili ni Sila. Ada akamzaa Yabali; huyo ndiye baba yao wakaao katika hema na kufuga wanyama. Na jina la nduguye aliitwa Yubali; huyo ndiye baba yao wapigao kinubi na filimbi. Sila naye akamzaa Tubal-kaini, mfua kila chombo cha kukatia, cha shaba na cha chuma; na umbu lake Tubal-kaini alikuwa Naama. Mwanzo 4:17-22*

Tubal-Kaini hakuwa wa ukoo wa wana wa Mungu (ikimaanisha wale waliomwabudu Mungu wa kweli) kupitia Sethi bali mzao wa Kaini. Baba yake alikuwa mtu wa kwanza jasiri vya kutosha kuoa wake wawili na kwa hivyo inaeleweka kwamba Tubal-Kaini angetiwa moyo kufanya jambo gumu sana - onyesho la ugumu wa mioyo ya ukoo wa watu ambao alitokea.

Shaba inachukuliwa kiishara kama kipengele kibaya katika Maandiko - kielelezo cha ugumu wa moyo.

*Nguvu zangu ni nguvu za mawe? au nyama yangu ni ya shaba? Ayubu 6:12 (KJV)*

*Kwa sababu nilijua wewe ni mkaidi, na shingo yako ni mshipa wa chuma, na paji la uso wako ni shaba."—Isaya 48:4 (KJV).*

*Wote ni waasi wabaya, waendao kwa masingizio; ni shaba na chuma; wote ni waharibifu.Yeremia 6:28 (KJV)*

*Mwanadamu, nyumba ya Israeli imekuwa takataka kwangu; wote ni shaba, na bati, na chuma, na risasi, katikati ya tanuru; nazo ni takataka za fedha. Ezekieli 22:18 (KJV)*

Chuma kilichotumiwa kinaonyesha kwamba mchakato huo umefanywa na mwanadamu badala ya kutengenezwa na Mungu.[25] Uhakika wa kwamba nyoka alitengenezwa kwa shaba unaonyesha uvuvio wa kishetani wa mchakato mzima.

Watu wanapotazama kwa imani kuelekea kwa nyoka wa shaba aliyeinuliwa, Mungu anawezeshwa kuwafikia kwa lengo lake kuu la

[25] Shaba ni mchanganyiko wa madini ya shaba na zinki

kuwapa uponyaji, msamaha, na wokovu. Baba yetu mpendwa anafika chini katika giza la udanganyifu wa kibinadamu na hutusadikisha juu ya upendo wake wa uponyaji na msamaha.

Watu wanaamini kwamba Mungu alituma nyoka kuwaadhibu na kwa hiyo nyoka kwenye mti anafunua ukweli wa nani waliyekuwa wanamwabudu hasa - Shetani. Kwa nini? Kwa sababu ni haki ya Shetani isiyo na huruma ambayo wanaamini iko katika moyo wa tabia ya Mungu wakati kwa kweli ni tabia ya Shetani na mwanadamu.

Umuhimu wa maneno ya Kristo kwa Nikodemo hauwezi kuzidishwa:

> *Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele Yohana 3:14-15 (KJV).*

Yesu anatumia neno hilo kuonyesha kwamba anachokifanya ni sawa na kile alichokifanya akiwa na Musa.

1. Anajihusisha na matendo ya kipagani ya kutengeneza sanamu ya kile kinachoogopwa ambacho kitawadhuru.
2. Ameinuliwa juu kwa mfano wa nyoka anayewakilisha haki ya nyoka.
3. Ameinuliwa juu katika muktadha wa shaba iliyotengenezwa na mwanadamu inayoakisi ugumu wa asili ya mwanadamu katika kuhitaji kitu kama hicho.
4. Anakidhi matakwa ya serafi/nyoka ambaye wakati fulani alisimama mbele za Mungu.

Yesu anaeleza waziwazi kwamba alipaswa kuinuliwa na kuuawa, si kwa sababu Mungu alidai hivyo, bali kwa sababu Shetani na mwanadamu walidai hivyo. Hakukuwa na njia nyingine kwa Mungu kufikia jamii ya wanadamu kwa upendo wake wa kusamehe isipokuwa kukidhi matarajio ya kibinadamu ya kile kilichohitajika ili kutuokoa.

Ni jambo la kushukuru, Maandiko yanatupa mifano kadhaa inayoonyesha Baba yetu anataka tuendelee kukua kutoka kwenye ishara ya kipagani ya shaba ya upatanisho hadi kwenye nafasi ya kuzungumza tu na Baba yetu na kutumaini msamaha na neema yake. Katika sura inayofuata tutachunguza ishara ya kuupiga mwamba na kuzungumza na mwamba kama ushahidi wa safari hii ya kuelewa upatanisho.

Katika sura za mbele tutachunguza samani za Patakatifu na maana ya safari kutoka kwenye madhabahu ya shaba kwenye Ua hadi kwenye sanduku la agano la dhahabu. Pia tutachunguza maana na mfuatano wa sikukuu kuanzia Pasaka hadi Siku ya Upatanisho kama ushahidi zaidi wa Mungu akitaka tutambue kwamba njia zetu si njia Zake na kwamba Yeye anataka kweli kutufundisha njia zake.

Tena, hii itaonyeshwa katika lugha ya Danieli 7 (Kiaramu) na 8 (Kiebrania) na umuhimu wa tofauti hizo.

Katika mambo haya yote na zaidi Mungu anatuonyesha kwamba hataki tubaki katika mawazo ya Mbadala wa Adhabu na ufahamu wa kibinadamu kwamba haki ya Mungu au haki inadai kifo. Baba yetu anajua alihitaji kukutana nasi katika eneo hili la giza ili atuongoze katika nuru ya kutambua kwamba tunahitaji tu kujua tabia yake na kisha kwa neema yake tutubu tabia zetu na kumwomba atubadilishe.

Pia ni muhimu kuelewa kwamba ili kuwa na upatanisho wa kweli, inatupasa kuelewa michakato yetu wenyewe ya mawazo kuhusu haki na upatanisho kabla ya kuelekea kwenye uhalisi wa upatanisho wa Baba yetu wa mbinguni. Kwa hivyo, Mbadala wa Adhabu ni sehemu muhimu ya mchakato wa upatanisho. Huwezi kuendelea kwa kweli hadi Mahali Patakatifu Pa Patakatifu pa Upatanisho wa Mungu hadi uweze kufahamu mtazamo wetu wa uongo wa kibinadamu wa upatanisho katika Ua.

Baba yetu ni wa thamani kama nini kukutana nasi katika dhana zetu zenye giza za haki! Ni ajabu jinsi gani kwamba Yesu alikuwa tayari kuinuliwa juu ya Msalaba ambao ulitosheleza haki ya kibinadamu ya

kishetani, ili tu kutupa sisi nafasi ya kuamini kwamba Mungu angetusamehe.

Sifa kwa Baba kwamba hatuachi katika mtazamo huu wa kipagani wenye giza wa upatanisho bali anatuita katika nuru ya ukweli ambapo tunatambua kwamba Mungu hataki dhabihu au toleo la aina yoyote, anataka tu tujue tabia yake ili kwamba tupate kutubu na kuunganishwa Naye.

SURA YA 8

# KUPIGA MWAMBA

Ili mwanadamu kusadikishwa kwamba Mungu amemrejesha kwa upendeleo, alipaswa kutosheleza haki ya Shetani hivyo kuthibitisha vipengele vya kweli vya nadharia ya fidia ya upatanisho. Shetani aliteka nyara wanadamu na kutusadikisha kwamba Mungu alikuwa na hasira juu yetu na kwamba haki yake ilidai kifo. Ili kumwachilia mwanadamu, Mungu aliruhusu Mwanawe kuteswa na kuuawa na jamii ya wanadamu na kuturuhusu tuamini kwamba haki yake ilitimizwa katika kifo cha Mwana wake. Je, ni vipi tena anaweza kuleta wokovu kwa akili ya mwanadamu mwendawazimu? Ilibidi tusadikishwe kwamba haki yetu ilitendeka.

> *Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; Warumi 8:3*

Sheria ya Mungu ikawa dhaifu kupitia mawazo yetu ya kimwili. Sheria ile iliyowekwa kuleta uzima tuliiona kuwa inaleta kifo. (Warumi 7:10). Kwa nini? Mfumo wa haki wa Shetani ulitudanganya na kuchukua fursa mbaya kupitia sheria na kutuua. (Warumi 7:11).

Mungu alimfanya Mwanawe kuwa dhambi kwa ajili yetu - kumaanisha kwamba alimruhusu auawe chini ya mfumo wetu wa haki wa asili, ulioongozwa na Shetani, ili tuweze kuamini kwamba Mungu ametusamehe. Hili ni sawa na agizo la Musa kuupiga mwamba.

> *Musa akamlilia BWANA, akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe. BWANA akamwambia Musa, Pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israeli pamoja nawe; na ile fimbo yako ambayo uliupiga mto kwayo, uitwae mkononi mwako, ukaende. Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu;* ***nawe utalipiga jabali****, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. Kutoka 17:4-6*

Watu walitaka kumuua Musa kama adhabu kwa kutotimiziwa mahitaji yao mara moja. Mungu alitoa mbadala - mwamba. Mwamba unawakilisha nani?

> *... na wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho. Kwa maana waliunywea mwamba ule wa kiroho uliowafuata,* ***na mwamba ule ulikuwa Kristo****. 1Wakorintho 10:4*

Kupigwa kwa mwamba kuliwakilisha kuridhika kwa watu waliokuwa wakidai adhabu kwa ajili ya Musa. Mwamba, unaowakilisha Kristo, ulikuwa ni mbadala. Ulipopigwa, ukiwakilisha kusulubishwa kwa Kristo (Mathayo 26:31), maji, yakiwakilisha upendeleo wa Mungu uliowashukia.

Miaka 40 baadaye, baada ya kuteseka na matokeo ya kutanga-tanga nyikani kwa sababu ya kutoamini kwao, watu walikuwa na kiu ya maji tena.

> *Na hapo hapakuwa na maji kwa ule mkutano; wakajikusanya juu ya Musa na juu ya Haruni. Watu wakashindana na Musa, wakanena, wakisema, Ingalikuwa heri kama tungalikufa wakati ule ndugu zetu walipokufa mbele za BWANA! Mbona mmewaleta kusanyiko la BWANA hata jangwa hili ili tufe huku, sisi na wanyama wetu? Na*

*mbona mmetupandisha kutoka Misri ili kutuleta hata mahali hapa pabaya? Si mahali pa mbegu, wala tini, wala mizabibu, wala makomamanga; wala hapana maji ya kunywa. Hesabu 20:2-5*

Kwa mara nyingine tena, walimlaumu Musa kwa kushindwa kuwapa mahitaji yao. Mungu alikuwa amewapelekea mana kwa miaka 40. Alikuwa amewapa maji kwa miaka yote 40. Je, ingewezekana kwamba Israeli wangejifunza kumwamini Mungu na sasa wangeweza tu kuomba maji kwa imani?

*Musa na Haruni wakatoka pale palipokuwa mkutano, wakaenda hata mlangoni pa hema ya kukutania, wakaanguka kifudifudi; utukufu wa BWANA ukawatokea. BWANA akasema na Musa, akinena, "Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako,* ***ukauambie mwamba*** *mbele ya macho yao utoe maji yake, nawe utawatokezea maji katika mwamba, na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao." Hesabu 20:6-8*

Wakati huu Musa alipaswa 'kusema na mwamba' ili maji yatoke, ishara ya uhai na wokovu. Hakukuwa na haja ya kupiga chochote. Hakukuwa na haja ya Mbadala wa Adhabu wakati huu. Ilibidi azungumze tu na mwamba.

Ishara hii inatufundisha kwa njia rahisi, mchakato wa hatua mbili za upatanisho. Tunapouacha utumwa wa dhambi kwa mara ya kwanza kama ilivyoonyeshwa katika msafara kutoka Misri, mwamba lazima upigwe. Matumizi ya nguvu yalipaswa kutumika kwenye mwamba ili kuruhusu maji kutoka humo.

Kama watu wa Mungu walio karibu na nchi ya ahadi, baada ya kuingia katika ulimwengu wa kuamini kwamba Mungu ametupa maji ya uzima kupitia mwamba uliopigwa, sasa tunaalikwa kuzungumza na mwamba bila hitaji la dhabihu. Hii ni hatua ya pili. Kukaa jangwani kunawakilisha ukuaji wa tabia ya maisha ya Kikristo:

*Nawe utaikumbuka njia ile yote BWANA, Mungu wako aliyokuongoza miaka hii arobaini katika jangwa, ili akutweze, kukujaribu kuyajua yaliyo moyoni mwako, kwamba utashika amri*

*zake, au sivyo. Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyoijua wewe wala baba zako hawakuijua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha BWANA. Kumbukumbu la Torati 8:2-3*

Cha kusikitisha, Musa hakuweza kufunua uzuri wa kuzungumza tu na mwamba wakati huo. Ukatili wa watu katika kumlaumu kwa kila jambo ulimjaribu kutenda kulingana na mfumo wa haki tulioupokea kutoka kwa Adamu uliovuviwa na Shetani. Musa alipiga mwamba kwa hasira mara mbili akionyesha hitaji la adhabu na matumizi ya nguvu. Hatuthubutu kumlaumu Musa kwa kushindwa kwake. Je, tunafikiri tungefanya vizuri zaidi huku watu hao wakinung'unika kila wakati?

*Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia, Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu? Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili; maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia. Hesabu 20:10-11*

Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba katika kuupiga mwamba kama ishara ya kifo cha Kristo, Musa alijihukumu kuwa mmoja ambaye sasa lazima afe. Kulingana na mawazo yake dhambi lazima iadhibiwe, na hivyo Mungu alishughulika na Musa kama alivyotenda.

*Kisha BWANA akanena na Musa na Haruni, akawaambia, Kwa sababu hamkuniamini mimi, ili kunitakasa mbele ya macho ya wana wa Israeli, kwa hiyo hamtawaingiza kusanyiko hili katika nchi niliyowapa. Hesabu 20:12*

Katika kuupiga mwamba mara mbili, Musa hakutakasa tabia ya Mungu machoni pa watu. Hasira yake katika kuupiga mwamba wa mbadala unaofanana na Kristo, ilifunua kwamba angejihukumu kulingana na ufahamu wake mwenyewe wa haki. Hili pia linaonekana katika maneno ya Musa, "Je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?....," wakijihusisha na kitendo hiki wenyewe badala ya Mungu.

Wengi wanashangaa kwa nini Mungu hakumruhusu Musa afike katika nchi ya ahadi pamoja na Israeli. Lakini Musa alijihukumu mwenyewe chini ya mfumo wa haki wa uongo. Baada ya kuupiga mwamba, alijua kwamba hakuwa ameitii sauti ya Mungu. Alijua kwamba alikuwa amefanya kosa. Sasa baada ya kuupiga mwamba, alijihukumu mwenyewe kulingana na jinsi alivyokuwa amewahukumu watu, alidhihirisha kwa kuupiga mwamba mara mbili. Alitaka kuifikia nchi ya ahadi, lakini moyoni alijihukumu kwa kutofanya kile ambacho Bwana alikuwa amemtaka afanye.

Ni lazima watu watambue uzito wa kosa la Musa. Kutaniko zima lilikuwa likitenda kazi katika mfumo huu wa haki wa uongo. Kama Kaini, walikuwa wakilia kwamba adhabu hii ni kubwa kuliko Musa awezavyo kustahimili, lakini wote kwa ndani walihisi kwamba uovu huu haungeweza kusamehewa. Kwa hiyo Bwana alilazimika kuruhusu hukumu ambayo Musa na Haruni walikuwa wameitoa iwarudie.

Hadithi ya Israeli kupokea maji kutoka kwenye mwamba mwanzoni na mwisho wa safari yao inatupa mchakato wa hatua mbili za upatanisho. Kupigwa kwa mwamba (Kristo) ilibidi kutokea ili watu wakubali kwamba maji (uzima) yangetolewa kwao. Mwishoni mwa safari, walijaribiwa tena ili kuona kama wangeweza kuingia katika njia ya Mungu ya upatanisho na hiyo ni kwa kusema tu na mwamba (Kristo). Sadaka na kafara hazihitajiki katika hatua ya pili au ya Agano Jipya ya upatanisho.

Hili linaongeza uzito kwenye maneno ya Yesu kwamba alimaliza kazi ya Baba Yake usiku kabla ya Yeye kufa. Hakuna kifo kilichohitajika katika kazi ya Mungu ili kukamilisha upatanisho. Kilichohitajika tu ni ufahamu wa tabia yake na kuomba tu msamaha, tukiamini kwamba Yeye ndiye mpaji kwa wale wanaomtafuta kwa bidii. (Waebrania 11:6).

SURA YA 9

# UPATANISHO WA MWANADAMU

Sura mbili zilizopita zimeweka kwa ajili yetu mchakato wa hatua mbili za upatanisho. Mfumo wa haki wa uongo wa Shetani uliorithiwa na wanadamu lazima utimizwe kabla ya watu kuamini katika msamaha wa Mungu. Sadaka ya Kristo Msalabani ni kwa ajili ya kuiridhisha haki ya binadamu ambayo inafungua mlango kwa ajili yetu kuamini ukweli wa tabia ya Mungu.

Mara tu tunapoelewa kanuni hii, tunaweza kuanza kuvifungua visa kadhaa katika Agano la Kale vinavoonyesha Mungu kama Mmoja anayedai kifo. Lakini uhalisia wake ni tofauti kabisa.

Fikiria kisa cha Israeli kwenye mipaka ya Kanaani:

> *Basi Israeli akakaa Shitimu, kisha watu wakaanza kuzini pamoja na wanawake wa Moabu; kwa kuwa waliwaalika hao watu waende sadakani, sadaka walizowachinjia miungu yao; watu wakala chakula, wakaisujudu hiyo miungu yao. Ikawa Israeli kujiungamanisha na Baal-peori; hasira za BWANA zikawaka juu ya Israeli. Kisha BWANA akamwambia Musa, Watwae wakuu wote wa hao watu,*

*ukamtungikie BWANA watu hao mbele ya jua, ili kwamba hizo hasira kali za BWANA ziwaondokee Israeli. Basi Musa akawaambia waamuzi wa Israeli, Waueni kila mtu watu wake waliojiungamanisha na Baal-peori. Hesabu 25:1-5*

Israeli walidanganywa na Balaamu. Ingawa aliheshimiwa na Israeli kama nabii, Balaamu alikuwa amepotea njia, akifuata pupa zake badala ya Mungu. Alichukua malipo kutoka kwa mfalme wa Midiani ili kuwalaani Israeli. Lakini majaribio yake yalikatishwa tamaa kwa sababu ya Israeli kuwa chini ya ulinzi wa Mungu, na badala yake akawabariki. Kisha kwa ujanja akapendekeza wawaalike Waisraeli kwenye karamu ambapo wangekunywa divai, kuacha ulinzi wao, na kuanguka katika ibada ya miungu ya kipagani - hii ingeondoa baraka za Mungu na kuleta laana. Mtume Paulo anarejelea tukio hili na matendo mabaya waliyojihusisha nayo kama sehemu ya ibada hiyo:

*Wala tusifanye uzinzi kama baadhi yao walivyozini, wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu. 1Wakorintho 10:8*

Waisraeli walikuwa wameziacha amri za Mungu. Walisujudu na kuabudu miungu mingine, na kushiriki katika uasherati wao. Israeli hawakujua mambo waliyokuwa wakiyafanya. Walikumbuka kile kilichotokea kwenye tukio la ndama wa dhahabu na hukumu zilizowapata wakati huo.

Mungu alikuwa amewaonya Israeli kukaa karibu naye na kutembea katika amri na sheria zake ili wawe salama.

*Lakini msiponisikiza, wala hamtaki kuyafanya maagizo hayo yote; nanyi mkizikataa amri zangu, na roho yenu ikichukia hukumu zangu, hata ikawa hamtaki kuyafanya maagizo yangu yote, bali mwalivunja agano langu; mimi nami nitawatenda jambo hili; nitaamrisha uje juu yenu utisho, hata kifua kikuu na homa, zitakazoharibu macho yenu, na kuidhoofisha roho; nanyi mtapanda mbegu yenu bure, kwa kuwa adui zenu wataila. Mambo ya Walawi 26:14-16*

Israel ilipatwa na ugonjwa hatari ambao ulisambaa katika kambi hiyo. Tunajifunza hili mbele kidogo kutoka kwenye kisa hiki katika Hesabu 25.

> *Na waliokufa kwa tauni hiyo walikuwa watu ishirini na nne elfu. Hesabu 25:9*

Paulo anataja kwamba watu 23,000 walikufa kwa siku moja, lakini jumla ya watu 24,000 walikufa wote pamoja. Israeli walipomwacha Mungu wao, Mungu alilazimika kuwaruhusu kuvumilia matokeo ya uchaguzi wao.

> *BWANA hujulikana kwa hukumu anayoifanya; mtu mbaya amenaswa katika kazi ya mikono yake mwenyewe. Zaburi 9:16*

Kwa njia sawa na ile ya kwamba Mungu hakuwazuia tena nyoka kuingia kambini, pia Hakumzuia Shetani kushambulia miili yao kwa magonjwa. Walijifanyia hivyo wenyewe kwa sababu waliabudu miungu mingine.

Ikiwa mwanamke atamuacha mume wake anayempenda na kuingia kwenye uhusiano na mwanaume ambaye anaanza kumpiga na hatimaye kumuua, je, tunamlaumu mume wake mpendwa kwa kifo chake kwa sababu hakumzuia mwanamke huyo kuingia kwenye uhusiano mwingine? Je, ingefaa kiasi gani kumlazimisha kurudi?
Je, hilo lingemdhihirisha mume kuwa mpenda uhuru?

*Katika huzuni kubwa, Baba yetu wa mbinguni alilazimika kuruhusu uchaguzi wa Waisraeli wa kuabudu miungu mingine—miungu iliyobuniwa na Shetani.*

Katika huzuni kubwa, Baba yetu wa mbinguni alilazimika kuruhusu uchaguzi wa Waisraeli wa kuabudu miungu mingine—miungu iliyobuniwa na Shetani. Katika kuabudu miungu hii, Israeli walijiweka chini ya udhibiti wake (Shetani) ambao ulimruhusu kuanza kuwaangamiza.

Tauni ilipoanza kupita kambini na watu kuanza kufa, hatia na matokeo ya matendo yao yaliwafanya watambue dhambi yao. Kwa mitazamo ya kibinadamu, njia pekee ambayo Israeli wangeweza kupata kibali kwa Mungu tena ilikuwa ni kutolewa kwa adhabu, ambayo ilipelekea kwenye vifo vya wachache wao, ili wengine wapate kupatanishwa na Mungu.

Ili kukidhi haki ya watu, Mungu alimwambia Musa yafuatayo:

> *"Kisha BWANA akamwambia Musa, Watwae wakuu wote wa hao watu, ukamtungikie BWANA watu hao mbele ya jua, ili kwamba hizo hasira kali za BWANA ziwaondokee Israeli." Hesabu 25:4*

Mungu alikuwa akifunua tu dhambi ya mwanadamu katika usemi huu. Mwitikio wa asili wa mwanadamu kwa matokeo mabaya ya maamuzi mabaya ni kutafuta mtu mwingine wa kulaumiwa. Hii ndiyo njia pekee ambayo watu wangekubali rehema; dhabihu au Mbadala wa Adhabu ilihitajika. Taifa zima lilikuwa limeshiriki katika sikukuu hiyo lakini wale waliokuwa katika nyazifa za juu zaidi katika kuwatia moyo wafanye maovu sasa walikuwa wametundikwa mbele ya macho ya watu.

Watu walipowatazama wale watu walioning'inia mbele ya jua, kama ule mchakato wa kumtazama yule nyoka wa shaba, watu wangeweza kuanza kuamini kwamba Mungu angewasamehe ili waweze kuponywa na tauni.

Wakati tauni ilipokuwa ikiendelea na viongozi wa uasi wakiuawa, mmoja wa wakuu wa Israeli alimleta mwanamke Mmidiani katikati ya kambi akikusudia kulala naye hadharani.

> *Na tazama, mmoja wa wana wa Israeli akaja na kuwaletea ndugu zake mwanamke Mmidiani mbele ya macho ya Musa, na machoni pa mkutano wote wa wana wa Israeli, waliokuwa wakilia mlangoni pa hema ya kukutania. Hesabu 25:6*

Waisraeli wengine walipokuwa wakilia na kutubu kwa ajili ya dhambi zao, kiongozi huyo wa kabila la Simeoni alithubutu bila haya kumleta mwanamke huyo mgeni kambini ili kufanya uasherati naye. Ijapokuwa wengi katika kambi hiyo walikuwa wamefanya dhambi, matendo ya mtu huyu yalitoa fursa kwa ajili ya haki ya binadamu kujidhihirisha yenyewe. Zimri Msimeoni akawa mchukua dhambi si kwa ajili yake tu bali kwa taifa zima.

*Basi Finehasi, mwana wa Eleazari, mwana wa Haruni kuhani, alipoona hayo, akainuka kutoka katikati ya mkutano, akashika mkuki mkononi mwake; naye akamfuata yule mtu wa Israeli ndani ya hema, akawachoma wote wawili, yule mwanamume wa Israeli, na yule mwanamke tumboni mwake. Basi tauni ikakomeshwa kati ya wana wa Israeli. Na waliokufa kwa tauni hiyo walikuwa watu ishirini na nne elfu. Hesabu 25:7–9*

Finehasi alipoona matendo ya ukatili ya Zimri, hisia yake ya haki iliamshwa. Wakati Israeli walipokuwa wakitubu dhambi zao, mtu huyu alipuuzia dhambi yake mbele yao. Finehasi, akifuata kanuni za haki na hukumu ya kibinadamu, alichukua Mkuki na kuwaua Zimri na Kosbi katika tendo la ngono. Hili lilionekana kuwa sahihi kwa taifa, na waliamini lingekidhi haki ya Mungu (ingawa kwa hakika ilikuwa ni haki ya kibinadamu ambayo ilielekezwa kwa Mungu ambayo ilitulizwa).

Ilikuwa ni mara baada ya kitendo hiki kwamba tauni ilikomeshwa. Kisha Mungu akaweka baraka kwa Finehasi kwa njia ifuatayo:

*Finehasi, mwana wa Eleazari, mwana wa Haruni kuhani, amezigeuza hasira zangu zisiwe juu ya wana Wa Israeli, kwa kuwa alikuwa na wivu kati yao kwa wivu wangu mimi, hata nisiwaangamize wana wa Israeli katika wivu wangu. Basi kwa hiyo, sema, Tazama, nampa yeye agano langu la amani; tena kwake yeye, na kizazi chake baada yake, litakuwa agano la ukuhani wa milele; kwa sababu alikuwa na wivu kwa ajili ya Mungu wake, na kuwafanyia upatanisho wana wa Israeli. Hesabu 25:11-13*

Katika hatua ya kuwaua Zimri na Kosbi, Finehasi alileta upatanisho kwa Israeli. Hili linafuata muundo sawa na kupigwa kwa mwamba. Israeli hawakuamini kwamba Mungu angewasamehe mpaka Zimri afe, kwa sababu haki ya kibinadamu inadai kifo kabla ya msamaha kutokea. Bila kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi. (Waebrania 9:22 ).

Mungu alimbariki Finehasi kwa sababu alitenda kwa nia njema. Mungu hakumhukumu kwa kumuua Zimri kwa sababu Mungu alijua kwamba hatua ya kwanza kwa wanadamu kukubali upatanisho ilikuwa kifo cha mwenye hatia kubwa zaidi kati ya taifa hilo.

Kama Finehasi hangefanya alichofanya, Israeli wangebaki chini ya hukumu ya Mungu kama walivyoelewa. Hawangeweza kuamini kwamba Mungu angewasamehe. Kwa hiyo, tauni ingeendelea mpaka wengi katika kambi wangeangamia.

Ikiwa Israeli wangejua ukweli wa tabia ya Mungu na kwamba Hakutamani dhabihu, wangeweza kuja na kuomba msamaha na wangekubaliwa. Wangeweza kusema na mwamba na kupokea maji ya uzima bure. Lakini njia za mwanadamu si njia za Mungu, kwa hiyo Zimri alipaswa kufa ili taifa zima lisiangamie.

Sababu ambayo ilimfanya Mungu kumwambia Musa kuwatundika wahalifu hao mbele ya watu ni kwa sababu huu ni mchakato wa upatanisho wa kibinadamu.

> *Kulikuwa na njaa siku za Daudi muda wa miaka mitatu, mwaka kwa mwaka; naye Daudi akautafuta uso wa BWANA. BWANA akasema, Ni kwa ajili ya Sauli, na kwa nyumba yake yenye damu, kwa kuwa aliwaua hao Wagibeoni. Ndipo mfalme akawaita Wagibeoni akawaambia; (basi Wagibeoni si wa wana wa Israeli, ila ni wa masalio ya Waamori; na wana wa Israeli walikuwa wamewaapia; lakini Sauli akatafuta kuwaua katika juhudi yake kwa ajili ya wana wa Israeli na Yuda;) basi Daudi akawaambia hao Wagibeoni, Niwatendee nini?* ***Na kwa tendo gani nifanye upatanisho****, mpate kuubariki urithi wa BWANA? Na hao Wagibeoni wakamwambia, Si jambo la fedha wala*

*dhahabu lililo kati ya sisi na Sauli, au nyumba yake; wala si juu yetu kumwua mtu ye yote katika Israeli. Akasema Mtakayoyanena, ndiyo nitakayowatendea ninyi. Wakamwambia mfalme, Yule mtu aliyetupoteza, na kutufanyia shauri la kutuharibu, tusikae katika mipaka yo yote ya Israeli, basi,* ***na tutolewe watu saba katika wanawe, nasi tutawatundika mbele za BWANA katika Gibeoni****, katika mlima wa BWANA. Mfalme akasema, Nitawatoa. 2 Samweli 21:1–6*

Tunaona katika matendo haya, kanuni za upatanisho wa mwanadamu. Laana ya njaa ilikuwa imeshuka juu ya Israeli. Ili kuiondoa laana, watu saba walipaswa kufa. Katika kesi hiyo, watu hawakuwa na hatia. Hawakuwa wametenda uhalifu wowote dhidi ya Wagibeoni. Hata hivyo walichaguliwa kama Mbadala wa Adhabu kwa ajili ya dhambi ya baba yao. Mara baada ya hatua hii kuchukuliwa, Israeli waliamini kwamba dhambi imesamehewa na kwa hiyo mvua inaweza kurudi na ukame utakwisha.

Kipengele hiki cha kifo cha wasio na hatia ni sehemu muhimu ya upatanisho wa mwanadamu. Kama tunavyoona katika kisa cha Msalaba wa Kristo, wasio na hatia lazima wauawe pamoja na wenye hatia.

*Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana, akisema, Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu akamkemea, akisema, Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo?* ***Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa****. Luka 23:39–41*

Tutaangalia mifano zaidi katika Agano la Kale ya wenye hatia na wasio na hatia kufa ili upatanisho wa kibinadamu utendeke. Kama tutakavyogundua katika sura ya 11, kifo cha watu wenye hatia waliotundikwa mbele ya jua kwenye mipaka ya Kanaani pamoja na Zimri mwenye hatia hakikutosha kuleta upatanisho kwa ajili ya Israeli. Ilibidi kuwe na kifo cha wasio na hatia kabla ya upatanisho kupatikana.

Sababu ambayo ilimfanya Mungu kumwambia Musa kuwatundika watu waliokuwa viongozi katika uasi wa Israeli inaelezwa katika kisa cha Daudi na Wagibeoni. Alijua kuwa hii ndiyo njia pekee ambayo msamaha ungeweza kupatikana katika akili za watu, kwa hiyo akawaambia yale yaliyokuwa mawazo yao. Ni hatua ya kwanza katika mchakato wa hatua mbili za upatanisho. Kifo cha watu hawa hakiakisi tabia ya Mungu bali tabia ya mwanadamu na kile anachofikiri juu ya Mungu. Tunaona kanuni hii tena na tena katika Agano la Kale:

> *Wakaondoka asubuhi na mapema, wakatoa dhabihu, wakaleta sadaka za amani, watu wakaketi kula na kunywa, wakaondoka wacheze. BWANA akamwambia Musa, Haya! Shuka; kwa maana watu wako uliowatoa katika nchi ya Misri wamejiharibu nafsi zao, wamepotoka upesi kuiacha ile njia niliyowaamuru, wamejifanyizia ndama ya kuyeyusha wakaiabudu na kuitolea dhabihu, wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika nchi ya Misri. Kutoka 32:6-8*

Waisraeli walipokuwa kwenye Mlima Sinai na Musa akiwa mlimani akipokea maagizo kutoka kwa Mungu, Israeli walichoka kusubiri na kuanguka katika mazoea yao ya zamani ya kuabudu tangu walipokuwa Misri. Musa aliporudi, watu walihisi hatia yao. Sadaka ilihitajika kabla ya watu kuamini katika msamaha wa Mungu.

> *...ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, Mtu awaye yote aliye upande wa BWANA, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia, Akawaambia, BWANA, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake. Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu. Kutoka 32:26–28*

Mara tu wahalifu wakuu walipouawa, Musa angeweza kutafuta upatanisho kwa ajili ya dhambi ya taifa.

*Musa akasema, Jiwekeni wakfu kwa BWANA leo, naam, kila mtu juu ya mwanawe na juu ya ndugu yake; ili awape baraka leo. Hata asubuhi yake Musa akawaambia watu, Mmetenda dhambi kuu; na sasa nitakwenda juu kwa BWANA,* ***labda nitafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yenu.*** *Kutoka 32:29–30*

Mwenye hatia zaidi katika ule uasi alikuwa ametolewa dhabihu. Lakini upatanisho haujakamilika. Haja ya damu isiyo na hatia ilibakia.

*Musa akarejea kwa BWANA akasema, Aa! Watu hawa wametenda dhambi kuu wamejifanyia miungu ya dhahabu. Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao – na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika. Kutoka 32:31–32*

Musa anapofikiria dhambi iliyotendwa na Waisraeli, anakuwa na wasiwasi ikiwa Mungu anaweza kuwasamehe. Sadaka ya mwenye hatia inaweza isitoshe. Labda ikiwa yule asiye na hatia atatolewa, basi Mungu angesamehe Israeli. Musa anajitoa kama sadaka isiyo na hatia ili kukamilisha hitaji la Mbadala wa Adhabu.

Kwa mtazamo wa kibinadamu hili ni tendo la ajabu la upendo kwa upande wa Musa. Linafunua upendo wa kujitoa kafara wa Mwokozi wake. Walakini, dhabihu hii liko ndani ya mipaka ya kupigwa kwa mwamba. Ni hatua ya kwanza katika mchakato wa upatanisho. Hatua hii ya kwanza ina vipengele viwili; kifo cha mwenye hatia zaidi pamoja na kifo cha asiye na hatia.

Mungu hakukubali kafara ya Musa kwa sababu kifo cha Musa hakingeleta upatanisho ambao Musa aliutamani kwa ajili ya watu. Kwa mtazamo wa kibinadamu, ukosefu wa yule asiye na hatia ulimaanisha kwamba Israeli ingeendelea kutilia shaka kukubalika kwao kwa Mungu na hivyo kuanguka katika dhambi. Hii ilimaanisha kwamba Israeli ingeendelea kupatwa na mapigo.
BWANA akamwambia Musa, Mtu ye yote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu.

*Basi sasa uende ukawaongoze watu hawa mpaka mahali pale ambapo nimekwambia habari zake; tazama, malaika wangu atakutangulia;*

*pamoja na hayo siku nitakayowajilia nitawapatiliza kwa ajili ya dhambi yao. BWANA akawapiga hao watu, kwa walivyoifanya ile ndama, ambayo Haruni aliifanya. Kutoka 32:33–35*

Ikiwa yule asiye na hatia angetolewa dhabihu kwa niaba ya Israeli, wangeweza kuamini kwamba Mungu alikuwa amewasamehe na tauni ingekomeshwa.

Kama tulivyogundua katika sura ya nne, tamaa ya kuua ni udhihirisho wa uadui wa kibinadamu dhidi ya Mwana wa Mungu na mwanamke ambaye aliongoza Adamu kula tunda. Tamaa ya kuwaua wenye hatia ni udhihirisho wa kisasi cha kishetani. Tamaa ya kuwaua wasio na hatia ni ufunuo wa tamaa ya Shetani, tangu mwanzo, kumwua Mwana wa Mungu. Kanuni hizi mbili, kuua wenye hatia na wasio na hatia zinaonyeshwa katika hadithi za Biblia na ni udhihirisho wa uzao wa asili wa Mwanzo 3:12 - "mwanamke uliyenipa."

Kisa cha ukengeufu wa Yordani na Midiani hatimaye kinahitimishwa katika Hesabu 31 na mauaji ya watoto wasio na hatia. Kabla ya kuchunguza kisa hiki, tunahitaji kuchunguza kanuni ya injili ya jinsi Mungu anavyoruhusu hali yetu ya dhambi kudhihirika ili tuweze kujiona jinsi tulivyo ili tuweze kutubu.

SURA YA 10

# DHAMBI ILIPOZIDI, NEEMA ILIKUWA NYINGI ZAIDI

Je, ni mchakato gani ambao Mungu huutumia kumwongoza mwenye dhambi kwenye wokovu? Je, Mungu humwonyeshaje mwanadamu uadui uliofichwa moyoni mwake?

> *Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Yeremia 17:9*

Ingekuwa rahisi sana kwa Mwana wa Mungu kutuambia, "Mnajaribu kuniua" na sisi kwa kumwamini, tupige magoti kwa machozi na kuomba msamaha na kuamini kwamba Mungu ni mwingi wa rehema hata tunasamehewa.

Tunaona kile kinachotokea wakati Yesu alipojaribu kuwaambia watu fulani kwamba walikuwa wanajaribu kumuua.

*Musa hakuwapa torati, lakini hakuna hata mmoja wenu anayeishika sheria? Kwa nini mnatafuta kuniua?" Watu wakajibu, wakasema, Una pepo; Ni nani anayetaka kukuua?" Yohana 7:19-20*

Je, unakabiliana vipi na kitu ambacho kimefichwa ndani ya moyo wa mtu ambacho hata hajui kabisa kipo? Bila kutumia nguvu, Mungu huturuhusu kukabiliana na matokeo ya uchaguzi wetu wenyewe ili kile kilicho ndani yetu kidhihirike ili tuweze kukiona.

Chukua kwa mfano kisa cha mwanamke mgeni ambaye alimwomba Yesu amponye binti yake. Wanafunzi wa Yesu walipofushwa kutokujua hali yao ya ubaguzi. Huenda Yesu angewaambia yale yaliyokuwa yamefichwa mioyoni mwao, lakini wangeudhika au kumkataa tu kwa sababu ya kuwataka kuja katika uhalisia ambao hawakuwa tayari kuukubali.

*Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo. Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu. Mathayo 15:22–23*

Ikiwa Yesu angekubali ombi la mwanamke huyo mara moja, wanafunzi hawangeanza kutambua jinsi hali yao ilivyokuwa mbaya. Kwa kukaa kimya, dhambi ya ubaguzi ya wanafunzi ilionekana katika ombi la kumfukuza. Lakini Yesu haishii hapo. Anaonekana kukubaliana na wanafunzi kwa jinsi anavyozungumza.

*Lakini akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Mathayo 15:24*

Yesu anaonekana kuthibitisha ubaguzi wao. Kwa wanafunzi, kauli hii ilionekana kana kwamba Yesu alikuwa akimtenga kwa sababu hakuwa Myahudi katika mwili. Lakini Yesu ni Mwokozi wa ulimwengu wote, hivyo nyumba ya Israeli inajumuisha wale wote wanaopokea Roho wa kweli wa Mungu.

*Maana yeye si Myahudi aliye Myahudi kwa nje, wala tohara si ile ionekanayo tu katika mwili; bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani; na tohara ni ya moyo, katika Roho, si katika andiko; ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu. Warumi 2:28–29*

Kwa wale wanaosikiliza katika mfumo wa mwili, wangesikia tu Yesu akimtenga mwanamke huyu na hivyo kuthibitisha upendeleo wao dhidi yake. Ukweli huu ni muhimu kuelewa amri zote za Mungu katika Agano la Kale ambazo zinaonekana kuhimiza mauaji.

Ndiyo maana Neno la Mungu lina makali kuliko upanga wowote ukatao kuwili. Neno la Mungu hufichua kwa mwanadamu mbegu inayokaa ndani yake. Ikiwa ubinafsi unatawala moyo, basi Neno la Mungu litaonekana kuthibitisha mawazo yao wenyewe, lakini kwa wale wanaomsikiliza Roho wa Kristo, watasikia kwa njia inayoakisi tabia ya Kristo.

*Ndiyo maana Neno la Mungu lina makali kuliko upanga wowote ukatao kuwili. Neno la Mungu hufichua kwa mwanadamu mbegu inayokaa ndani yake.*

Kwa wale wanaomsikiliza Roho wa Mungu, wangesikia maneno ya Yesu kwa mwanamke huyu kama mwaliko. Ni msikilizaji ndiye anayeamua maana ya maneno. Maneno ya Yesu yanazungumza kwenye mwili na Roho. Kwa wazi, mwanamke huyo alikuwa katika Roho kwa sababu hakuacha ombi lake, bali alikaribia na kumwabudu Yesu, akisisitiza ombi lake.

*Kisha akaja akamsujudia, akisema, "Bwana, nisaidie!" Mathayo 15:25*

Binti huyu wa thamani kwa Mungu aliona kitu ndani ya Yesu ambacho hakikumkatisha tamaa kuendelea na ombi lake. Lakini kulikuwa na kitu ndani yake ambacho bado kilihitaji kutoka. Kumilikiwa kwa bintiye na pepo wachafu kunazungumza baadhi ya giza ambalo mwanamke huyu alilipata. Alijiona hana thamani ndani yake. Kukubali kukumbatia hali ya kujiona huna thamani ni dhambi

kwa kuzingatia thamani tuliyo nayo machoni pa Mungu. Anasema sisi ni wapendwa wake, na kuamini kuwa hatuna thamani kunakanusha ukweli wa utambulisho wetu kwa Mungu. Yesu anafika ndani zaidi ya nafsi yake kwa kuakisi mawazo yake kuhusu yeye mwenyewe na yale ambayo wanafunzi walihisi juu yake.

> *Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa. Mathayo 15:26*

Sikio lililo katika mwili litasikia kwamba Yesu alimwita tu mbwa, na hivyo kuzidisha hisia zao za ubaguzi au kinyume chake kutofaa kwao wenyewe. Lakini katika Roho, sikio linaona kwamba Yesu hakumwita mbwa bali alikuwa akimuuliza kama aliamini kwamba alikuwa mtoto wa Mungu. Angeweza kujibu, "Mimi ni mtoto wa Mungu" na kusisitiza ombi lake katika muktadha huu. Badala yake, kisha anafichua kujihukumu kwake kama mtu asiyefaa kitu. Kwa wakati huu, Roho wa Mungu anamsadikisha zaidi juu ya neema nyingi sana.

> *Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao. Mathayo 15:27*

Ni Roho wa Kristo anayemvuta ili kushinda hisia zake za kuwa mbwa, na badala yake kuamini kuwa anaweza kuwekwa huru kutokana na mahangaiko yake makubwa juu ya bintiye pamoja na hisia zake kwamba anaadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake.

Furaha katika moyo wa Yesu inadhihirishwa katika maneno yake ambayo huzungumza juu ya upendo wa Yesu kwa binti Yake.

> *Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile. Mathayo 15:28*

Ni mshituko ulioje ambao wanafunzi waliupata! Kufuatia kila tamko la Yesu katika mwili, wangechanganyikiwa kabisa na kile kinachoonekana kuwa badiliko la ghafula kwa kumponya binti wa mwanamke huyo. Hili lingejaribu imani yao Kwake, lakini kwa shukrani waliishikilia. Ni mpaka usiku kabla ya kusulubishwa

ambapo uadui ndani ya mioyo ya wanafunzi ulifunuliwa. Hawakuwa na habari kwamba kulikuwa na uadui ndani yao. Yesu alijaribu kwa upole kuwaonya:

*Ndipo Yesu akawaambia, "Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu, kwa maana imeandikwa, 'Nitampiga mchungaji, na kondoo wa kundi watatawanyika.' Lakini baada ya kufufuka, nitawatangulia kwenda Galilaya."Petro akajibu, akamwambia, Ijapokuwa watu wote watachukizwa kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe. Mathayo 26:31-33 (KJV)*

Yesu anawaonya wanafunzi wake kwa upendo kuhusu yaliyo ndani yao. Badala ya kuomba msaada, Petro anakana yale ambayo Yesu anayasema na kudai kwa uthabiti hukumu yake mwenyewe. Ikiwa Petro angemsikiliza Yesu na kuomba msaada, basi huenda hangeshindwa au angalau anguko lisingekuwa kubwa sana.

*Lakini haya yote yamekuwa, ili maandiko ya manabii yatimizwe. Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia. Mathayo 26:56*

*Punde kidogo, wale waliohudhuria wakamwendea, wakamwambia Petro, Hakika wewe nawe u mmoja wao; kwa sababu hata usemi wako wakutambulisha. Ndipo akaanza kulaani na kuapa akisema, Simjui mtu huyu. Na mara akawika jogoo. Petro akalikumbuka lile neno la Yesu alilolisema, Kabla ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu. Akatoka nje, akalia kwa majonzi. Mathayo 26:73–75*

Maskini Petro, uadui moyoni mwake dhidi ya Mwana wa Mungu ulidhihirishwa kwa njia ya ajabu sana. Kisa chake kinathibitisha maneno ya Maandiko kuwa kweli.

*Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi; Warumi 5:20*

Huenda Yesu angezuia matukio ambayo yaliwafanya wanafunzi kumwacha. Huenda angejiweka huru kutoka kwa viongozi wa Kiyahudi na kuwaongoza kwenye usalama, lakini wasingeweza kamwe kujua kilichokuwa ndani yao; uadui ungebakia.

Upatanisho na Baba yetu wa mbinguni unahitaji kuondolewa kwa uadui uliofichika ndani ya mioyo yetu. Utaratibu huu unakamilishwa kupitia kwa Mungu kuruhusu hali kutokea ambayo inafichua kile kilicho ndani ya ufahamu wetu. Mambo haya yanapojitokeza, Roho wa Mungu anamimina neema yake juu ya mwenye dhambi na kuwaalika kupokea msamaha. Hivi ndivyo upatanisho unavyofanyika. Paulo anauelezea katika muktadha mwingine kama huu:

> *Na tumaini hilo tunalo mbele za Mungu kwa njia ya Kristo. Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu.*
>
> *Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha. Basi, ikiwa huduma ya mauti, iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika; je! Huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu? Kwa maana ikiwa huduma ya adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi. 2 Wakorintho 3:4–9*

Paulo anatuonyesha kazi ya maagano mawili. Kazi tukufu ya Agano la Kale ni huduma ya mauti. Inatufunulia uadui ndani ya mioyo yetu. Lakini kazi ya Agano Jipya ni bora zaidi. Inatukomboa kutoka kwenye uadui na dhambi zetu. Tunapokea uhakikisho wa msamaha. Kuhukumiwa kwa sheria katika Agano la Kale kunafanya kazi yake kutuleta kwa Kristo. Miguuni mwa Yesu, tunaweza kupata neema yote tunayohitaji ili kukombolewa kutoka kwenye uadui wetu uliofichika na kupatanishwa na Mungu na kupokea upatanisho.

Kazi ya sheria inawakilishwa na Musa kwa sababu sheria ilitolewa kwake. Lakini Mungu aliandika sheria na kumpa Musa. Hatupaswi kufikiri kwamba hii ina maana kwamba sheria imetungwa na mwanadamu - Kristo alimpa Musa sheria kupitia malaika wake.

*Maana torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; bali neema na kweli zilikuja kwa njia ya Yesu Kristo. Yohana 1:17*

*Kwa maana kuna Mungu mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu.1Timotheo 2:5*

*Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi;* ***iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe.*** *Wagalatia 3:19 (KJV).*

Bila sheria kuleta usadikisho wa dhambi mioyoni mwetu, hatungeweza kamwe kujua undani wa upotovu wetu. Huwezi kupata uponyaji bila utambuzi sahihi. Sheria hutambua tatizo letu wakati uadui wetu uliofichika unapofichuliwa. Katika mahali pale pale tunapofichuliwa Kristo anatusihi kwamba tumesamehewa na hii inatuwezesha kukombolewa kutoka kwenye uadui.
Paulo anaendelea katika Wagalatia:

*Basi je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! Kwa kuwa, kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha, yakini haki ingalipatikana kwa sheria. Wagalatia 3:21*

Sheria haipingani na ahadi za Mungu. Sheria haiwezi kutoa uzima, bali jukumu lake ni kukupeleka kwa yule aliye na uzima.

*(kwa maana ile sheria haikukamilisha neno); na pamoja na hayo kuliingizwa matumaini yaliyo mazuri zaidi, ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu. Waebrania 7:19 (KJV)*

Ukitoa neno lililotolewa na wafasiri, basi utabakiwa na upatanifu mkamilifu wa kile ambacho Daudi alikiandika katika Zaburi:

*Sheria ya BWANA ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amini, Humtia mjinga hekima. Zaburi 19:7*

Sheria haiwezi kumfanya mtu yeyote kuwa mkamilifu, lakini inaleta tumaini lililo bora zaidi. Hivi ndivyo inavyoongoa roho. Inatenda kama mwalimu wa shule kutuleta kwa Kristo. (Wagalatia 3:24). Kwa hiyo, Agano la Kale linazungumza na utu wa kale kwa lugha ya

kibinadamu. Huzungumza kwa njia ya kukuza mawazo yake mabaya kama vile ambavyo maneno ya Yesu yalivyoonekana kuonyesha kwamba hakutumwa kumsaidia yule mwanamke Mkanaani. Pale shida inapotokea na ukweli unapodhihirika, basi neema hutolewa kwa roho ili iweze kuja katika uzoefu wa Agano Jipya.
Huu ni mlango mwembamba wa kuingilia, kwa sababu Yesu alituambia kwamba ni wachache katika ulimwengu huu ambao watachagua kuingia kupitia mchakato huu wa kufichuliwa dhambi zao na kufunuliwa kupitia sheria, ili kupokea neema ya upendo wa Mungu unaosamehe.

Ikiwa tunatumia mfumo huu wa Agano la Kale na Agano Jipya kufanya kazi pamoja ili kutuleta kwenye wokovu, tunaweza kuweka baadhi ya mambo ambayo tumeyaangalia hapo awali katika mfumo huu ili kutupa picha ya wazi zaidi ya jinsi hili linavyofanya kazi.

| Agano la Kale | Agano Jipya |
|---|---|
| Piga Mwamba | Sema na Mwamba |
| Madhabahu ya Shaba — Ua | Sanduku la Dhahabu — Mahali Patakatifu pa Patakatifu |
| Mungu anahitaji Dhabihu | Mwanadamu anahitaji Dhabihu |
| Haki inadai kifo | Haki inatoa Rehema bure |
| Mungu alimuua Kristo | Mwanadamu alimuua Kristo |
| Mawazo ya Mwanadamu | Mawazo ya Mungu |
| Upatanisho wa Mwanadamu | Upataanisho wa Mungu |

Mawazo ya Mungu sio mawazo yetu, lakini Mungu hukutana nasi mahali tunapofikiri, na huleta wale ambao wako tayari katika

ufahamu wake. Kila mmoja wetu hupitia mchakato huu wa hatua mbili ili kuletwa katika maelewano na Mungu; kupokea upatanisho.

Utaratibu huu ni muhimu kuuelewa. Kwa kila mmoja wetu kupokea upatanisho, uadui uliofichika mioyoni mwetu lazima ufunuliwe [Agano la Kale] ili tuweze kupokea neema ya Mungu [Agano Jipya]. Tunapoelewa mchakato huu wa maagano mawili basi tunakuwa na mfumo sahihi wa kuelewa visa kama vile vya mauaji ya watoto wasio na hatia katika Hesabu 31.

SURA YA 11

# MAUAJI YA WASIO NA HATIA

Mojawapo ya kauli nzuri sana za Maandiko imejumuisha uadui usiofahamika.

> *Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao – na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika. Kutoka 32:32 (KJV).*

Katika Mlima Sinai, Musa anashindana akilini mwake kati ya mipaka ya msamaha wa Mungu na mfumo wa haki ambao watu wote wanauelewa - kifo kama adhabu ya uasi. Akiwa kijana, Musa alionyesha imani yake kwamba mwenye hatia lazima aadhibiwe kwa kifo.

> *Hata siku zile, Musa alipokuwa mtu mzima, akatoka kuwaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. Akamwona Mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake. Basi akatazama huko na huko, na alipoona ya kuwa hapana mtu, akampiga Mmisri yule, akamficha ndani ya mchanga. Kutoka 2:11-12*

Miaka arobaini Jangwani kuchunga kondoo, ililainisha kanuni hii ya kulipiza kisasi kwa Musa lakini bila ufunuo kamili wa tabia ya Mungu kama ilivyofunuliwa katika Kristo, ilikuwa vigumu sana kuondoa kabisa wazo hili potofu.

Mungu, akijua jinsi ilivyo vigumu kuondoa dhana potofu kama hizo zilizokita mizizi ndani ya mwanadamu na kutokuwa tayari kulazimisha ufahamu tofauti juu ya mwanadamu, humfundisha mwanadamu mahali alipo, akiandika maelezo ya kina ya majaribio Yake ya kumfikia mwanadamu, ili kwamba siku moja mwanadamu kwa baadaye anaweza kuunganisha vipande pamoja na kupata ufahamu sahihi zaidi wa tabia Yake na haki Yake. Haya ndiyo yote ambayo Mungu anaweza kuyafanya na yale ambayo ameyafanya kwa miaka 6000: Yeye hutembea na wanadamu kupitia ufahamu wao wenye giza wanapokula tunda chungu la uchaguzi lao, wakati wote huo akizungumza nao kwa upole kupitia Roho Wake kuhusu njia bora zaidi.

> *Basi huyo mtu Musa alikuwa mnyenyekevu sana kuliko wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi. Hesabu 12:3*

Musa alikuwa mtu mvumilivu zaidi, mwenye kujali sana duniani wakati huo na kungekuwa na wachache sana baada yake ambao wangemiliki kiwango chake cha unyenyekevu. Hata hivyo chuki iliyofichika ya Adamu bado ilikuwa imefichwa katika tabia ya Musa. Baba yetu wa mbinguni alitaka kumkomboa Musa kutoka katika uadui huo uliofichika.

Kama tulivyogundua katika sura iliyopita, njia pekee ya kufanya hivyo ilikuwa kuruhusu mielekeo ya asili ya Musa kuzidi katika hali ngumu. Hii ingeruhusu neema ya Mungu kuongezeka zaidi. Mara tu Musa alipoupiga mwamba huo mara mbili kwa hasira kwa sababu ya ukosefu wa imani wa watu, uadui uliofichika ndani ya Musa ulijitokeza. Kupigwa kwa mwamba ilikuwa ishara ya kupigwa kwa Kristo. Kabla Musa hajapanda Mlima Nebo na kwenda kaburini, Mungu angefunua kina cha uadui ndani ya Musa kiasi kwamba

ilionekana kuwa Musa alikuwa na tabia sawa na Farao ambaye alijaribu kumuua akiwa mtoto mchanga.

Katika sura ya 9 tuliona kuuawa kwa wenye hatia ndani ya Israeli kwa kuruhusu ibada ya uongo na uasherati kambini. Sasa ulikuwa wakati wa taifa la Midiani lenye hatia kuvuna kile lilichopanda. Mungu anazungumza na Musa:

*Walipize kisasi wana wa Israeli juu ya Wamidiani; kisha baadaye utakusanywa uwe pamoja na watu wako. Hesabu 31:2*

Hapa kuna kazi ya mwisho kwa Musa kabla hajafa; kisasi juu ya Wamidiani. Lakini ni kisasi cha nani kilikuwa kinaridhishwa hapa? Zingatia tafsiri zingine mbili:

*"Lipiza kisasi cha wana wa Israeli juu ya Wamidiani, kisha utakusanywa kwa watu wako." Hesabu 31:2 (YLT)*

*Na [lipiza kisasi kwa wana wa Israeli] juu ya Wamidiani; na mwisho utaongezwa kwa watu wako. Hesabu 31:2 (Apostolic Polyglot)*

Musa na Waisraeli walielewa nini kwa kulipiza kisasi?

*Basi Musa akanena na watu, na kuwaambia, Wavikeni silaha baadhi yenu kwa vita, nao waende kupigana na Wamidiani, ili kulipiza kisasi kwa ajili ya Bwana juu ya Midiani. Hesabu 31:3*

Kisasi kwa Musa kilimaanisha kuwaua na kuwaangamiza wale waliofanya makosa. Musa alionyesha kisasi cha kibinadamu kama kisasi cha Mungu. Hii inadhihirisha kwa Mungu sifa za tabia za Israeli, akiwemo Musa. Usaliti wa hila wa Balaamu katika ushirika na Wamidiani unasababisha kosa la Musa kuwa kubwa. (Warumi 5:20). Mungu alisema na Musa juu ya kisasi cha wana wa Israeli. Musa alisema juu ya kisasi cha Yehova. Musa anawaambia Waisraeli kujizatiti kwa ajili ya vita. Mungu hakutaja neno vita au kuwa na silaha. Je, Mungu hujilipiza vipi kisasi kwa adui zake?

*Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu; kwa maana imeandikwa, kisasi ni juu yangu mimi, mimi nitalipa, asema Bwana. Kwa hiyo* ***"Adui yako akiwa na njaa, mpe chakula; akiwa na***

> ***kiu, mpe maji ya kunywa; maana kwa kufanya hivyo utampalia makaa ya moto juu ya kichwa chake."*** *Warumi 12:19–20*

Kisasi cha Mungu ni kuwalisha adui zake na kuwapa kitu cha kunywa wanapoona kiu. Adui yako anapokuwa na fadhili kwako, hutesa dhamiri (ikiwa kuna dhamiri yoyote iliyobaki) na husababisha usumbufu mkubwa kwa roho. Hivi ndivyo Mungu anavyowageuza adui zake, ambao ni pamoja na watu wote katika hali yao ya asili, kuwa marafiki zake—wema Wake kwetu hutuongoza kwenye toba na upatanisho. (Warumi 2:4).

Elisha aliwatendeaje adui zake?

> *Naye mfalme wa Israeli alipowaona, akamwambia Elisha, Ee baba yangu, niwapige? Niwapige? Akamjibu, Usiwapige; je! Ungetaka kuwapiga watu ambao umewatwaa mateka kwa upanga wako na uta wako? Weka chakula na maji mbele yao, wapate kula na kunywa, na kwenda kwa bwana wao. Basi akawaandalia chakula tele; nao walipokwisha kula na kunywa, akawaacha, wakaenda zao kwa bwana wao. Na vikosi vya Shamu havikuja tena katika nchi ya Israeli. 2 Wafalme 6:21-23*

Kwa nini makundi ya wavamizi wa Siria hayakuja tena katika nchi ya Israeli? Ni kwa sababu ya makaa ya moto juu ya vichwa vyao. Askari hawa walidhani watakufa. Badala ya kuuawa walifanyiwa karamu kubwa iliyofika mioyoni mwao na kuwafanya waaibike kwa kutaka kuwaua Waisraeli, kwa hiyo wakaacha.

> *Hakuna giza ndani ya Mungu, lakini kama wanadamu wanaomwakilisha Mungu hawaelewi tabia Yake, hii husababisha giza kumzunguka Mungu.*

Lakini kama tulivyosema, haikuwa kisasi cha Mungu kilichokuwa kikitekelezwa; kilikuwa kisasi cha Israeli. Musa aliupiga mwamba,

mfano wa Kristo, tena kwa kusema kwamba kilikuwa kisasi cha Mungu ambacho kilikuwa kikitekelezwa. Lilikuwa ni dhihirisho la uadui uliofichika ambao ulianzia katika moyo wa Adamu.

Mtu mpole zaidi katika dunia yote ghafula anafunua uadui uliofichwa ndani yake katika tamaa ya kuwaua Wamidiani. Ikiwa Mungu hangesema kile Alichofanya, uadui huu uliofichwa usingeweza kujitokeza.

Ni kutoelewa maana ya Mungu ndiko kunakomfanya Mungu kufunikwa na giza. Hakuna giza ndani ya Mungu, lakini kama wanadamu wanaomwakilisha Mungu hawaelewi tabia Yake, hii husababisha giza kumzunguka Mungu.

> *BWANA ametamalaki, nchi na ishangilie, Visiwa vingi na vifurahi.* ***Mawingu na giza vyamzunguka,*** *Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chake. Zaburi 97:1–2*

Mawingu haya ni nini?

> *Basi na sisi pia,* ***kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi*** *namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, Waebrania 12:1*

Katika kitabu cha Waebrania, Paulo anakusanya orodha ya mashujaa wengi wa Agano la Kale. Hawa ni mashahidi kwa Mungu katika historia. Bado kutoelewa kwao tabia ya Mungu kunasababisha Mungu kuzingirwa na mawingu meusi. Nuru ya Mungu inatafuta kuangaza kupitia giza hili. Ni ndani ya utu wa Yesu ndipo nuru safi huangaza gizani.

> ***Kwa maana Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa katika giza,*** *ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo. 2 Wakorintho 4:6 (KJV)*

Mungu alipozungumza na Israeli kwenye Mlima Sinai, alizungumza nao kupitia mawingu ya giza. Giza hili halipo kwa Mungu bali katika

ubinadamu. Tetemeko la ardhi, umeme na radi ni onyesho la mawazo ya wanadamu kuhusu Mungu.

> *Ikawa siku ya tatu, wakati wa asubuhi,* ***palikuwa na ngurumo na umeme, na wingu zito juu ya mlima,*** *na sauti ya baragumu iliyolia sana. Watu wote waliokuwa kituoni wakatetemeka. Musa akawatoa hao watu katika kituo, akawaleta ili waonane na Mungu; wakasimama pande za chini za kile kilima. Mlima wa Sinai wote pia ukatoa moshi, kwa sababu BWANA alishuka katika moto; na ule moshi wake ukapanda juu kama moshi wa tanuu, mlima wote ukatetemeka sana. Kutoka 19:16–18*

> *Watu wote wakaona umeme na ngurumo na sauti ya baragumu, na ule mlima kutoka moshi; na watu walipoona hayo wakatetemeka, wakasimama mbali. Wakamwambia Musa, Sema nasi wewe, nasi tutasikia, bali Mungu asiseme nasi, tusije tukafa. Musa akawaambia watu, Msiogope, maana Mungu amekuja ili awajaribu, na utisho wake uwe mbele yenu, ili kwamba msifanye dhambi. Basi hao watu wakasimama mbali, naye Musa akalikaribia lile giza kuu Mungu alipokuwapo. Kutoka 20:18-21*

Mungu aliruhusu vipengele vya asili kuakisi kile wanadamu wanachofikiri kuhusu Mungu. Ardhi ilikuwa chini ya himaya ya watu na ilishuhudia yale waliyokuwa wakimfikiria Yeye. Kwa utaratibu huu Mungu anasababisha sheria iingie ili dhambi ya wanadamu ipate kuwa dhahiri zaidi kwao.

Kama tulivyotangulia kusema, ni muhimu kwamba kina cha uadui ndani ya Musa kifichuliwe kabla hajafa. Mungu hafanyi hivi ili kumhukumu Musa, bali ili Musa apate neema nyingi. Mungu halaani kamwe; husadikisha tu kuleta uponyaji wa uadui kwa upatanisho wa kina zaidi, lakini ni mwanadamu ambaye, katika kutoelewa kwake, anaona kazi hii ya kusadikisha kuwa ni ya kuhukumu, na katika hatia na hofu anaangamia.

Israeli waliingia vitani na Midiani wakiwa na mawazo ya kwamba wanapigana vita vya Mungu na kulipiza kisasi chake. Wamidiani

waliangamizwa. Israeli walihakikisha kwamba Balaamu, yule nabii wa uongo, aliangamizwa pia. Lakini wanaporudi, Musa anatenda kwa hasira kali.

*Musa akawakasirikia majemadari wa jeshi, na hao maakida wa elfu elfu, na wakuu wa mia mia, hao waliorudi kutoka katika kupiga vita. Musa akawauliza, Je! Mmewaponya wanawake wote hai? Tazama, hawa ndio waliowakosesha wana wa Israeli, kwa shauri la Balaamu, wamfanyie BWANA dhambi katika hilo jambo la Peori, na kwa hivyo pigo lilikuwa katika mkutano wa BWANA. Basi kwa ajili hiyo mwueni kila mume katika hao watoto, na kila mwanamke aliyemjua mume kwa kulala pamoja naye. Hesabu 31:14–17*

Je, Mungu alimwambia Musa lolote kuhusu kuwaua watoto wa kiume?

Ni katika njia gani watoto wachanga wa kiume wa Midiani walikuwa wamewashawishi Waisraeli na kusababisha tauni kuwaangamiza Waisraeli 24,000? Wanawake wote ambao wamewahi kulala na mwanamume waliuawa. Lakini wasichana ambao hawakulala na mwanamume waliwekwa hai ili wafundishwe kulala na wanaume Waisraeli na kuwa watumwa wao.

Si vigumu kuelewa mantiki ya kibinadamu kwa nini wanawake waliuawa lakini kwa nuru ya tabia ya Yesu ambaye alimsamehe mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi, inatufunulia sisi sote mioyo yetu iko wapi kwenye swali hili.

Uhai wa Musa uliokolewa wakati Farao wa Misri alipoamuru kwamba watoto wote wa kiume Waisraeli wauawe na watoto wa kike waachwe.

*Kisha mfalme wa Misri akasema na wazalisha wa Waebrania, mmoja jina lake aliitwa Shifra, na wa pili jina lake aliitwa Pua; akasema, Wakati mwazalishapo wanawake wa Kiebrania na kuwaona wa katika kuzaa, ikiwa ni mtoto mwanamume, basi mwueni, bali ikiwa ni mtoto mwanamke, na aishi. Kutoka 1:15–16*

Cha kuvutia pia ni kwamba Musa alipokimbia Misri alipata kimbilio katika nchi ya Midiani.

> *Farao aliposikia jambo hili, akataka kumwua Musa. Lakini Musa akakimbia mbele ya Farao, akakaa katika nchi ya Midiani; akaketi karibu na kisima. Kutoka 2:15*

Musa alimwoa binti Yethro, kuhani wa Midiani. (Kutoka 2:16-21). Mambo haya yote yanapaswa kutufanya tutetemeke. Musa alikuwa mtu mpole zaidi aliyepata kuishi. Jaribio lililo sahihi lilipokuja, ilifunuliwa kwamba Musa angeweza kuonyesha tabia zile zile kama Farao ambaye alitaka kuwaua watoto wa Israeli.

Ikiwa kweli unataka kujua kile kilichofichwa ndani ya nafsi yako, tazama uso wa Musa na ujione mwenyewe. Mambo haya yote yaliandikwa kwa ajili ya kujifunza kwetu. (Warumi 15:4). Hakuna kitu kizuri kwa mwanadamu; hakuna wamtafutao Mungu. (Warumi 3:11–12 ). Kama Yesu alivyotuambia, hakuna aliye mwema ila Mmoja, Mungu.

Katika mauaji ya wafalme wa Midiani, tunaona dhabihu ya wenye hatia. Katika wanawake waliokuwa wamewatongoza wanaume Waisraeli, tunaona pia dhabihu ya wenye hatia. Katika kifo cha wanawake ambao hawakuwadanganya Israeli na wavulana wa Midiani, tunaona dhabihu ya wasio na hatia - na hii inakamilisha upatanisho wa Mbadala wa Adhabu. Yote hayo yana mwangwi wa shtaka la bustani "yule mwanamke ambaye wewe, (Mwana), ulinipa.": mwanamke mwenye hatia na Mwana asiye na hatia wanahukumiwa kifo ili kukamilisha upatanisho kwa ajili ya Adamu.

Sehemu ya sura hii iliyobakia inazungumzia nyara za vita na jinsi zilivyogawanywa na kile kilichowekwa wakfu kwa Mungu. Kisha tunasoma jambo muhimu sana juu ya somo la upatanisho.

> *Nasi tumeleta matoleo ya BWANA, aliyopata kila mtu, ya vyombo vya dhahabu, na mitali, na timbi, na pete za muhuri, na vipini, na vikuku, ili kuzifanyia upatanisho nafsi zetu mbele ya BWANA. Hesabu 31:50*

Katika kuwaua Wamidiani na kuchukua nyara za vita na kutoa dhabihu kwa Mungu, Waisraeli walifanya upatanisho kwa ajili yao wenyewe. Lakini wanadamu wanafanyaje upatanisho kwa ajili yao wenyewe wakati hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja? Kama vile Mungu alivyokuwa amesema, kisasi cha Israeli kilikuwa kinatimizwa, kwa hiyo upatanisho uliofanywa ulikuwa kwa ajili yao wenyewe.

Kwa muda mfupi, Musa anaonekana kama Farao, akiwa na uzao uleule wa uadui unaosukumwa na tamaa ya kuhifadhi taifa lake. Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba Mungu hamhukumu mtu ye yote kwa kushindwa kwake bali atawaonyesha ukweli ili apate kuwapa rehema na uponyaji wa kiroho ikiwa watakubali ukweli.

Watu wengi wanashtushwa na pendekezo la kwamba Musa alitenda vibaya. Hili ni jaribio la kuhalalisha uadui uliojificha ndani ya mioyo yao. Yesu hakuwahi kuamuru kuuawa kwa yeyote; si sehemu ya tabia yake. Kristo alivumilia Msalaba katika kifo cha Wamidiani hao wote, ili mchakato wa injili ndani ya Musa ukamilike.

Usifanye makosa, Wamidiani walipokea matokeo ya asili ya uchaguzi wao. Walikuwa wakitafuta kuharibu Israeli na Mungu akaruhusu maovu ya baba zao yapatilizwe kwa watoto. Mungu hakuzuia matokeo ya kuanguka, lakini tabia ya Mungu haijawakilishwa katika mauaji ya Wamidiani.

Ni maombi yangu kwamba katika kusoma hadithi hizi kwa macho mapya kanuni za upatanisho zitachukua umuhimu mkubwa zaidi. Ninaomba kwamba upotovu wa asili yote ya mwanadamu ufunuliwe na kuwekwa mavumbini ili sisi sote tushikamane na Kristo kama tumaini letu la wokovu. Hakuna aliye mwema, hakuna hata mmoja. Ndiyo maana historia hii tumeipewa; 'imeandikwa ili kuwa maonyo kwa ajili yetu sisi, ambao tumefikiwa na utimilifu wa nyakati. 1 Wakorintho 10:11 (NIV).

Sisi sote tuna mwili sawa na Musa na Farao. Tuna uwezo wa kufanya kama walivyofanya hata ikiwa sisi ni watu wapole zaidi duniani.

Kisha, tunageukia Patakatifu ili kuelewa kwa undani zaidi jinsi Mwana wa Mungu anavyoshughulika na chuki yetu iliyofichwa ili kutuleta katika upatanisho na Mungu.

SURA YA 12

# PAZIA LA MWILI WAKE

*Ee Mungu, njia yako i katika patakatifu; Ni nani aliye Mungu mkuu kama Mungu wetu? Zaburi 77:13*

Maana ya msingi ya neno njia ni "barabara". "Barabara yako iko katika Patakatifu." Sehemu ya kuanzia ya barabara ni pale ambapo mwanadamu aliyeanguka ameketi gizani, na mwisho ni pale Baba wa nuru anapowakilishwa. Barabara kati ya ncha hizi mbili inafunuliwa katika Patakatifu, inayomwakilisha Kristo. Sambamba na hili Yesu anasema "Mimi ndimi Njia" ambayo kwa Kigiriki ni τρόπος ambayo pia humaanisha njia au barabara. "Njia yako, Ee Mungu, i katika Patakatifu" na Kristo ndiye njia ya kwenda kwa Baba. Yesu anasema, "Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi." Njia hii Inaanzia pale mwanadamu alipo, na inaishia pale Mungu alipo.

Anza




Sasa, kwenye barabara hii, tunaweza kuweka nyanja nyingine ya ufahamu na hiyo ni Isaya 55:8–9. Tukiweka hilo kwenye chati hii, tunazo njia za mwanadamu na njia za Mungu.

Anza | **MWANADAMU** Njia za Mwanadamu | **MUNGU** Njia za Mungu

Kuna tofauti gani kati ya hizo mbili? Tofauti kati ya haki na dhambi. Ziko kinyume kabisa. Njia, ili kutoka kwenye njia za mwanadamu kwenda kwenye njia za Mungu, inapitia mabadiliko kamili kama inavyowakilishwa mahali pengine katika Maandiko kama giza hadi nuru.

Tunayo aya nyingine tunayoweza kuweka juu ya hili. Ezekieli 36:26, "Nitautoa moyo wa jiwe katika mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama."Hatusemi kwamba Mungu ni mwili bali inawakilisha ulaini, upole, upole wa Mungu kuliko ukatili, ukali na ugumu wa tabia ya mtu. Haya ni baadhi ya mfanano ambapo kuna kinyume. Ili Mungu atukomboe na kutufikia, Mungu alimtuma Mwana wake wa pekee. Ilimbidi Mungu amtume Mwanawe hadi hapa tulipo.

Tunawakilishwa na kondoo waliopotea. Kristo anakuja kwetu kwa sababu "Hakuna amtafutaye Mungu." (Warumi 3:11). Mwanadamu hatembei kumwelekea Mungu. Kristo anatembea au anakimbia kuelekea kwa mwanadamu ili kuwachukua wale walio tayari kuwarudisha kwa Baba.

Hali ya mwanadamu katika giza la dhambi ni mbaya kwa sababu nuru ya haki inapotujia, Biblia inatuambia kwamba kwa kawaida tunaiacha nuru. Kwa asili, hatuielewi nuru wala kuitamani.

> *Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza. Yohana 1:5*
>
> *Na hii ndiyo hukumu, ya kwamba nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru, kwa maana matendo yao yalikuwa maovu. Yohana 3:19*

Kwa kuwa mawazo ya Mungu si mawazo yetu, kila kitu anachokisema kinafasiriwa katika giza letu kama kitu kilicho kinyume chetu na chenye madhara kwetu. Tunaona haya kwa wana wa Israeli katika Mlima Sinai:

> *Kuonekana kwa utukufu wa BWANA kulikuwa kama moto uteketezao juu ya kilele cha mlima, machoni pa wana wa Israeli. Kutoka 24:17*

Utukufu mzuri wa Mungu ulionekana kama moto ulao au uteketezao kwa watu. Ili Mungu amfikie mwanadamu, ilimbidi aje pale mwanadamu alipokuwa. Lakini Mungu anapotujia, kwa kawaida tunaogopa kwamba anakuja kutudhuru kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa hiyo tunahitaji mpatanishi wa kutuombea mambo yetu mbele ya Yule tunayemdhania kuwa anataka adhabu na kifo chetu.

Uadui ulioanzia katika moyo wa Adamu dhidi ya Mungu na kupita kwa jamii yote ya wanadamu unazuia uwezekano wa mawasiliano yenye matokeo bila mpatanishi. Mpatanishi kama huyo ni Kristo, Mwana wa Mungu.

> *Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani. Waefeso 2:13–15*

Kristo aliushinda ukuta wa utengano kati yetu na Mungu kupitia pazia la mwili wake. Wakristo wengi wanaamini kifungu hiki kinarejelea ukuta kati ya Myahudi na Mmataifa uliobomolewa kwa kuondolewa kwa sheria ya Musa. Ona kile ambacho Biblia Habari Njema inakisema:

> *Kwa maana* ***Kristo mwenyewe ametuletea amani kwa kuwafanya Wayahudi na watu wa mataifa kuwa watu mmoja****. Kwa mwili wake mwenyewe aliubomoa ukuta uliowatenganisha na kuwaweka maadui.* ***Aliifuta Sheria ya Kiyahudi*** *pamoja na amri zake na kanuni zake, ili kuunda kutoka katika jamii hizo mbili watu wamoja wapya katika muungano na yeye*

*mwenyewe, kwa njia hiyo kufanya amani. Waefeso 2:14–15 (Biblia Habari Njema)*

Watu wengi wanaelewa neno *amri* kama lililoonyeshwa katika King James kama likirejelea sheria ya Musa. Hii ni tafsiri ya neno la Kiyunani *dogma.*

Ukichunguza Agano la Kale la Kiyunani (LXX) juu ya neno dogma, hairejelei kamwe sheria ya Musa bali amri zilizotungwa na mwanadamu na mara nyingi amri za adhabu na kifo.

- Ezra 6:8 - Amri ya Kiajemi ya kujenga hekalu.
- Ezekieli 20:26 kutoka mstari wa 25 - Mungu aliwaacha wafuate sheria ambazo hazikuwa nzuri. Mungu aliwaharibu kwa amri zao wenyewe.
- Danieli 2:13 - Amri ya kifo ya kuwangamiza wenye hekima.
- Danieli 3:10, 29 - Amri ya kifo katika uwanda wa Dura na mfalme wa Babeli.
- Danieli 4:6 - Amri ya kuwaleta wenye hekima wote.
- Danieli 6:8, 10, 12, 13, 15, 26 - Ishara amri ya kifo ya kutomwabudu Mungu ila mfalme.

Hivi ndivyo neno hilohilo limetumika katika Agano Jipya:

- Luka 2:1 - Amri ya Kaisari.
- Matendo 16:4 - Amri ya Mitume kuweka mipaka ya kile kinachofundishwa kutoka kwenye sheria ya Musa kutokana na msimamo wa kupita kiasi wa baadhi ya Wayahudi juu ya swali hili.
- Matendo 17:7 - Amri ya Kaisari.
- Waefeso 2:15 - Kristo amebatilisha amri zilizomo katika maagizo (za kibinadamu).

- Wakolosai 2:14 - Kufuta kabisa amri za kibinadamu zilizokuwa dhidi yetu.

Ukiangalia jinsi neno hili amri lilivyotumika katika Biblia nzima linaonyesha kwamba halina uhusiano wowote na sheria ambazo Musa aliandika katika Agano la Kale. Badala yake, linazungumzia sheria na matakwa ya binadamu na mara nyingi sheria zinazohusisha adhabu na kifo. Je, unaona jinsi uadui ndani ya mwanadamu unavyomfanya aelewe kile ambacho Paulo anakisema kama kuondoa sheria ya Mungu iliyotolewa kupitia kwa Musa badala ya kuondoa amri za kuhukumu za wanadamu?

Kama tulivyojadili katika sura ya nne kuhusu uovu uliofichika wa Adamu, amri ya kwanza ya mwanadamu ilikuwa kwamba Mwana wa Mungu afe kwa ajili ya matukio yaliyotokea katika bustani ya Edeni. Adamu alipitisha aina hii ya hukumu kwa watoto wake wote na hivyo hukumu hii inakaa ndani ya watu wote katika hali yao ya asili. Asili ya mwanadamu inajaribu kuficha chuki hii na kudai kumpenda Mungu, sawa na raia wa taifa la kiimla ambao wanaogopa kuuawa ikiwa hawatamheshimu mkuu wa nchi (Mfano: Korea Kaskazini).

Ili kutufikia, Kristo ilimbidi kuchukua mwili wetu ili kuubomoa ukuta wa utengano ulioundwa na mfumo wetu wa haki wa uongo ambao ulisababisha hukumu na adhabu za kifo. Kwa kuwa mmoja wetu, angeweza kutetea kesi yetu mbele ya Baba ambaye tunafikiri kimakosa yuko kinyume na sisi na kulipa gharama ambayo tulifikiri kimakosa ilihitaji kulipwa. Angeweza kuonyesha mwanadamu njia ya kweli ya kuhusiana na Mungu, bila mawazo ya ibada ya sanamu ya tabia Yake na kutokuwa na hali iliyokandamizwa sana ya kutomtumaini.

> *Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema, Dhabihu na toleo hukutaka, Lakini mwili uliniwekea tayari; Waebrania 10:5*

Haki ya Mungu haikudai kifo hiki. Hakutaka kamwe dhabihu, lakini badala yake mwili wa mwanadamu ulitayarishwa kwa ajili ya Yesu ambao ungemruhusu kuja karibu nasi. Mwili huo wa mwanadamu

haukuwa wa uzao wa Adamu kabla ya anguko, bali ulikuwa uzao wa Daudi baada ya anguko la mwanadamu.

> *Habari za Mwanawe Yesu Kristo Bwana wetu,* ***aliyetoka katika uzao wa Daudi kwa jinsi ya mwili.*** *Warumi 1:3 (KJV).*

Kristo akitwaa mwili wetu juu Yake, aliutiisha utukufu ndani Yake kwa kadiri ambayo tungeweza kustahimili kuwa mbele zake. Ikiwa Kristo angekuja katika mwili tofauti na wetu, uadui na hukumu ndani yetu vingeelekezwa Kwake na kama Adamu aliyekimbia bustanini, tungemkimbia. Utukufu wake ungefunuliwa ungeonekana kama moto uteketezao machoni petu.

Tunaona uthibitisho wa hilo tangu Yesu aliposafisha hekalu la Yerusalemu. Uungu ukamulika kutoka Kwake na wale waliokuwa na uadui mioyoni mwao dhidi ya Kristo mara moja walikimbia kuokoa maisha yao. Kwa vile sisi sote tuna uadui huu, hakuna hata mmoja wetu ambaye angeweza kubaki katika uwepo Wake, kwa hiyo aliuvisha uungu Wake kwa ubinadamu - ubinadamu wetu, na akaja karibu nasi na kutusadikisha kwamba angeweza kuzungumza na Baba kwa niaba yetu.

Ikiwa Kristo angemfikia mwanadamu katika hali yake ya uungu, angeonekana kwetu kama Baba yake. Kristo akiwa kioo kamili angemfanya mwanadamu amwone Kristo akija kwa nia ya kumwua. Mwanadamu anaona amri ya kifo ikimjia ili kumuua kwa sababu muda wote anafikiri hukumu za kifo; anadhani Mungu anafikiri kama yeye. (Zaburi 50:21).

Katika kuchukua asili yetu Kristo angeweza kuondoa uadui huu ulioakisiwa; Angeweza kuufunika kwa mwili wetu ili kwamba nguvu ya chuki yetu kwake isiweze kuakisiwa kwetu kwa nguvu sana. Kanuni hii inachukua muda kidogo kuielewa lakini unapoweza kuona kwamba hukumu ilitoka kwa Adamu na si kwa Mungu, basi tunaweza kufahamu kwamba hukumu yoyote tunayoona kwa Mungu ni mitazamo yetu wenyewe iliyoelekezwa kwake.

Kuna kina cha maana katika Waebrania 10:5 kama inavyohusiana na upatanisho. Mungu hakutaka dhabihu au kafara bali mwili wa mwanadamu ulitayarishwa kwa ajili ya Kristo ili kwamba katika mwili huu aweze kuondoa uadui, kudhihirisha tabia ya Baba, na wakati huohuo atambulikane kikamilifu na jamii ya wanadamu, akiwa amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria. (Wagalatia 4:4).

Asili ya mwanadamu ya Kristo inahusishwa kwa karibu na somo la upatanisho. Vyote viwili katika uwezo Wake wa kushinda uadui wetu na kuja karibu nasi duniani, pamoja na kustahili Yeye kuwa mpatanishi wa kweli wa mwanadamu kwa Mungu.

> *Kwa maana hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi Waebrania 4:15 (KJV).*

> ***Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na nyama, yeye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo****, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi. Waebrania 2:14*

Kristo ndiye mhusika mkuu aliyeelezewa katika mifano katika muundo wa Patakatifu aliopewa Musa. Kristo alipewa mwili ili akae nasi kama inavyoonyeshwa katika mfano katika mstari huu:

> *Na wanifanyie patakatifu, ili nipate kukaa kati yao. Kutoka 25:8*

Paa la Patakatifu lilifunikwa na ngozi ambazo zilificha kuta za dhahabu zinazong'aa na samani zilizokuwa ndani. Kristo alipokuja hapa duniani, hakuwa na uzuri wa nje ili tuweze kumtamani. ( Isaya 53:2 ).

Huduma ya Patakatifu ni mfano wa mchakato ambao Kristo anaupitisha ubinadamu ili kufika kwenye upatanisho. Kuna mwendelezo katika upatanisho, kwa sababu ya kuongezeka kwa ufahamu juu yetu wenyewe na wa Mungu.

Kristo aliufunika uungu wake na ubinadamu ili kutufikia mahali tulipo. Kisha anatuongoza katika njia ya Patakatifu hadi Patakatifu pa

Patakatifu. Pazia lililotenganisha kati ya Mahali Patakatifu na Patakatifu Zaidi pa Patakatifu linaashiria pazia la mwili wa Kristo. Patakatifu pa Patakatifu huwakilisha hali ya uungu ya Kristo na Mahali Patakatifu huwakilisha asili ya ubinadamu yake Kristo. Ua wa nje ndipo Kristo anapokutana nasi katika fikra zetu za shaba zilizotengenezwa na mwanadamu.

Vyumba viwili vya hema ni jengo moja linalowakilisha asili mbili zilizounganishwa katika moja.

Amri ya kifo iliyowekwa kwa Kristo kupitia mfumo wa haki wa Shetani kama inavyowakilishwa juu ya madhabahu ya shaba inaonyesha kifo cha Kristo Msalabani. Kristo hutosheleza haki ya kibinadamu ili kwamba aweze kutushika mkono kama mpatanishi wetu na kutuongoza mbali na mawazo yetu ya shaba kuelekea yale ya dhahabu ya tabia ya Baba yake. Kristo anatupitisha katika Patakatifu, njia mpya na iliyo hai hadi kwa Baba.

> *Kwa njia mpya na iliyo hai aliyoiweka wakfu kwa ajili yetu, kupitia lile pazia, yaani, mwili wake. Waebrania 10:20*

NJIA YAKO IKO KATIKA PATAKATIFU



Patakatifu hutupatia vidokezo vya kuendelea kwa njia kutoka Ua hadi Patakatifu Zaidi. Samani zote katika Ua ni za shaba, ambayo inawakilisha mawazo ya mwanadamu kuhusu upatanisho. Madhabahu ya shaba inawakilisha kuuawa kwa Mwana wa Mungu kwa uadui ulio ndani ya mwanadamu uliorithiwa kutoka kwa Adamu.

Tulimdhania Kristo amepigwa na Mungu na kuteswa (Isaya 53:4) madhababahuni. Mitazamo yetu ya haki inayodai adhabu hutufanya kumwona Kristo kuwa anakufa ili kukidhi haki ya Mungu wakati ukweli ni kukidhi haki yetu na kufichua uadui wetu dhidi ya Mungu na Mwanawe.

Kwa mtazamo wetu mbaya juu ya Mungu, tunaungama dhambi zetu kwenye madhabahu ya dhabihu, na kuwa na matumaini kwamba Mungu kweli anatusamehe kwa sababu tuna mwombezi wa kuwasilisha hoja zetu. Roho wa Yesu ndipo anaanza kutusafisha kwenye birika. Akili zetu zinaanza kufunguka kwa neno la Mungu na tunaanza kubadilika. Tunapoingia Mahali Patakatifu, kina cha uadui wetu dhidi ya Mungu kinawezeshwa kuchukulika kwa pazia lililo kati ya Patakatifu na Patakatifu Zaidi. Hili linaturuhusu sisi kuingia katika chumba cha kwanza.

Tunapoingia Mahali Patakatifu, Kristo hutulisha kwa maana Yeye ndiye mkate wa uzima. ( Yohana 6:48 ). Pia anatupa nuru kwa maana Yeye ni nuru ya ulimwengu. (Yohana 8:12 ). Pia anatuombea kwa kuwa yeye ndiye mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu. (1 Timotheo 2:5). Kadiri tunavyomkaribia Mungu ndivyo hisia ya hukumu inavyozidi kuwa kali kwa sababu ya uadui ambao ungali ndani yetu. Lakini dhambi hii inapoongezeka, neema inaongezeka zaidi kwa wale wanaoamini.

Wakristo walio wengi walisimama njiani. Wanapozidi kufahamu tabia zao mbovu wanapokaribia Patakatifu pa Patakatifu, Shetani huwajaribu kuelekeza uovu wao wenyewe kwa wengine badala ya kusulubishwa pamoja na Kristo. Njia ni nyembamba kama Yesu

asemavyo na ni wachache wanaoipata kwa sababu wanadamu wanapenda giza kuliko nuru.

Kwa wale wanaomshikilia Yesu kwa imani, tunaendelea kujilisha mkate ulio hai na njia yetu inaangazwa, tunaanza kujifunza zaidi kuhusu asili zetu potovu. Sheria huanza kuingia kwa undani zaidi ndani ya mioyo yetu na tunakubali kwa uchungu jinsi tabia zetu zinavyochukiza. Yesu anatutia moyo kwa neema, rehema na msamaha wake. Kadiri tunavyoona jinsi tulivyo waovu, ndivyo majaribu ya kuogopa adhabu na kuelekeza adhabu hii kwa wengine huongezeka. Hisia zetu potofu za haki hutufanya tuogope kwamba tutaadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu. Tunajaribiwa kuwa na mashaka ikiwa kama tunaweza kusamehewa.

Ili kukabiliana na mashaka, kama tulivyosema, wengine hujikita katika dhambi za wengine na kutaja wazi makosa na udhaifu wao, wakitaka kugeuza fikira kutoka kwenye dosari zao wenyewe. Kupitia haya yote, Roho wa Yesu anatuvuta tuitafakari tabia yake ya rehema na msamaha. Tunapokaribia Patakatifu pa Patakatifu, tunaalikwa kuona kwamba Mungu hataki dhabihu na sadaka.
Isipokuwa tunaweza kuwa huru kutoka kwenye uadui wa haki ya uongo, hatutaweza kuingia Patakatifu pa Patakatifu. Kadiri tunavyomkaribia Mungu, ndivyo mfumo wetu wa haki wa uwongo utakavyoakisi tabia yake. Kristo anafunika uadui huu tukiwa katika Mahali Patakatifu, lakini tusipopata uhuru kutoka katika ufahamu mbaya wa haki, hatutakuwa huru kamwe dhidi ya hofu ya kifo.

Kwa kadiri tunavyoshikilia wazo kwamba Mungu atawaangamiza waovu, (badala ya kuwa ni matokeo ya asili ya maamuzi yao), tutakuwa na hofu ya adhabu. Kila wakati dhambi zetu zinapofunuliwa kwetu, tutajaribiwa kuogopa kwamba tutashindwa na kupotea.

> *Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo. 1 Yohana 4:18*

Mungu ni upendo na tunapomjua Mungu jinsi alivyofunuliwa katika Mwanawe, tutajua kwamba Baba yetu hamdhuru au kuua mtu yeyote. Kisha tunaweza kutubu tabia zetu za kuhukumu ambazo zinadai kifo na uadui unaweza kuuawa ndani yetu. Hili litatuweka huru kutembea katika Patakatifu Zaidi.

*Mungu ni upendo na tunapomjua Mungu jinsi alivyofunuliwa katika Mwanawe, tutajua kwamba Baba yetu hamdhuru au kuua mtu yeyote.*

Tunapoacha kushikilia tena amri ya kifo ndani yetu kwa njia ya haki ya uongo, hatutaiona tena ikiakisiwa katika tabia ya Mungu. Kwa kuwa woga wetu umetoweka, hatutahitaji kujitetea kwa kuelekeza mfumo wetu mbovu wa haki kwa Mungu. Tunaweza kukomesha uovu huu wa kutunga sheria katika muktadha wa haki inayodai kifo.

Bila Yesu kuchukua asili yetu na kuua uadui kwa kuuzuia usiakisiwe kwetu katika kioo cha tabia yake isiyo na doa, hatungeweza kamwe kumkaribia Mungu.
Somo la asili ya Kristo kwa hiyo ni muhimu kwa mchakato wa upatanisho. Ninatoa shukrani kwa Baba kwamba aliruhusu aonekane kama Hakimu anayehukumu ili niweze kumkaribia. Aliruhusu kuonekana kama mimi, lakini tunapokuja kwenye nuru ya tabia yake, anaweza kutukemea kwa upole kwa ufahamu wetu mbaya na kutuweka huru.

Pasipo Pazia la Mwili wa Kristo uadui wetu unakuzwa katika tabia ya Mungu

> *Wewe huketi na kumnena ndugu yako; unamsingizia mwana wa mama yako mwenyewe. Mambo haya umeyafanya, nami nikanyamaza;* ***ulidhani ya kuwa mimi ni kama wewe;*** *lakini nitakukemea, na kuyapanga mbele ya macho yako. Zaburi 50:20-21*




Haki yetu ya uwongo inatufanya tuseme kinyume na kila mmoja kwa sababu tunafikiri Mungu ni kama sisi. Lakini kwa shukrani anatuvuta kwake na kuweka utaratibu mbele yetu ukweli wa jambo hilo, yaani, ikiwa tutamwacha atuvute kupitia mwili wa Mwana wake.

Kristo alichukua uadui wetu wa chuki ndani Yake ili tuweze kumwangalia bila kumkimbia mara moja. Kubeba uadui huu ni ukweli wa ndani zaidi wa Msalaba wa Kristo. Anabeba juu Yake asili yetu ambayo ndiyo maana halisi ya aya hizi katika Isaya:

> *Hakika ameyachukua masikitiko yetu na amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa. Isaya 53:4*

> *Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale. Isaya 63:9*

> *Kisha akawaambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Luka 9:23*




*Pazia la Mwili wa Kristo hufyonza uadui wetu na kuruhusu upatanisho kwa Mungu*

Ni huzuni na masikitiko kuwahukumu watu wanaotuzunguka. Ni jambo baya sana kubeba chuki mioyoni mwetu. Yesu hana budi kubeba chuki hii yote mabegani mwake ili tu tusimkimbie atakapokuja kwetu.

Kukamilika kwa mchakato wa upatanisho ni kwa mioyo yetu kuwekwa huru kutokana na hitaji la hukumu, adhabu, na kifo. Tutakubali rehema ya Mungu kwa hiari na kuwa na furaha kueneza hili kwa wote wanaotuzunguka. Hapo hatutakuwa tena na ufahamu wa dhambi (Waebrania 10:2) kwa sababu uadui umeondolewa kabisa kutoka kwetu; kwa hiyo hatutaweka tena jambo hili kwa Baba yetu wa thamani aliye mbinguni na tutakoma kuamini kuwa Yeye ndiye anayeua wale wanaomkosea. Tutakuwa huru kutokana na mateso yanayotokana na woga wa kuadhibiwa na Baba yetu. Tutaingia katika pumziko kamili katika mikono ya Baba yetu.

Haya yote yanatimizwa kupitia mwili wa Kristo aliyebomoa ukuta wa kati wa utengano kati yetu na Mungu kupitia pazia la mwili wake. Jina la Bwana Yesu Kristo litukuzwe.

Kristo alifunua ukweli wa tabia ya Baba alipokuwa hapa duniani. Kristo aliuchukua uadui wa mwanadamu hadi kaburini pamoja Naye na akatoka bila kuwa na huo uadui. Ikiwa ukweli wa tabia ya Mungu

ungeweza kwenda katika ulimwengu wote wakati huo, mwisho ungeweza kutokea ndani ya kizazi kimoja.

Mungu alionyesha hili kwa kupasua pazia la hekalu akionyesha kwamba ukweli ulikuwa umefunuliwa ambao ungeruhusu kuingia katika Patakatifu pa Patakatifu.

> *Basi, pazia la Hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka, miamba ikapasuka. Mathayo 27:51*

Cha kusikitisha ni kwamba, ingechukua miaka 2000 zaidi kabla ya uadui ambao Kristo aliupeleka kaburini kuuawa katika watakatifu wa mwisho wa historia ya dunia—wale 144,000.

Baba yetu hakushtushwa na ukweli huu. Danieli aliambiwa miaka 600 kabla ya Kristo ujio wa nguvu ya pembe ndogo ambayo ingepindua injili kupitia mafundisho yake ya kuchukiza.

Lakini kabla ya kwenda kwa Danieli, tunahitaji kuzungumzia mambo mawili. Kwanza, jinsi Mungu ambavyo hutuleta kwenye wokovu kupitia maagano mawili. Pili, jinsi hili linavyotumika kwenye mfumo wa dhabihu na hasa kisa cha Ibrahimu kumtoa mwanawe Isaka.

SURA YA 13

# MUKTADHA WA KISA CHA IBRAHIMU NA ISAKA

Kisa cha Ibrahimu na Isaka ni kisa muhimu na ufunguo muhimu katika kuelewa upatanisho. Martin Luther alimsifu Abraham kwa “imani pofu” katika kukataa kwake kuhoji kama ilikuwa sawa kumuua Isaka. Immanuel Kant anapinga hili, akibisha kwamba amri hiyo chafu haingetoka kwa Mungu. Kabla ya kufikia kiini cha kisa hiki, tunahitaji kuweka hatua.

Kuanzishwa kwa mfumo wa dhabihu kwa wanadamu kulitupatia fursa ya kuona uadui uliokuwepo ndani yetu. Ilikuwa ni kioo cha kukuza chuki ndani ya Mababa wa zamani ili kuwaongoza kwenye neema kwa njia ya imani. Habili alitambua maana ya dhabihu, akakiri uadui wake na kupata wokovu.

*Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini. Kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki, Mungu akazishuhudia sadaka*

*zake; na kwa hilo, ijapokuwa amekufa, angali akinena. Waebrania 11:4*

Kaini hakujua maana ya dhabihu, lakini alikataa kukubali kwamba mwana-kondoo aliyechinjwa alikuwa ishara ya kile kilichokuwa moyoni mwake dhidi ya Mwana wa Mungu. Kwa hiyo, alichagua tu kuleta dhabihu inayoakisi kazi ya mikono yake mwenyewe.

*Ikawa hatimaye Kaini akamtolea BWANA sadaka ya mazao ya nchi. Habili naye akaleta wazaliwa wa kwanza wa kundi lake na mafuta yao….Mwanzo 4:3-4*

Inastahili kuzingatiwa kuwa mchakato wa maneno ya wakati kwa kweli unamaanisha *mwisho wa siku au mwisho wa mwaka*. Hii imeonyeshwa katika Tafsiri ya Young's Living:

*Ikawa **mwisho wa siku**, Kaini akamletea Bwana katika matunda ya nchi zawadi. Mwanzo 4:3 (YLT)*

Baba yetu wa mbinguni hakutamani wingi wa umwagaji wa damu, ilikuwa mara moja tu kwa mwaka ambapo dhabihu ililetwa. Bila kioo hiki kichungu cha dhabihu, uadui ndani ya Adamu na wanawe ungebakia kufichwa kabisa.

Shetani aliwavuvia wazao wa Adamu kufasiri dhabihu kupitia mtazamo wa haki yake ya uwongo. Kupitia sanaa za uelekezaji wa kisaikolojia, dhabihu zilikuja kueleweka kama kitu ambacho Mungu alikidai ili kutosheleza ghadhabu yake dhidi ya dhambi zetu.

Kwa kawaida hufuatia kwamba ikiwa Mungu anadai dhabihu ili kutulizwa, basi kadiri sadaka inayotolewa inavyokuwa ya gharama ya juu zaidi, ndivyo utoshelevu wa ghadhabu ya Mungu unavyoongezeka. Nabii Mika anazungumza katika mchakato huu wa mawazo kwa njia hii:

*Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kusujudu mbele za Mungu aliye juu? Je! nije mbele zake na sadaka za kuteketezwa, pamoja na ndama wa mwaka wa kwanza? Bwana atapendezwa na maelfu ya kondoo waume, na mito elfu kumi ya mafuta? **Je! nimtoe mzaliwa wangu***

*__wa kwanza kwa kosa langu__, mzao wa tumbo langu kwa dhambi ya roho yangu?.Mika 6:6–7*

Ilikuja kuwa jambo la kawaida miongoni mwa mataifa ya wapagani kutoa watoto wao kwa miungu yao ili kuiridhisha. Musa aliagizwa kuzuia vitendo hivi vya kutisha kama ifuatavyo:

*Wala usiruhusu mzao wako awaye yote apite katikati ya moto kwa Moleki, wala usilinajisi jina la Mungu wako; Mambo ya Walawi 18:21*

Hii ilikuwa ni amri muhimu sana kwa sababu nchi ambayo Waisraeli walikuwa wakienda ilikuwa ikitoa dhabihu za watoto kwa karne nyingi:

*Na kumwaga damu isiyo na hatia, damu ya wana wao na binti zao, waliowachinjia kwa sanamu za Kanaani; na nchi ikatiwa unajisi kwa damu. Zaburi 106:38*

Katika wakati wa Ibrahimu desturi ya kutoa watoto dhabihu ilikuwa imeenea sana. Akiwa ametoka katika eneo la Babeli, na hasa alipoingia katika nchi ya Kanaani, Abrahamu alikuwa anafahamu desturi hii.

Abrahamu alimpenda Mungu na alitii kwa uaminifu amri ya kutoka Babeli na kuacha starehe zote za ushirika wa familia. Abrahamu na Sara walikuwa na tatizo, hawakuweza kupata mrithi. Hii ilikuwa ni fursa ya mashaka kuingia katika akili ya Ibrahimu, ambayo Shetani aliitumia kwa sababu alichukia imani ya Ibrahimu.

Alipokuwa akiingia katika nchi ya Kanaani, Abrahamu aliingia katika mapatano na baadhi ya makabila ya Waamori ili kupata usalama dhidi ya vitisho ambavyo vingeweza kutokea. Wakati Lutu mpwa wa Abrahamu alipochukuliwa mateka katika vita na Kedorlaomand, Abrahamu alijiunga na washirika wake Waamori ili kuchukua jeshi hilo lenye kutisha.

Ibrahimu na washirika wake walipata ushindi mkubwa. Akiwa na ushindi mkubwa, Ibrahimu hakupata nyara. Alipokea baraka za Melkizedeki kwa sababu alihitaji uhakikisho wa upendo wa Mungu.

Pambano na Kedorlaoma lilifunua ndani ya Ibrahimu uadui uliokuwa umefichwa hapo awali. Hapo awali alikuwa mtu wa amani, lakini tukio hili lilifunua roho ndani yake ambayo haikuonyeshwa hapo awali.

> *Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji; nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele unaokaa ndani yake. 1Yohana 3:15*

Wakati mpwa wa Ibrahimu alipochukuliwa, roho ya vita iliamshwa katika nafsi yake. "Mwanadamu amezaliwa kwa taabu, kama vile cheche zinavyoruka juu." Ayubu 5:7 Aliporudi nyumbani kutoka vitani, bila shaka Abrahamu alisumbuliwa na mawazo yasiyofaa. Alipokumbuka nyuso za watu waliokufa kwa panga na mikuki, aliogopa adhabu ambayo ingempata. Kila mtu anayeua, kama Kaini, anahofia kutwaliwa maisha yake.

> *"Kwa maana wote waushikao upanga wataangamia kwa upanga." Mathayo 26:52 (KJV)*

Yesu alisema hayo kwa Petro, akieleza kwamba vurugu husababisha kumfukuza Roho wa Mungu anayependa amani, na akimwacha mwanadamu amechanganyikiwa na kuogopa madhara ya matendo yake. Hivi ndivyo Ibrahimu alivyohisi, na Mungu anatafuta kumhakikishia Abrahamu upendo na ulinzi Wake:

> *Baada ya mambo hayo neno la BWANA likamjia Abramu katika maono, kusema, Usiogope, Abramu. Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana." Mwanzo 15:1*

"Baada ya mambo hayo" ikimaanisha baada ya pambano na Kedorlaoma, Mungu anamwambia Abrahamu asiogope. "Mimi ni ngao yako," kumaanisha "nitakulinda," na kuwa thawabu yako kubwa sana. Ni ahadi iliyoje.

Ibrahimu alikuwa akijitahidi kuamini hili kwa sababu kulikuwa na huduma ya kifo ikitokea katika maisha ya Ibrahimu kwa kukosa uwezo wa kupata watoto. Anapokumbuka hisia za uadui ndani ya nafsi yake alipokuwa akipenyeza mkuki wake kwenye viuno vya wale

waliomchukua mpwa wake na kuwatazama machoni walipoanguka chini, aliogopa kwamba angepoteza nguvu zake katika ahadi za Mungu.

Kuchelewa kwa Ibrahimu kupata mtoto kulileta hofu hizi wazi. Mungu alipomkumbusha kuwa Yeye ndiye thawabu kuu ya Ibrahimu, mashaka ndani yake yalijitokeza:

> *Abramu akasema, Tazama, hukunipa mzao; Hakika aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu! Mwanzo 15:3*

Mungu alikuwa amemuahidi Abrahamu, uzao na nchi hapo awali. (Mwanzo 13:14-16). Walipaswa kuwa wengi kuliko ambavyo yeye angeweza kuhesabu. Lakini kufikia wakati wa Mwanzo 15, Ibrahimu anakuwa na mashaka kwamba Mungu anaweza kutimiza ahadi yake kwa sababu ya kushindwa kwake hapo awali. Anapendekeza kwa Mungu suluhisho la mtoto wa kuasili.

Mungu anakataa suluhisho hili la jani la mtini na kusema tena ahadi yake kwa Ibrahimu ya kumpa watoto kutoka kwenye mwili wake mwenyewe. Wakati wa kupendeza unatokea pale Ibrahimu anaposhinda mashaka yake na kwa imani anashikilia ahadi tena.

> *Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki. Mwanzo 15:5-6*

Lakini Mungu anapomuahidi Abrahamu nchi yote anakuwa na mashaka zaidi.

> *Kisha akamwambia, Mimi ndimi BWANA, niliyekutoa Uru wa Wakaldayo, ili nikupe nchi hii uirithi. Akasema, Bwana MUNGU, nitajuaje ya kuwa nitairithi? Mwanzo 15:7-8*

Ibrahimu, akiwa ametoka katika hali ya kutisha ya vita, alikabiliwa na wazo kwamba hilo lilimaanisha vita zaidi kwa upande wake. Kama vile hapo awali Ibrahimu alivyokuwa amepanga mpango wa kuwa na mrithi nje ya ahadi za Mungu, sasa alifikiria kupigana na majirani

zake wote na makabila yote katika nchi hizi ili kuwachukua. Hii itakuwa kazi kubwa katika mwili. Kwa wakati huu imani ya Ibrahimu inajikwaa na ana shaka juu ya jinsi hili linavyoweza kutokea.

Kwa nini Ibrahimu anatilia shaka? Uadui uliobaki ndani yake unamzuia kuikumbatia kikamilifu ahadi ya Mungu. Ili kumwonyesha Ibrahimu tatizo, Mungu anazungumza maneno ambayo yanakuwa kama kioo katika nafsi ya Ibrahimu.

> *Kwa hiyo akamwambia, Niletee ndama wa miaka mitatu, na mbuzi mke wa miaka mitatu, na kondoo mume wa miaka mitatu, na hua, na mwana njiwa. Mwanzo 15:9*

Mungu hamwambii Abrahamu nini cha kufanya na wanyama hao, lakini wanajulikana kwa Abrahamu, kwa kuwa walikuwa wanyama waliozoea kutumiwa kufanya agano kati ya wanadamu. Kwa Ibrahimu, kuwapasua wanyama katikati ilikuwa ahadi yake kwa Mungu ya kuwa mtiifu katika mambo yote. Kwa Mungu, kuchinjwa kwa wanyama hao kuliwakilisha chuki ya mwanadamu ambaye anamchinja Mwanawe. Mungu anajinyenyekeza kuingia katika agano hili na Ibrahimu kwa njia sawa kabisa na kwamba alikuwa tayari kuingia katika agano na Israeli ambapo waliahidi, kama Ibrahimu, kuwa mtii katika kila kitu. Hii ndiyo huduma ya kifo; ni uzoefu wa Agano la Kale uliokusudiwa kusababisha dhambi kuwa nyingi ili iweze kuungamwa na kusamehewa bure.

Tunajua Ibrahimu alikuwa katika hali ya uelewa wa Agano la Kale katika shughuli hii, kwa sababu katika sura inayofuata Ishmaeli anazaliwa kupitia mpango wa Sara kupata mtoto kupitia mjakazi wake, Hajiri.

Paulo katika kutoa maoni yake juu ya kisa hiki anatoa nuru muhimu.

> *Kwa maana imeandikwa ya kuwa, Ibrahimu alikuwa na wana wawili mmoja kwa mjakazi, na mmoja kwa mwungwana. Lakini yule wa mjakazi alizaliwa kwa mwili, yule wa mwungwana kwa ahadi. Mambo haya husemwa kwa mfano; kwa maana hawa ndio kama maagano mawili, moja kutoka mlima Sinai, lizaalo kwa utumwa,*

*ambalo ni Hajiri. Maana Hajiri ni kama mlima Sinai ulioko Arabuni, umelingana na Yerusalemu wa sasa; kwa kuwa anatumika pamoja na watoto. Bali Yerusalemu wa juu ni mwungwana, naye ndiye mama yetu sisi. Wagalatia 4:22-26*

Kutoweza kwa Sara kuzaa mtoto, ilikuwa ishara ya uadui ambao ulikuwa bado ndani ya moyo wa Ibrahimu. Mungu angeweza kumwacha Ibrahimu azae mwana mara moja lakini kwa sababu aliona kwa Ibrahimu mwana wa thamani ambaye alikuwa tayari kumsikiliza, Mungu alimjaribu na kudhihirishia uadui uliofichwa, uliorithiwa kutoka kwa Adamu na kukuzwa na Ibrahimu. Alifanya hivi kwa sababu alitaka Ibrahimu apate amani ya kweli na pumziko, ambayo ingetokea tu ikiwa uadui huu ungetambuliwa na kuachiliwa na Ibrahimu.

Sara, katika hali yake ya kukata tamaa, na hisia ya aibu kwa kutozaa mtoto, anamtia moyo Abrahamu azae mtoto kupitia Hajiri, mjakazi wake. Katika kusikiliza sauti ya mke wake, Ibrahimu alifunua ukosefu wake wa imani katika ahadi na akafunua nia yake ya kutekeleza ahadi mwenyewe kwa matendo yake mwenyewe.

Miaka 13 baada ya kuzaliwa kwa Ishmaeli Mungu anamtokea Ibrahimu. Ilikuwa wakati huu ambapo Mungu alibadilisha jina la Ibrahimu kutoka kwa Abramu. Abramu maana yake ni *baba wa juu* huku Ibrahimu maana yake ni *baba wa umati wa watu.*

Mungu anaweka wazi kwa Ibrahimu ahadi kwa mara nyingine tena, akiongeza maelezo zaidi na zaidi. Hata kama Mungu anazungumza Ibrahimu anapata shida kuamini. Abrahamu angewezaje kuwa baba wa umati mkubwa akiwa na umri wa miaka 99? Je, angemilikije nchi yote? Ilionekana kuwa ngumu kuamini.

Kwa mara nyingine tena, Mungu anadhihirisha uadui ndani ya Ibrahimu kupitia amri ya tohara. Tohara ilianzia Misri, kwa mujibu wa mwanahistoria wa Kigiriki Herodotus.[26] Ibrahimu alipokwenda

[26] https://en.wikipedia.org/wiki/History_of_circumcision

Misri, Hajiri akawa mtumishi wa Sara. Huenda ikawa ni kupitia kwa Hajiri kwamba tohara ilianzishwa kwa familia yao, kutokana na urithi wake wa Misri. Tohara nchini Misri ilifanywa kwa vijana wa kiume kati ya ujana na utu uzima. Ishmaeli alikuwa na umri wa miaka 13 wakati Mungu alipomtokea Ibrahimu na huenda Hagari alikuwa akiibua suala hili kuhusu mwanawe Ishmaeli.

Ingawa hatuwezi kuwa na uhakika, jambo moja ni hakika; ilikuwa ni desturi ya kipagani. Haikutoka kwa watu wa Mungu. Ili Mungu awaelekeze watu wake kuhusu desturi ya kipagani, ni lazima iwe sehemu ya kioo kinachofunua dhambi iliyo ndani ya mwanadamu.

*Ili Mungu awaelekeze watu wake kuhusu desturi ya kipagani, ni lazima iwe sehemu ya kioo kinachofunua dhambi iliyo ndani*

Kutokana na ukweli kwamba Ibrahimu hakuweza kumwamini Mungu, ishara ya mateso au maumivu ilidhihirishwa. Ishara hii kutoka kwenye taratibu za huko Misri, kama onyesho la utu uzima, sasa ilitumiwa na Mungu ili kukuza kutokuamini kwa Ibrahimu ili kumwongoza kwenye toba. Paulo anaweka wazi kwamba tohara haikuwa muhimu kwa haki kwa imani.

> *Basi je! Uheri huo ni kwa hao waliotahiriwa, au kwa hao pia wasiotahiriwa? Kwa kuwa twanena ya kwamba kwake Ibrahimu imani yake ilihesabiwa kuwa ni haki. Alihesabiwaje basi? Alipokwisha kutahiriwa, au kabla hajatahiriwa? Si baada ya kutahiriwa, bali kabla ya kutahiriwa. Warumi 4:9-10*

Kama vile mfumo wa dhabihu ulivyoagizwa kwa Adamu na wanawe kwa sababu ya uadui uliofichika ndani yao, ndivyo tohara ilitolewa kwa Ibrahimu na uzao wake ili kuikuza dhambi yao ili kuwaongoza kwenye toba. Bila shaka, katika mfumo wa Agano la Kale, ilikuwa ni alama ya heshima na tofauti kwa Ibrahimu. Ikiwa tohara ingekuwa kanuni ya milele ingebaki milele lakini kama mfumo wa dhabihu,

matumizi yake hayakuwa na thamani tena baada ya Kristo kufunua tabia ya Baba na kuupeleka uadui wa Adamu kaburini.

*Kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu, bali kuzishika amri za Mungu ndilo jambo la maana.1Wakorintho 7:19*

Ushahidi wa kwamba Ibrahimu bado hakuwa na imani wakato Mungu akimwahidi kila kitu unapatikana zaidi katika kisa hiki.

*Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara. Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake. Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akacheka, akasema moyoni, Je! Mtu wa umri wa miaka mia, kwake atazaliwa mtoto? Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa?Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako. Mwanzo 17:15-18*

Ibrahimu alimcheka Mungu moyoni mwake. Huku ni kutoamini. Hili lilimsababishia Mungu maumivu. Je, unapenda kuchekwa unapoahidi kitu cha maana kwa wale unaowapenda? Na zaidi ya hili kuwafanya wakupendekezee kitu kingine kama suluhisho?

Mungu kwa neema anakubali kutahiriwa kama muhuri wa imani ambayo Abrahamu alikuwa ameeleza hapo awali kwa kuamini kwamba Mungu angempa mrithi.

*Naye aliipokea dalili hii ya kutahiriwa, muhuri ya ile haki ya imani aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa; apate kuwa baba yao wote waaminio, ijapokuwa hawakutahiriwa, ili na wao pia wahesabiwe haki; Warumi 4:11*

Wakati ulipofika wa Isaka kuzaliwa, Mungu alipeleka ujumbe kwa Abrahamu. Sara akisikiliza katika hema anafuata kutoamini kwa mume wake na anacheka wazo la kuzaa watoto baada ya kukoma hedhi. Kwa mwonekano wa kidunia hili haliwezekani.

*Wakamwambia, Yu wapi Sara mkeo? Akasema, Yumo hemani. Akamwambia, Hakika nitakurudia wakati huu huu mwakani, na*

*tazama, Sara mkeo atapata mwana wa kiume. Sara akasikia mlangoni pa hema iliyokuwapo nyuma yake. Basi Ibrahimu na Sara walikuwa wazee, na umri wao mkubwa, na Sara alikuwa amekoma katika desturi ya wanawake. Kwa hiyo Sara akacheka moyoni mwake, akisema, Niwapo mkongwe, nitapata furaha, na bwana wangu mzee? BWANA akamwambia Ibrahimu, Mbona Sara amecheka akisema, Mimi kweli nitazaa mwana, nami ni mzee? Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda BWANA? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume. Akakana Sara, akisema, Sikucheka, maana aliogopa. Naye akasema, Sivyo, umecheka. Mwanzo 18:9-15*

Licha ya ugumu wao ya kuamini, Mungu kwa fadhili aliwapa Abrahamu na Sara mtoto. Ibrahimu alikuwa ameonyesha imani katika Mwanzo 15 kuhusu ahadi na licha ya kujikwaa kwake, ambapo dhambi ilizidi, neema ya Mungu bado ilikuwa nyingi zaidi.

Shangwe isiyoelezeka katika nyumba ya Abrahamu haikuchukua muda mrefu sana kwa sababu Hajiri hakuthamini mtoto wake kuwekwa kuachwa nyuma kwa sababu ya Isaka. Ushindani ulioonyeshwa hapo awali kabla ya kuzaliwa kwa Isaka ulijitokeza tena kupitia mateso ya Isaka kutoka kwa Ishmaeli. Sara alipeleka madai yake kwa Ibrahimu:

*Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. Mwanzo 21:9-10*

Mungu anamwambia Ibrahimu amsikilize mke wake. Hata katika maneno haya, dhambi ya Ibrahimu inakuzwa, kwa sababu Ibrahimu alikuwa amemsikiliza mke wake hapo awali katika mwanzo wa kuunda tatizo hili. Kwa hiyo sasa katika kumsikiliza mke wake tena, uchungu wa matendo yake ulikuzwa na utambuzi wake wa kushindwa kwake wakati uliopita unakuwa wazi zaidi. Ni huzuni iliyoje kwa Ibrahimu kutengana na mwanawe Ishmaeli. Ingekuwa chungu sana kwake; uchungu zaidi kuliko kukata nyama yake katika

tohara. Tunaona katika Ibrahimu kazi ya Agano la Kale. Ni huduma inayokuzwa ya mauti. Imekusudiwa kuleta neema tele kwake.

Kupitia uzoefu huu wa kunyenyekea, utegemezi wa Ibrahimu juu yake mwenyewe ulipungua na akawa na nguvu katika imani. Mungu alitambua kwamba ndani ya Ibrahimu ule usaliti wa Adamu ungedhihirika ili yeye, pamoja na wanadamu wengine wote, waweze kuona uadui wa mwanadamu dhidi ya Mungu na Mwanawe; dhambi kamili ilizidi sana ili neema ya ajabu ya Mungu inaweze kuwa nyingi zaidi.

SURA YA 14

# IMANI YA IBRAHIMU

Katika kilele cha Mlima Moria, wanadamu wote wameketi katika hukumu. Tumeitwa kuamua maana ya agizo la Mungu kwa Ibrahimu la kumtoa mwanawe, mwana ambaye Ibrahimu alikuwa amemngoja kwa maisha yake yote; mwana ambaye Mungu alikuwa amemwahidi na ambaye matumaini yake yote yalikuwa ndani yake. Kama vile Kierkegaard alivyosema: "Kama vile imani ya Abrahamu inavyojaribiwa na Mungu katika Kitabu cha Mwanzo, vivyo hivyo imani ya msomaji mwenyewe hujaribiwa kwa kutafakari mwenyewe kisa cha Biblia."

Martin Luther aliwahi kusoma habari za Ibrahimu akimtoa Isaka kwenye madhabahu ya sadaka. Mkewe, Katie, kwa huruma zote za mama alisema, "Siamini. Mungu hangemtendea hivyo mwanawe!" Luther akajibu, "Lakini, Katie," "alifanya hivyo."

Rembrandt anadakia na kukikabili kisa namna kutatiza. Mkono wa Abraham unasukumwa juu ya uso wa Isaka katika kile kinachoonekana kuwa uungaji mkono wa kimyakimya kwa kile ambacho Alice Miller adokeza kuwa ni unyanyasaji wa watoto.[27]

---

[27] Alice Miller, The Untouched Key: Tracing Childhood Trauma in Creativity and Destructiveness, (New York: Doubleday, 1990)

Ili kupanda Mlima Moria bila kushikwa kwenye kichaka sawa na kondoo dume, tukumbuke mambo tuliyoyazingatia katika sura zilizopita zinazopelekea kwenye hatua hii.

Katika sura ya 3 tulichunguza mitazamo ya wanadamu kuhusu haki ya Mungu. Ukristo unamwonyesha Mungu kuwa mkali asiyebadilika katika shughuli zake. Anaeleweka kama kiumbe asiyechoka kuwawinda wavunja sheria na kuwaadhibu ama wao au mbadala.

Katika sura ya 4 tulizingatia usaliti uliofichika wa Adamu; hali mbaya ya kutoelewa maneno ya Mungu kwamba siku utakapokula matunda ya Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya, utakufa. Akififikiri kwamba Mungu alidai kifo cha mke wake, alimwita Mungu mbele ya mahakama yake ya ndani na kumhukumu Mungu kwa kile alichoamini kuwa ni nia ya Mungu. Tunakazia jambo muhimu la kwamba Adamu alielewa vibaya maana ya maneno ya Mungu na kuyaweka katika muktadha wa hukumu ya kifo inayotolewa na haki isiyo ya kweli. Katika kujilinda, Adamu anaelekeza mawazo yake ya uongo kwa Mungu na anamwogopa sana. Jaribio lolote la Mungu kumwendea linachukuliwa kama ishara ya kifo. Adamu na uzao wake wana chuki ya kina dhidi ya Mungu, lakini imefichwa ndani kabisa ya ufahamu wake.

Katika sura ya 5 tunaona Jua la haki likiangaza nuru ndani ya akili iliyotiwa giza ya wanadamu katika ufunuo kamili wa tabia ya Mungu kwa mwanadamu katika huduma ya kidunia ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kamwe Yesu hakuonyesha haki ambayo ilimtaka akatishe maisha ya mtu mwingine kwa lazima. Kupitia mtazamo huu tunaalikwa kutembea na Yesu katika njia ya kwenda Emau na kumwacha atufunulie katika vitabu vya Musa na Manabii mambo yote yanayomhusu yeye mwenyewe. (Luka 24:44).

Katika sura ya 6 tuligundua haki bandia ya Shetani na jinsi alivyotunga sheria ya Mungu kwa upotovu kupitia mtazamo wake wa haki ya uwongo. Kisa cha Absalomu kinarudisha nyuma pazia juu ya shauku ya kishetani ya kutwaa kiti cha enzi cha Mungu.

Katika sura ya 7 tunaona jinsi ambavyo Mungu hukutana na mwanadamu katika mitazamo yake yenye giza ya upatanisho. Nyoka aliyeinuliwa juu katika chuma cha shaba iliyotengenezwa na mwanadamu, iliyowekewa alama za upatanisho wa kipagani huku akiwa na kidokezo cha serafi wa moto aliyeanguka kutoka mbinguni, inatufunulia kwamba Mungu alikuwa akikutana na mwanadamu katika mahali penye giza pa mawazo yake yaliyopotoka. Ukiwa umetiwa doa na kanuni mbovu za uadilifu wa kishetani, ubinadamu hauwezi ila kuwaza uungu kama mtu anayedai kifo kwa ajili ya uvunjaji sheria.

Katika sura ya 8 tulifunua ukweli kwamba ni kwa kifo cha Kristo tu juu ya msalaba wa kipagani wa Kirumi ndipo mwanadamu angeweza kuanza kuamini kwamba Mungu angeweza kutupa rehema. Ukweli huu ulionyeshwa katika amri ya Musa ya kuupiga mwamba mwanzoni jangwani, wakati wa mwisho wa safari hiyo, aliagizwa kuzungumza na mwamba ili kupokea maji ya uzima. Hili lilikuwa ni kuthibitisha kwamba bila kumwaga damu kusingeweza kuwa na upatanisho; kwa maana wanadamu, waliojawa na haki ya uwongo, hawakuweza kukubali kwamba Mungu angeweza kusamehe bila hukumu ya kifo kutumika.

Katika sura ya 9 tunaanza kufahamu kwa mshangao wakala wa kuokoa wa Mungu katika Kristo akichukua mwili wa kibinadamu kama wetu ili kuondoa uadui wetu dhidi ya Mungu na hivyo kumruhusu Yeye kuja karibu na maskani kati yetu. Hii inathibitisha ukweli kwamba Mungu hakutaka dhabihu bali mwili ulitayarishwa kwa ajili ya Kristo kuja karibu nasi na kutuongoza kuwa na imani katika Kristo kama mpatanishi. Pia tuliangalia mfumo wa Patakatifu kama njia kutoka kwenye shaba hadi dhahabu na kutoka kwenye mawazo ya uwongo ya kibinadamu ya upatanisho hadi upatanisho wa kweli wa Mungu.

Katika sura ya 10 tulijumuisha hatua muhimu ya mchakato wa maagano mawili ya kupatanishwa na Mungu. Nafsi ya mwanadamu haitambui kiwango halisi cha upotovu wake. Kupitia huduma ya

Agano la Kale, kina cha dhambi zetu kinakuzwa kupitia matokeo ya matendo yetu wenyewe. Hili linafanywa ili dhambi yetu iweze kueleweka kikamilifu kwetu. Katika wakati wa utambuzi, neema ya Agano Jipya inatolewa kwetu ili tuweze kuachiliwa kutoka kwenye uadui wetu na kupatanishwa na Mungu. Kama tulivyogundua katika kisa cha mwanamke Mkanaani, ufahamu wake wa kile ambacho Kristo alikuwa akisema, ingawa si sahihi, ulikuwa ni kichocheo cha kukamilishwa kwa imani yake. Huu ndio muktadha wa kisa cha Mlima Moria.

Ingawa ni vigumu kubeba tabaka hizi zote za mawazo na kuzitumia mara moja kwenye kisa cha Abrahamu na Isaka, nyanja ya mwisho tuliyozungumzia katika sura ya 10 inaweza kutumika kama njia ya kutusaidia, ikisaidiwa na wazo la maisha ya Kristo duniani kuwa jumla ya tabia ya Mungu. Ikiwa tunaweza kuchukua angalau tabaka hizi mbili za mawazo kwenye kisa, basi tuna fursa ya kuleta tabaka zingine baadaye ili kuikamilisha picha. Ni taswira ya neema kuu kwa upande wa Mungu badala ya utisho wa kutisha wa Mungu anayedai Ibrahimu amuue mwanawe wa thamani.

Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa.

> *Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Mwanzo 22:1-2*

Tunakumbuka maneno ya Yesu kwa mwanamke Mkanaani, “Si vema kuchukua mkate wa watoto na kuwatupia mbwa.” (Mathayo 15:26). Jibu la mwanamke huyo linaonyesha kwamba aliamini kwamba Yesu alimwita mbwa. Hakuelewa kile ambacho Yeye alikisema, na hivyo kufanya jaribu la imani yake kuwa kubwa zaidi kuliko lilivyotakiwa kuwa. Kauli ya Yesu ilikuwa kioo cha mawazo yake kuhusu yeye mwenyewe. Yesu hakufikiri kwamba mwanamke huyu wa thamani alikuwa mbwa, bali alipanga maneno yake kwa njia ya kuwafundisha mwanamke huyu na wanafunzi wake masomo muhimu.

Jambo hilohilo lilitukia Abrahamu alipomwomba Mungu uthibitisho wa kwamba angemiliki nchi ambayo Mungu aliahidi. Mungu alimwambia Abrahamu alete ndama wa miaka mitatu, mbuzi jike wa miaka mitatu, mwana-kondoo wa miaka mitatu na hua. Maneno haya yalikuwa na maana kwa Ibrahimu katika muktadha wake mwenyewe.

Mungu alilijua hilo vizuri. Mungu hakumwambia la kufanya na hao wanyama, lakini Ibrahimu alikwenda mbele katika mfumo wa uliozoeleka ambao alielewa maneno hayo. Mungu alimruhusu Abrahamu afanye kile alichofikiri kwamba Mungu anakitaka, ili kumfundisha mambo muhimu.

Mungu alipomwambia Abrahamu amchukue mwana wake wa pekee, maana ya maneno hayo ilidokeza kwamba Abrahamu alitenda kulingana na uelewaji wake mwenyewe wa maneno hayo. Mungu alijua angelielewa kwa namna hii, na akatumia kutokuelewa huku kwa upande wa Ibrahimu kuleta nje mawazo ya ndani ya Ibrahimu huku akifanya jaribu la imani kuwa kubwa zaidi.

Fikiria kishazi "mtoe kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa." Neno mtoe lina maana zifuatazo katika Kamusi ya Brown, Driver na Briggs:

> *Kuleta, sababisha kupanda au kupanda, kusababisha kwenda juu, kuleta, kuleta dhidi, kuchukua, kuleta, kuteka, kufundisha, kusababisha kupanda, kuamsha, kuchochea (kiakili), kutoa, kuleta (za zawadi), kuinua, kusababisha kupanda, kutoa - aina ya Hiphil ya H5927*

Katika muktadha huu tunaona jinsi tafsiri ya Young's Literal inavyotafsiri neno hili:

> *Akasema, Umchukue, nakuomba, mwanao, mwanao wa pekee uliyempenda, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria,* ***ukampandishe huko*** *kuwa sadaka ya kuteketezwa juu ya mlima mmoja wapo ambao nitakuambia." Mwanzo 22:2 (YLT)*

Walipokuwa wakienda kupanda Mlima Moria, neno kupanda ni chaguo la asili kwa safari hiyo. Neno la sadaka ya kuteketezwa lina

maana mbili. Ya kwanza ni sadaka ya kuteketezwa na ya pili ni kupanda, ngazi au kwenda juu. Strong's Concordance inaitafsiri hivi.
Kishirikishi hai cha kike cha H5927; hatua au (kwa pamoja ngazi, kama kupanda); kwa kawaida dhabihu ya kuteketezwa (kama kupanda moshi): - kupandisha, sadaka ya kuteketezwa (dhabihu), kwenda juu. Tazama pia H5766.
Tazama jinsi neno la sadaka ya kuteketezwa linavyotafsiriwa katika mstari huu:

> *Tena palikuwa na madaraja saba ya* ***kuliendea****, na matao yake yalikuwa mbele yake; nalo lilikuwa na mitende, mmoja upande huu, na mwingine upande huu, juu ya miimo yake." Ezekieli 40:26 (KJV).*

Kwa hiyo, kile ambacho Mungu alizungumza kinaweza kutafsiriwa hivi:

> *Kisha akasema, Mchukue sasa mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukakwee huko na kupanda juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Mwanzo 22:2*

Maelezo haya ni muhimu kuelezea kioo kinachofanya kazi katika maandishi. Mungu alijua jinsi ambavyo Abrahamu angeelewa maneno aliyomwambia. Kwanza, hebu tuchunguze kile Mungu anachokisema kuhusu dhabihu ya watoto:

> *Nao wamemjengea Baali mahali pake palipo juu, ili kuwachoma moto wana wao, wawe sadaka za kuteketezwa kwa Baali; tendo nisiloliamuru mimi, wala kulinena, wala halikuingia moyoni mwangu; Yeremia 19:5*

Mungu anaonyesha kupitia Yeremia kuhusu wakati ambapo Israeli walitoka Misri.

> *Maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru kwa habari za sadaka za kuteketezwa na dhabihu, siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri; lakini naliwaamuru neno hili, nikisema, Sikilizeni sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu;*

*mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru mpate kufanikiwa. Yeremia 7:22-23*

Kama tulivyosema hapo awali, mfumo wa dhabihu ulitolewa kwa mwanadamu kama kioo cha mawazo yake kwa Mungu na Mwanawe. Mungu kamwe hakutaka dhabihu. Mwanadamu anayetafuta kujitetea dhidi ya shtaka zito la kutaka kumuua Mwana wa Mungu, anaweka hili kwa Mungu kama jambo ambalo Mungu analitamani. Ni jambo la kikatili kwa mwanadamu kumfanyia Mungu, lakini mwishowe, linafanya tu majaribio ambayo mwanadamu anapaswa kukabiliana nayo kuwa makubwa zaidi.

Jinsi Ibrahimu alivyomwelewa Mungu hudhihirisha kile kilichokuwa ndani yake. Ibrahimu alilelewa katika mazingira ya dhabihu ya watoto; watu wa nchi ya Kanaani, alimokaa, walifanya machukizo hayo. Dhambi alizokuwa amefanya hapo awali zote zilishuka juu yake, mawazo ya hukumu na kwa hiyo adhabu.

Dhamiri yenye hatia ya Ibrahimu ilijaribiwa kuamini kwamba hakusamehewa na Mungu isipokuwa alimtolea Mungu kitu. Kwa hiyo Mungu aliakisi Agano hili la Kale lenye kasoro, akimfikiria Ibrahimu ili kumtoa kwalo. Mungu alitaka Ibrahimu awe na uhusiano wa upendo na Yeye bila kurudi nyuma katika woga na ukosefu wa usalama kwa sababu ya kutoelewa kwake tabia ya Mungu.

| Mandhari ya Hukumu | **Hukumu** | **Kutakaswa kwa Hekalu** |
| Ufalme wa Kristo | Ujio wa pili | Atavunjika pasipo kazi ya mikono ya mwanadamu |

[41] https://www.chabad.org/library/article_cdo/aid/4399/jewish/Day-of-Judgment.htm

Swali lilipoulizwa katika Danieli 8:13 hadi lini watu wa Mungu watakandamizwa na mifumo ya kutuliza ya Upagani na Upapa, jibu ni kwamba, kama tulivyojadili, siku 2300 za kiunabii ambazo ni miaka 2300 halisi.

Waadventista Wasabato walifikia hitimisho kwamba kipindi cha mwisho cha hukumu kingeanza mwaka wa 1844 wakati Siku ya Upatanisho mwaka huo ilipoadhimishwa.

Wakati huu watu wa Mungu wanaungama dhambi zao na kutubu Mungu anapochunguza vitabu vya kumbukumbu. Wale ambao wameungama dhambi zao na kujinyenyekeza mbele ya Mungu wamehifadhiwa katika Kitabu cha Uzima. Wale ambao hawatatubu na kushikilia dhambi zao wataondolewa kwenye Kitabu cha Uzima. Kristo anawaombea wale wote ambao wamekiri jina lake na kusihi damu yake kwa niaba yao. Kazi ya hukumu inapokamilika, dhambi zote za watu huwekwa juu ya kichwa cha Azazeli anayemwakilisha Shetani. Yeye ndiye aliyesababisha anguko la mwanadamu, akamtenga na Mungu na kuwashawishi watu wote kumtenda Mungu dhambi.

Kwa ufahamu huu, dhambi imeshughulikiwa na wale waliojinyenyekeza mbele za Mungu wanapokea upatanisho. Hakuna kikwazo kati yao na Mungu tena na wako tayari kuingia katika ufalme wa milele wa Kristo.

Sasa kwa kuwa tumeweka utaratibu wa jinsi Siku ya Upatanisho ilivyoeleweka kwa Wayahudi na Waadventista Wasabato, sasa tunakaribia kutumia mambo ambayo tumejifunza katika sehemu ya kwanza ya kitabu hiki kuhusu mchakato wa upatanisho. Lakini kwanza tunahitaji kutofautisha kati ya mtazamo wa kawaida wa Kiprotestanti wa upatanisho na uelewa wa Waadventista katika nuru ya mfumo wa Patakatifu wa Agano la Kale.

SURA YA 18

# ULINGANISHO KATI YA UPATANISHO WA WAPROTESTANTI NA WAADVENTISTA

Katika sura ya 3 tulichunguza jinsi wazo la Kikristo la upatanisho lilivyositawi karibu na wazo la kuridhika kwa haki ya kimungu. Ikiwa haki ya Mungu inadai adhabu, na ghadhabu ya Mungu inatoshelezwa katika adhabu hiyo, basi inasimama ikiwa na kwamba mara tu adhabu inapotolewa, mchakato wa upatanisho unakamilika. Hapa kuna usemi mmoja wa wazo hili:

> *Katika Ukristo, upatanisho unarejelea maelewano yanayohitajika kati ya wanadamu wenye dhambi na Mungu mtakatifu.* ***Upatanisho huu unawezekana kupitia dhabihu ya upatanisho ya Yesu Kristo****, kama inavyoonyeshwa katika Warumi 3:25, Warumi 5:11, na Warumi 5:19. upatanisho ndio ujumbe mkuu wa Biblia*.

*“Kupokea upatanisho ni upatanisho wetu halisi kwa Mungu katika kuhesabiwa haki, unaojengwa juu ya ulidhishaji wa Kristo,” kulingana na Matthew Henry’s Commentary. “Sisi Wakristo, sisi waamini, kwa sasa katika nyakati za injili, au sasa katika maisha haya, tumepokea upatanisho, ambao ulifananishwa na dhabihu chini ya sheria, na ni tegemeo la furaha yetu mbinguni*.”[42]

Wazo la kawaida la Kikristo ni kwamba upatanisho unamaanisha maelewano. Nakala tuliyonukuu hapo juu inakwenda mbali zaidi kuelezea jinsi hili linavyotokea:

*upatanisho ni neno ambalo linapatikana katika baadhi ya tafsiri katika Warumi sura ya tatu, mstari wa 25.* ***Mungu alimtoa Yesu kama dhabihu ya upatanisho.*** *Tafsiri zingine zingetumia neno kipatanisho, na wazo hapo ni la mbadala anayebeba ghadhabu. Sawa?*

*Yesu Kristo msalabani anachukua ghadhabu ya Mungu. Ni mapatano kati ya baba na mwana. Baba anamimina hasira yake juu ya dhambi alizobeba Kristo, na ghadhabu yake inatoshelezwa. Na kwa sababu hiyo, mwenye dhambi mwenye hatia anayemwamini Kristo anapata kuachwa huru. Inahusiana kwa kiasi fulani na kuhesabiwa haki, lakini ni njia ambayo kuhesabiwa haki kunawezekana.*[43]

Tovuti ambayo tumeinukuu inatafuta kuelezea kanuni ya Kikristo ya upatanisho kwa maneno rahisi kwa wale wasiokuwa na uelewa. Wataalamu wa Biblia wameeleza hili kwa lugha yenye maana nyingi zaidi lakini maana yake ni kwamba Mungu anapatanishwa na mwanadamu kwa kifo mbadala cha Kristo. Hili linatosheleza hasira na haki ya Mungu. Mwenye dhambi anaungama dhambi yake na kusema anasikitika, lakini ni kifo cha Kristo kinachoathiri upatanisho kwa sababu ni haki ya Mungu inayoonekana kuwa inahitaji upatanisho. Hawezi kukubali kusema kwetu tu samahani; Haki yake inahitaji kuridhika.

---

[42] https://www.christianity.com/wiki/salvation/what-is-atonement-biblical-meaning-and-definition.html

[43] Ibid

Katika muktadha huu ni dhahiri kwamba mara Yesu anapokufa Msalabani, upatanisho unakamilika. Hakuna kilichobaki isipokuwa kuamini. Maadamu mwenye dhambi anashikamana na Kristo, anakingwa dhidi ya hukumu ya Mungu dhidi ya dhambi.

Wakristo hurejelea mfumo wa dhabihu wa Agano la Kale kama unaoashiria kifo cha Kristo Msalabani, lakini tunatilia mkazo kidogo kwenye mlolongo wa matukio katika mwaka wa kidini wa Kiyahudi kwamba una maana yoyote zaidi ya Msalaba wenyewe.

Waadventista Wasabato walisema kwamba orodha ya sikukuu zinazotolewa katika Mambo ya Walawi 23 kwa hakika hutoa mchakato wa hatua kwa hatua kutoka wakati wa Kristo hadi Ujio wa Pili, unaoashiria mfululizo wa matukio badala ya tukio moja lililounganishwa na upatanisho. Katika kuunganisha Siku ya Upatanisho na utakaso wa Patakatifu katika 1844, kiwango cha kina cha ufahamu wa upatanisho kilianzishwa.

Waadventista, katika kuelekeza kwenye mifano, walisema kwamba upatanisho ulifanywa kupitia huduma ya kuhani baada ya mnyama kutolewa dhabihu, si wakati wa kutoa dhabihu. Joseph Waggoner, kiongozi mwingine wa Waadventista anaeleza hivi:

> *Imeonekana kwamba mwenye dhambi alileta sadaka yake; kwamba ilichinjwa; na kwamba kuhani akaitwaa damu na kufanya upatanisho; na hapa inathibitishwa zaidi kwamba upatanisho ulifanywa katika patakatifu.* ***Hii inathibitisha kwa uwazi kabisa kwamba kuuwawa kwa dhabihu hakukufanya upatanisho, bali kulikuwa ni matayarisho yake; kwa maana upatanisho ulifanywa katika patakatifu, lakini dhabihu haikuchinjwa katika patakatifu.***
>
> *Mambo haya, bila shaka, yalikuwa ya mfano, na yana utimizo wake katika kazi ya Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kwamba yeye*

*ni Kuhani Mkuu, na mpatanishi pekee katika injili; lakini utaratibu na namna ya utumishi wake lazima uamuliwe na Maandiko.*[44]

Mtazamo wa Waadventista wa upatanisho ulidumisha mtazamo ule ule wa haki kama Ukristo wote, lakini ulionyesha mifano katika Agano la Kale ambayo ilionyesha kwamba mwenye dhambi hakuwa na upatanisho kwa ajili ya dhambi zake kwa kuua tu dhabihu, lakini badala yake kuhani alipaswa kupaka damu ya dhabihu kwenye Patakatifu na kwa hiyo ni kwa njia ya maombezi ya kuhani ya damu ya dhabihu ambayo upatanisho ulipatikana. Hili lilitokea katika Patakatifu penyewe na si katika Ua.

Kwa sehemu kubwa ya Ukristo, utulizaji wa haki ya Mungu hutokea Msalabani, wakati kwa Waadventista utulizaji huu unafanyika, kwa mujibu wa mfano wa Agano la Kale, kwa njia ya upatanishi wa Kuhani wetu Mkuu mbinguni baada ya dhabihu kufanywa duniani. Waggoner anaendelea:

*"Wote wanakubali wazo la kutopendezwa kwa Uungu na kupata kuridhishwa na yule asiye na hatia kutolewa dhabihu mahali pa mwenye hatia." Hili lazima liwe wazo sahihi.* ***Haki au kuchukizwa kwa Mwenyezi Mungu kunaridhishwa kwa dhabihu, lakini kwa kweli hutulizwa kwa upatanishi wa Kuhani wetu Mkuu.***[45]

Msisitizo wa upatanisho kwa ajili ya Waadventista ulikuwa kwa Kristo aliye hai kusihi damu yake mbele za Baba katika Patakatifu pa mbinguni. Kifo cha Kristo Msalabani kilikuwa muhimu kwa kazi ya Yesu kusihi damu yake mbele ya Baba, lakini Msalaba wenyewe haukuwa upatanisho uliokamilika. Hakungekuwa na huduma nzuri mbinguni ili kukamilisha upatanisho bila damu ya Kristo, lakini bila maombezi ya Kristo mbinguni kama Kuhani wetu Mkuu dhabihu isingekuwa upatanisho kamili.

---

[44] J.H. Waggoner, The atonement in the Light of Nature and Revelation, (Review and Herald, 1884), page 187
[45] Ibid, page195

Mfumo mzima wa mtazamo wa Waadventista wa upatanisho uliegemezwa juu ya mfumo wa Patakatifu. Sherehe za kila mwaka wa Kiyahudi zinasimulia hadithi ya mpango wa wokovu kutoka kwenye Msalaba hadi Kuja kwa Kristo mwisho wa ulimwengu huu.

> *Somo la patakatifu lilikuwa ni ufunguo uliofungua fumbo la kukatishwa tamaa kwa 1844. Lilifunguka ili kuona mfumo kamili wa ukweli, uliounganishwa na wenye upatano, ukionyesha kwamba mkono wa Mungu ulikuwa umeongoza harakati za wana marejeo na kufunua wajibu wa sasa kama ulivyoleta nuru kwenye nafasi na kazi ya watu wake*.[46]

Wakati Waprotestanti wanawasilisha mfumo wote wa dhabihu wa Agano la Kale unaoelekeza kwenye Msalaba, Waadventista walizama zaidi katika mifano kwa sababu ya mfumo wa kinabii waliougundua katika Danieli na Ufunuo unaounganisha kazi ya hukumu katika Siku ya Upatanisho hadi tarehe 22 Oktoba 1844.[47] Ilionekana kwamba wakati sikukuu ya Pasaka ilipoashiria kifo cha Kristo Msalabani, sikukuu nyingine zote ziliwakilisha matukio mfululizo katika historia ya Kikristo tangu wakati wa Msalaba hadi Ujio wa Pili.

| Sikukuu | Tarehe | Maana halisi |
|---|---|---|
| 1. Pasaka | Siku ya 14 ya Mwezi wa 1 | Msalaba wa Kristo |
| 2. Mikate isiyotiwa chachu | Siku ya 15-22 ya mwezi wa 1 | Kristo akiwa Kaburini |
| 3. Mavuno ya kwanza | Siku baada ya Sabato katika kipindi cha miakate isiyotiwa chachu | Kufufuka kwa Kristo |

[46] E.G. White, The Great Controversy, (Review and Herald, 1911), page 423
[47]Kwa maelezo zaidi juu ya somo hili angalia sura ya 15-19 ya kitabu kitwacho As You Judge kinachopatikana katika fatheroflove.info

| | | |
|---|---|---|
| 4. Sikukuu ya majuma | Siku 50 baada ya mavuno ya kwanza (katika mwezi wa 3) | Siku ya Pentekoste |
| 5. Matarumbeta | Siku ya 1 ya mwezi wa 7 | Tangazo la Hukumu |
| 6. Siku ya Upatanisho | Siku ya 10 ya mwezi wa 7 | Siku ya Hukumu |
| 7. Sikukuu ya Vibanda | Siku ya 15-22 ya mwezi wa 7 | Ujio wa Kristo mara ya pili |

Ukristo ungeonyesha kwamba njia ya Mungu ni kupitia Msalaba. Waadventista wangeelekeza kwenye Zaburi 77:13 na kusema kwamba njia ya Mungu ya wokovu iko katika Patakatifu. Msalaba ni kiini cha mpango mzima, lakini mpango wa wokovu ni mchakato si tukio tu. Kilele cha mpango wa wokovu ni siku kuu ya hukumu ambayo kulingana na mlolongo wa Danieli 7 na 8, hutokea kabla ya Ujio wa Pili wa Kristo.

Mwasisi wa Kiadventista, Uriah Smith, anaonyesha maana muhimu sana ya tofauti hii ya Upatanisho kati ya Waprotestanti na Wadventista:

> *Katika mlolongo mrefu wa masomo ambayo suala la patakatifu linasimama kwa muungano wa ukaribu sana, na katika ufahamu wake ambalo linadhibiti ushawishi mkubwa, fundisho la upatanisho linachukua nafasi kuu.*
>
> *Tayari tumeona kwamba kutakaswa kwa patakatifu, hukumu ya upelelezi ya watakatifu, kufutwa, au ondoleo, la dhambi, na utimilifu wa siri ya Mungu, yote ni kitu kimoja. Sasa tunatoa kauli ya ziada kwamba huu pia ni upatanisho.*
>
> ***Mara kwa mara usemi unasemwa kwamba Kristo alipatanisha dhambi zetu msalabani, unaonyesha jinsi wazo***

> ***linavyokubalika kwamba kumwaga damu yake na upatanisho ni kitu kimoja. Lakini hili linasababisha makosa mawili ya juu na ya msingi. Watu wamesukumwa na wazo hili hadi kupindukia kwenye makosa katika mwelekeo tofauti****, na wametumia wakati wao katika vita visivyo vya lazima na visivyo na matunda.*
>
> *Maandiko yanatangaza wazi wazi kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya wote. Sasa, kwa mtazamo wa kwamba kifo cha Kristo ni upatanisho,* ***hitimisho linafikiwa kwa urahisi kwamba dhambi za wote zimepatanishwa, na hivyo kwamba hakuna hukumu inayoweza kubaki kwa yeyote. Tawi hili la hoja linachanua mara moja hadi katika Ulimwengu****.*
>
> ***Lakini Maandiko yanatuhakikishia kwa uwazi kwamba wote-hawataokolewa kama wengine wanavyofanya sasa, na mwishowe watabakia kuwa chini ya laana. Kwa hawa, bila shaka, hakuna upatanisho unaofanywa; na kama upatanisho na kifo cha Kristo ni kitu kimoja, kinachofuata ni kwamba kifo chake hakifiki mbali zaidi ya upatanisho, na hivyo kwamba hakufa kwa ajili ya wote, bali kwa ajili ya wachache tu waliochaguliwa. Juu ya tawi hili la hoja tunapata matunda machungu ya ukalvini wa hali ya juu.***
>
> *Mada ya patakatifu inatuondolea madai ya uwongo ya makosa haya yote mawili. Shida katika hali zote mbili iko katika dhana ya kawaida kwa yote wawili, ambayo ina kasoro; na kwa dhana ya uwongo, hata iweje hoja inayoegemezwa juu yake, haiwezekani kufikia hitimisho sahihi. Kifo cha Kristo na upatanisho sikitu kimoja. Na hili linaondoa ugumu wote. Kristo hakufanya upatanisho alipomwaga damu yake msalabani. Hebu ukweli huu usimamishwe milele katika akili. Uriah Smith The Sanctuary and the 2300 Days, (1877) kurasa 275.276*

Patakatifu pana ukweli muhimu ambao utamwokoa msomaji wa Biblia kutokana na makosa ya Ukalvini na kinyume chake Ulimwengu wote. Katika kizazi ambapo Ulimwengu wote unazuka upya miongoni mwa watu wa Mungu, ni muhimu kutambua kwamba si

mada ya Patakatifu au Upatanisho inayoeleweka kwa usahihi pale unapofuata njia hii.

Matokeo ya hili tutachunguza katika sura inayofuata. Tutafunga sehemu hii kwa kusisitiza tofauti kubwa kati ya fikra kuu za Kikristo na Uadventista. Kuna lengo moja tu kuu katika mawazo ya Kikristo: kwamba kwa kuua mbadala badala ya mwanadamu, haki ya Mungu inaweza kutimizwa. Ingawa hili linalingana na kupigwa kwa mwamba na kuchinjwa kwa mwana-kondoo kwenye madhabahu ya shaba, halizungumzii ishara ya kuzungumza na mwamba au maana ya kweli ya mbuzi wawili waliotolewa kwenye Siku ya Upatanisho.

Kupitia kanuni mbili za msingi za:

1. Mfumo wa Kinabii wa Danieli
2. Mfumo wa Patakatifu wa Mwaka wa Kiyahudi,

mpango wa wokovu unakuwa mchakato unaofunika kipindi chote cha historia ya Kikristo na mambo makuu mawili ya msingi yanayojumuisha upatanisho:

1. Msalaba wa Kristo katika A.D. 31 na
2. Hukumu inayoanza mwaka 1844 A.D

Sehemu hizi kuu mbili zina uwezo wa sio tu kupiga mwamba lakini kuchukua hatua muhimu inayofuata ya kuzungumza na mwamba. Lakini kama tutakavyogundua, kwa sababu Uadventista haukuepuka kutoka kwenye mfumo wa haki wa Shetani-mfumo unaodai kifo-dhana ya Waadventista ya upatanisho inasimamia tu kuimarisha tatizo la haki ya uongo ya Shetani na adhabu.

Hii haipendekezi kwamba njia ambayo Waadventista wameifuata si sahihi. Kinyume chake, kazi ya Mungu, kama tulivyojadili hapo awali ni kusababisha dhambi kuongezeka ili tupate neema ya kweli. Mafundisho ya Waadventista ya hukumu, au kama wanavyoiita, Hukumu ya Upelelezi, yanazidisha mfumo wa haki wa uongo

unaokaa ndani yetu sote.[48]Yanaweka wazi mfumo sahihi wa kuja katika nuru tukufu ya injili ya kweli lakini harakati hizi zilisimama njiani na kurudi nyuma kutoka kwenye hatima yake. Uadventista uliupa ulimwengu urithi wa haki iliyoimarishwa bila kuchukua hatua za mwisho katika ufahamu wa Agano Jipya wa hukumu iliyo huru kutokana na haki ya adhabu inayodai dhabihu.

Danieli alionyeshwa kwamba mfumo wa dhabihu za kutuliza za Upagani na Upapa ungedumu hadi 1844. Kutoka wakati huu ujumbe ungekuja ambao ungeweka huru injili kutoka kwenye dhana potofu ya haki ya Mungu inayohitaji kutulizwa. Kama tutakavyojadili zaidi, ujumbe ulikuja mwishoni mwa miaka ya 1800 ambao uliwapa Waadventista ufunguo ambao wangeweza kuepuka mfumo wa utulizaji wa Shetani, lakini ujumbe huo ulikataliwa na hivyo kanisa halikuweza kufanya lolote ila kurudi nyuma kutoka kwenye hisia kali ya kuhukumu ya adhabu hadi kwenye mtazamo mkuu zaidi wa injili inayopatikana katika makanisa ya Kiprotestanti.

Lakini sasa tugeukie kwenye ukamilisho wa ufahamu wa awali wa Waadventista wa jinsi dhambi inavyoondolewa katika Patakatifu na kufutwa kabla ya Ujio wa Pili wa Kristo.

[48] Tazama kitabu As You Judge, sura ya 19. Kinachopatikana katika fatheroflove.info

SURA YA 19

# PATAKATIFU PA MBINGUNI

Ikiwa umesoma hadi hatua hii, basi uko katika kiini kabisa cha mfumo wa Waadventista kwa ajili ya mpango wa wokovu. Kushughulikia hoja hizi hakuhitaji juhudi ya kuzipatanisha zote, lakini ninaomba utambue thamani katika mchakato huu.

Katikati ya fundisho la Waadventista la upatanisho kulikuwa na imani katika Patakatifu halisi mbinguni.

> *Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu. Waebrania 8:1-2*

James White, mmoja wa waanzilishi wa harakati za Waadventista, anaweka wazi hoja ya Patakatifu pa mbinguni kama ifuatavyo:

> *Msimamo wetu ni kwamba badiliko limetukia katika cheo na kazi ya* ***Kuhani wetu Mkuu halisi katika Patakatifu halisi mbinguni,*** *ambalo yapasa kulinganishwa na kuja kwa bwana-arusi katika ndoa.*

*Mtazamo huu ni ulinzi kamili dhidi ya umizimu. [umizimu unamaanisha njia ya kujifunza Biblia]* ***Hatuamini tu katika Yesu halisi, ambaye ni "Mhudumu wa Patakatifu," bali pia tunaamini kwamba Patakatifu ni halisi****.– Na zaidi, Yohana anaposema kwamba aliona "mmoja kama Mwana wa Adamu""katikati ya vile vinara saba," yaani, katika Patakatifu, hatujui jinsi ya kukifanya kile kinara cha taa kuwa cha kiroho, na Mwana wa Adamu kuwa halisi. Kwa hiyo tunaamini kwamba zote mbili ni halisi, na kwamba Yohana alimwona Yesu akiwa "Mhudumu" katika Mahali Patakatifu. Yohana pia alikuwa na mtazamo wa sehemu nyingine ya Patakatifu, ambayo mtazamo huo unahusu wakati wa kupigwa kwa tarumbeta ya malaika wa saba.*

*…Patakatifu pa Patakatifu, lilikokuwa na Sanduku la amri kumi, palifunguliwa ili Kuhani wetu Mkuu aingie kufanya upatanisho kwa ajili ya utakaso wa Patakatifu. Ikiwa tunachukua uhuru wa kusema hakuna Sanduku la kweli, lenye amri kumi mbinguni, tunaweza kwenda hatua zaidi na kukana Mji halisi, na Mwana halisi wa Mungu. Kwa hakika, Waadventista hawapaswi kuchagua mtazamo wa kiroho, badala ya ule ambao tumeuwasilisha. Hatuoni msingi wa kati kuchukuliwa.*[49]

Hili lilikuwa wazo jipya ndani ya fikra za Kikristo. Katika kutoa maoni yake juu ya Waebrania 8 na Patakatifu, Adam Clarke anaonyesha mtazamo wa kawaida.

*Hema lilikuwa mahali miongoni mwa Wayahudi ambapo Mungu, kwa ishara ya uwepo wake, alikaa.* ***Hii inaweza tu kuwa mfano wa mbinguni, ambapo Mungu, katika utukufu wake muhimu, anakaa****, na anaonekana kwa malaika na watakatifu waliotukuzwa; na kwa hiyo mbingu inaitwa hapa maskani ya kweli, ili kuitofautisha na mfano.*[50]

[49] James White, The Parable, page 16
[50] Adam Clarke, Commentary on Hebrews 8:2

Lakini vipi kuhusu kusimikwa kwa maskani hii? Ni kitu gani ambacho Bwana alikiweka mbinguni? Clarke anaendelea:

> *Hema la Kiyahudi lilikuwa kazi ya mwanadamu, ingawa lilifanywa kwa mwongozo wa Mungu;* ***mbingu, maskani hii ya kweli, kazi ya Mungu peke yake, na yenye utukufu usio na kikomo kuliko ile ya Wayahudi. Hema pia lilikuwa ni mfano wa asili ya kibinadamu ya Kristo****, Yohana 1:14: Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, και εσκηνωσεν εν ἡμιν, akakaa kwetu; kwa maana, kama vile uwepo wa Mungu ulivyokaa ndani ya hema, ndivyo utimilifu wa Uungu, kwa jinsi ya kimwili, ulikaa ndani ya mwanadamu Kristo Yesu. Na mwili huu wa mwanadamu ulikuwa kazi pekee ya Mungu, kwani haukuja kwa njia ya kizazi cha asili*.[51]

Clarke anaonyesha kwamba hema iliyosimamishwa na Mungu katika Waebrania 8:2 ni mbinguni na labda katika jitihada za kuwasilisha jambo fulani hususani zaidi, anapendekeza asili ya kibinadamu ya Kristo kama hekalu la mwili. Kwa Waadventista kuwasilisha wazo la jengo mahususi ndani ya mbingu ambamo Mungu na Mwanawe wanafanya kazi linapingana na theolojia ya Kikristo ya kawaida kwa kiasi kikubwa kwa msingi wa imani zao na kile inachosema kuhusu Mungu Mwenyewe. Kwa mfano, makala ya kwanza ya imani ya Kianglikana. inasema:

> *Kuna Mungu mmoja tu aliye hai na wa kweli, wa milele,* ***asiye na mwili, viungo, wala matamanio****; mwenye uwezo usio na kikomo, hekima, na wema; Muumba na Mhifadhi wa vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana. Na katika umoja wa Uungu huu kuna Nafsi tatu, za utu moja, nguvu, na umilele; Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu*.[52]

Imani katika Mungu wa Utatu-katika-Mmoja ambaye hana mwili huonyesha kwamba dhana yoyote halisi ya jengo halisi mbinguni

---

[51] Ibid

[52] http://anglicansonline.org/basics/thirty-nine_articles.html

ambamo Mungu hufanya kazi kama ubatili. Sikiliza uzoefu wa Carol, ambaye alilelewa kwa kanuni hii ya imani.

> *Mungu wangu alipokuwa hana mwili, viungo, au tamaa, nilihisi kama ndege mweupe kwenye ufukwe uliofunikwa na ukungu. Mahali fulani juu yangu, nilijua nguvu tukufu inatawala mbingu, lakini yote yalikuwa fumbo na nuru baridi nyeupe ya wenye akili. Juu ya daraja langu la malipo lakini lenye kufariji wakati huo huo kwa sababu alikuwa akisimamia, na sikuhitaji kufikiria sana kuhusu hilo*.[53]

Hisia ya kufunikwa na ukungu ni matokeo ya imani ya mizimu kwenye mafundisho ya Mungu. Joseph Bates, mwanzilishi mwingine wa vuguvugu la Waadventista, anafafanua hali hiyo kwa uzuri zaidi:

> *Kwa akili yangu mfumo huu wa kiroho, wakati neno la Mungu linakubali tafsiri halisi, na - kulingana na kanuni - halisi kwanza; ni, kutumia msemo wa mabaharia, kama meli inayoelea kuelekea Boston Bay usiku, kwenye theluji nene huku mwezi ukiwa umejaa. Hakuna kitu kinachoweza kudanganya zaidi kwa baharia; mawingu yanayoruka kwa wakati mmoja yanaangaza anga kwa wembamba wa mvuke wake, (yakimtia moyo baharia kuamini kwamba sasa ataona nyumba ya mwanga) wakati unaofuata inazidi kuwa nyeusi, na hivyo inaendelea kuwadanganya, mpaka ghafula meli inaangushwa kwenye miamba - kilio kimoja cha jumla kinapaa juu cha kuomba rehema! na matumaini yote yametoweka milele - meli na mabaharia wametapakaa ufukweni! Mungu mwema! utusaidie kujiepusha na tafsiri hizi za kiroho za neno Lako, ambapo limefafanuliwa wazi sana kwamba ujio wa pili na ufalme wa Kristo utakuwa kweli na halisi, kama matukio yaliyotukia kwenye Majilio ya kwanza, ambayo sasa yameandikwa katika historia*.[54]

---

[53] https://donnacarolvoss.com/2015/02/08/without-body-parts-passions/

[54] Joseph Bates,The Opening of the Heavens, (Press of Benjamin Lindsey, 1846),page 22

Mungu wa waanzilishi wa Waadventista alikuwa tofauti kabisa na yule wa ajabu wa Kikatoliki na Kiprotestanti. James White analiweka wazi, akikabiliana na makala ya kwanza ya imani ya Kianglikana:

> *Mungu ni nini? Yeye ana mwili, akili iliyopangwa, inayomiliki mwili na viungo. Yuko katika umbo la mwanadamu. Yesu Kristo ni nini? Yeye ni Mwana wa Mungu, na ni kama Baba yake, akiwa "mng'ao wa utukufu wa Baba yake, na chapa ya nafsi yake." Yeye ni mwenye akili na mwenye mwili, viungo na matamanio; mwenye mwili usioweza kufa na mifupa isiyoweza kufa*.[55]

James White anaposema kwamba Mungu yuko katika umbo la mwanadamu, maana yake ni kwamba tumeumbwa kwa mfano wa Mungu si tu katika maadili yetu, bali pia katika umbo. Nitamruhusu aeleze msimamo wake.

> *MWANADAMU aliumbwa kwa mfano wa Mungu. "Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu." "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba." Mwa.1:26, 27. Tazama pia sura ya 9:6; 1Kor.11:7.* ***Wale wanaokana utu wa Mungu, wanasema kwamba "mfano" hapa haimaanishi umbo la kimwili, bali sura ya kimadili****, na wanafanya hili kuwa mwanzo mkuu wa kuthibitisha kutokufa kwa watu wote. Hoja inasimama hivi: Kwanza, mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu wa kimadili. Pili, Mungu ni kiumbe asiyeweza kufa. Tatu, kwa hiyo watu wote hawawezi kufa. Lakini namna hii ya kufikiri ingethibitisha pia kwamba mwanadamu ni muweza wa yote, mjuzi wa yote, na yuko kila mahali, na hivyo kumvisha mwanadamu anayeweza kufa sifa zote za mungu. Wacha tujaribu*:
>
> > *Kwanza, mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu wa kimadili.*

[55] James White, Review and Herald, August 19, 1858

> *Pili, Mungu ni muweza wa yote, mjuzi wa yote, na yuko kila mahali.*
>
> *Tatu, kwa hivyo, mwanadamu ana uwezo wote, anajua yote, na yuko kila mahali.*

*Kile ambacho kinathibitisha kupita kiasi, hakithibitishi chochote kwa uhakika, kwa hiyo msimamo kwamba sura ya Mungu ina maana ya sura yake ya maadili, hakiwezi kudumu. Kama uthibitisho kwamba Mungu ni mtu, soma maneno yake mwenyewe kwa Musa: "Bwana akasema, Tazama, pana mahali karibu nami, nawe utasimama juu ya mwamba; na itakuwa, wakati utukufu wangu ukipita, nitakutia katika ufa wa mwamba, na kukufunika kwa mkono wangu nipitapo. Nami nitauondoa mkono wangu nawe utaona sehemu zangu za nyuma; lakini uso wangu hautaonekana." kut.33:21-23. Tazama pia sura ya.24:9-11. Hapa Mungu anamwambia Musa kwamba ataona umbo lake. Kusema kwamba Mungu alimdhihirishia Musa kwamba aliona umbo lake, wakati hana umbo, ni kumshitaki Mungu kwa kuongeza katika uwongo aina ya udanganyifu wa mauzauza juu ya mtumishi wake Musa.*[56]

Inapaswa kutosha kutokana na yale ambayo tumewasilisha kwamba fundisho la Patakatifu pa mbinguni kama Waadventista walivyoeleza kwanza linahusishwa kwa karibu na maoni yao juu ya mafundisho ya Mungu. Kukanusha kwao fundisho la Utatu wa kiroho ndiko kulikowaruhusu kimantiki kuwasilisha fundisho la Patakatifu halisi mbinguni. Imani za Kikatoliki na Kiprotestanti zinakanusha hili kabisa na kutoa mapendekezo kama hayo kuwa ya kipuuzi. Fundisho la Utatu linatupilia mbali fundisho la Waadventista la upatanisho, na hivyo kupotosha maana ya aina ya Agano la Kale inayohusiana na upatanisho. Tena, sikiliza mchakato wa mantiki wa Joseph Bates, kulingana na maoni yake juu ya Mungu.

*Na Danieli, nabii, anafundisha fundisho lile lile. "Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa Mwana wa Adamu*

---

[56] James White, The Personality of God, 1861

*akaja pamoja na mawingu ya mbingu, akamkaribia huyo Mzee wa siku, (inavyoelezwa katika mstari wa tisa) wakamleta karibu naye; naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme usioangamizwa kamwe." Dan 7:13,14. Sasa sote tunakubali mtu huyu alikuwa Yesu Kristo; kwa maana hakuna aliye duniani wala mbinguni aliyepata kuwa na ahadi ya ufalme wa milele ila yeye.* ***Na je, Mzee wa siku hakumpa? Je, haungekuwa upuuzi kusema kwamba alijipatia mwenyewe? Basi, inawezaje kusemwa (au kuthibitishwa) kama wengine, kwamba Mwana ndiye Mzee wa siku; - kifungu hiki, na moja katika Ufunuo tano, huthibitisha waziwazi Mungu na Mwana wake kuwa watu wawili mbinguni****. Yesu anasema, "Mimi nalitoka ndani ya Mungu, nami nimekuja; wala sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye ndiye aliyenituma. Yohana 8:42. "Nilitoka kwa Baba, na nimekuja ulimwenguni; tena nauacha ulimwengu na kwenda kwa Baba*."[57]

Haiwezekani kwa akili ya Utatu kuamini kweli kwamba Baba anatoa ufalme halisi kwa Mwanawe. Inaweza tu kuwa ishara kwa madhumuni ya mpango wa wokovu - na hii ni fikra ya uharibifu ya Utatu. Huilazimisha akili katika gia ya sitiari na kisha huondoa akilini uhalisia wa Patakatifu, Mwana wa Adamu na Mzee wa Siku. Ukweli huu unabadilishwa na lebo za sitiari ambazo zimetundikwa ukutani ili tuvutiwe kana kwamba tuko kwenye jumba la sanaa.

> *Theolojia ya kutuliza ya Upagani iliyoinuliwa na Roma na kupanuliwa na binti zake wa Kiprotestanti imekuwa fundisho la kawaida la Waadventista wa siku hizi.*

Kama tutakavyoeleza kwa undani baadaye, vuguvugu la Waadventista hatimaye liliacha nafasi ya kufahamu ukweli katika mwaka wa 1888 na hatimaye kubadili mtazamo wake wa Mungu kurudi kwenye Utatu. Kwa hiyo, uelewa

[57] Joseph Bates, Opening of the Heavens,1846,page 18

wake wa upatanisho ulikwama, kama Bates alivyoonya kwamba kungetokea. Waliachana na uelewa halisi wa vyumba viwili vya Patakatifu na kwa hivyo wakaachwa bila chaguo lolote isipokuwa kurudi kwenye mitazamo ya kawaida ya upatanisho. Kwa hiyo, theolojia ya kutuliza ya Upagani iliyoinuliwa na Roma na kupanuliwa na binti zake wa Kiprotestanti imekuwa fundisho la kawaida la Waadventista wa siku hizi. Kama Samsoni aliyecheza na Delila kimahaba, macho ya Uadventista yameng'olewa na kwa sasa anawasagia nafaka Wafilisti wa kiroho.

Fundisho la upatanisho kama linavyoonyeshwa katika mfano wa Agano la Kale linaweza tu kupata msisitizo kwa kujengwa juu ya fundisho la Mungu Mmoja, Baba na Mwanawe pekee.[58]

Joseph Waggoner anatoa baadhi ya sababu zake za kwa nini Utatu na fundisho la upatanisho haviwezi kufanya kazi pamoja.

> *Wanatheolojia wengi wanafikiri kweli kwamba upatanisho, kwa heshima na hadhi na ufanisi wake, unategemea fundisho la utatu. Lakini tunashindwa kuona uhusiano wowote kati ya hizo mbili. Kinyume chake, watetezi wa fundisho hilo kweli huanguka katika ugumu ambao wanaonekana kuhangaika kuuepuka. Ugumu wao uko katika hili: Wanachukulia kukana utatu kuwa ni sawa na kuukana uungu wa Kristo. Ingekuwa hivyo, tunapaswa kung'ang'ania fundisho la utatu kwa uthabiti kadiri yeyote awezavyo; lakini sivyo ilivyo. Wale ambao wamesoma maelezo yetu juu ya kifo cha Mwana wa Mungu wanajua kwamba tunaamini kwa uthabiti uungu wa Kristo; lakini hatuwezi kukubali wazo la utatu, kama linavyoshikiliwa na Wana utatu, bila kuacha madai yetu juu ya hadhi ya dhabihu iliyotolewa kwa ajili ya ukombozi wetu*.[59]

[58] Kwa maelezo zaidi juu ya somo hili angalia vitabu Understanding the Personality of God by Lynnford Beachy;The Wisdom of God na My Beloved by Adrian Ebens vinavyopatikana katika fatheroflove.info
[59] J.H. Waggoner, The atonement, page 165

Waggoner, anazungumzia suala tofauti ambalo linahusiana na nani au nini hasa kilikufa Msalabani. Waggoner anafafanua:

> *Waumini wa Utatu hushikilia kwamba neno "Kristo" linabeba asili mbili tofauti: moja ambayo ilikuwa ya kibinadamu tu; nyingine, nafsi ya pili katika utatu, ambayo iliishi katika mwili kwa muda mfupi, lakini hangeweza kuteseka, au kufa; kwamba Kristo ambaye alikufa alikuwa tu asili ya kibinadamu ambayo uungu ulikuwa umekaa. Madaraja yote mawili yana matoleo ya kibinadamu, na hakuna zaidi. Haijalishi jinsi Mwana aliyekuwepo awali alikuwa ameinuliwa; haijalishi ni utukufu kiasi gani, una nguvu kiasi gani, au hata wa milele; ikiwa utu wa kibinadamu tu ndio ulikufa, dhabihu ilikuwa ya kibinadamu tu. Na kwa kadiri kifo cha Kristo kinavyohusika, huu ni Socinianism (imani inayopinga utatu na wakati huo huo ikipinga Uungu wa Kristo). Kwa hiyo usemi huo ni wa haki, kwamba fundisho la utatu linashusha hadhi upatanisho, likiegemezwa tu juu ya toleo la kibinadamu kama msingi. Nukuu chache zitaonyesha usahihi wa madai haya:*
>
> *"Akiwa kama Mungu, alitii matakwa yote ya sheria, na kuifanya iheshimike katika kuhesabiwa haki kwa wenye dhambi; akiwa kama mwanadamu, alibeba laana yake juu ya mti, na kustahimili adhabu yake."— Manual of atonement, uk. 25.*
>
> *"Mateso ya Kristo yalivumiliwa katika asili yake ya kibinadamu. Ingawa ana asili ya kimungu, lakini katika hilo hangeweza kuteseka na kufa. Mateso yake yalivumiliwa katika hali yake ya kibinadamu." Id., uk. 88.*
>
> *"Si sehemu ya fundisho la upatanisho kwamba asili ya Mungu, katika nafsi ya Mwokozi, iliteseka."— Barnes on atonement, uk. 224.*
>
> *"Ilimpasa mpatanishi awe mwanadamu, apate kufa; kwa maana, kama Mungu, hangeweza kufa."— Buck's Theol. Dict.,*

*"Wana Utatu hawashikilii mateso au kifo cha uungu."— Mattison on the Trinity, uk. 39.*[60]

Ingawa Waggoner anatoa hoja akiwa ndani ya mfumo wa kutuliza, hoja yake ingali halali na inaonyesha shida nyingine kati ya nyingi ambazo fundisho la Utatu huleta kwenye upatanisho. Mwanafunzi wa Biblia anakabiliwa na taraja la kwamba ni sehemu tu ya Yesu iliyokufa, ambayo hatimaye inanyang'anya fundisho la Mbadala wa Adhabu. Hii inaleta mkanganyiko na kusababisha wengi kuacha majaribio yoyote ya kuelewa upatanisho.

Je, hii inahusianaje na somo la Patakatifu halisi mbinguni? Muundo mzima wa mfumo huu wa Patakatifu unategemea imani katika Baba halisi aliyemleta Mwanawe. Hii inathibitisha uhalisi wa Mungu na Mwanawe kuwa na mwili na viungo na kwa hivyo wanaweza kufanya kazi katika Patakatifu halisi palipoundwa kwa vitu halisia. Ona kile ambacho Waadventista wa baadaye, baada ya kukumbatia Utatu, wanakifanya kwenye vifungu kama vile Danieli 7 vinavyoeleza Mungu akiwa ameketi kwenye kiti cha enzi na akisimamia hukumu katika Patakatifu mbinguni.

*Inafaa kuzingatiwa ni ukweli kwamba kauli hii haitoi maoni yoyote juu ya kama washiriki wa Uungu wana miili ya kimwili. Waadventista wamesitasita kukisia kuhusu kipengele hiki cha asili ya Mungu. Wakizungumza juu Yake, wanasisitiza sifa Zake, kama vile utu, kuishi kwa nafsi yake, asiye na kikomo, kutobadilika, kujua yote, kuwepo kila mahali, uweza, utakatifu, na upendo. Ni kweli kwamba katika Biblia, Mungu anaonyeshwa kuwa mwenye masikio (Zab. 17:6), pua (2 Sam. 22:9), kinywa (Kum. 8:3), mkono (Zek. 2:9), miguu (Zab.18:9). Lakini hizi kwa kawaida hufikiriwa kuwa anthropomorphisms, yaani, usemi unaohusisha sifa za kibinadamu za Mungu. Ni majaribio; inadaiwa kuwasaidia wanadamu kumwelewa Mwenyezi Mungu aliye juu yao sana*.[61]

[60] Ibid, pages165-166
[61] DonF. Neufeld,Review and Herald, October 6, 1977

Ukitaka kumfuata Yesu hadi Patakatifu pa Patakatifu kwa imani, utaona kwamba fundisho la Utatu hatimaye litaharibu mchakato huu ikiwa una utimamu kiakili. Ninaweza kushuhudia hili kwa sababu ya ukweli kwamba niliposoma katika chuo cha theolojia cha Waadventista, karibu hakuna mtu aliyeamini katika Patakatifu halisi mbinguni, wala kushikilia mafundisho ya Waadventista ya upatanisho kama yalivyofundishwa na waanzilishi wake.
Hebu turudi kwenye namna ambavyo Waadventista wa awali walivyoelewa mchakato wa upatanisho, na kisha tutauweka katika muktadha wa yale tuliyowasilisha katika nusu ya kwanza ya kitabu hiki.

SURA YA 20

# HUKUMU NA KUONDOLEWA KWA DHAMBI

Nadhani maneno ya J.H. Waggoner ni mahali pazuri pa kuzindulia ufahamu wa Waadventista wa hukumu na mantiki ya kufutwa kwa dhambi kabla ya kuja kwa Kristo.

> *Hakuna ukweli uliojitenga, unaojitegemea katika mpango mkuu wa wokovu, hata kama hakuna jukumu maalum la "kuokoa" katika maisha ya Kikristo. Inachukua jumla ya neema yote kufanya tabia kamilifu ya Kikristo; na hivyo pia* ***inachukua ukweli wote na mafundisho ya injili kufanya mfumo mmoja kamili wa wokovu****. Msingi mkuu wa yote ni dhabihu ya Kristo; kumwaga damu yake kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Ebr 9:22. Kwetu sisi ni upatanisho kupitia kifo chake. Rum 5:10; 2 Kor 5:20. Kama vile kazi ya makuhani chini ya sheria ilivyofikia lengo lake kuu wakati kuhani mkuu alipoingia patakatifu pa patakatifu na damu ya sadaka ya dhambi, na kutakasa patakatifu pa Mungu na dhambi za watu,* ***ndivyo matokeo ya injili ya ondoleo inavyotimizwa***

> ***kikamilifu, si kwa kifo cha dhabihu; si kwa toba yetu na upatanisho na Mungu; bali, kwa tendo la Kuhani wetu Mkuu, aonekanaye usoni pa Mungu kwa ajili yetu, katika kuzifuta dhambi zetu na kuziondoa milele mbele ya kiti cha enzi chake Aliye juu.***[62]

Waggoner anaweka hoja muhimu kwamba kulingana na mifano katika Agano la Kale, upatanisho unakamilishwa na matendo ya Kuhani wetu Mkuu mbinguni. Dhambi hizi hazisamehewi tu bali zinaondolewa kupitia kazi ya upatanishi ya Kristo katika Patakatifu pa mbinguni.

Tulitaja katika sura iliyotangulia jinsi mbuzi wawili walivyochaguliwa katika Siku ya Upatanisho. Mmoja alikuwa mbuzi wa Bwana na mwingine mbuzi wa Azazeli. Nitampendekeza Stephen Haskell kuelezea mchakato wa Siku ya Upatanisho katika mfumo wa kale wa Kiyahudi. Kila hatua ni muhimu, na ninashukuru sana kwa kazi ambayo waanzilishi hawa wa Kiadventista wameifanya katika kuunganisha nyenzo hii ili kutupa msingi sahihi wa kuuelewa upatanisho.

> *Kuhani mkuu akamchinja mbuzi wa BWANA, kisha akavikwa mavazi yake ya kifahari, na dirii ya kifuani ya hukumu, yenye majina ya kabila kumi na mbili za Israeli juu ya moyo wake, na vile vito vya shohamu vilivyokuwa na majina ya makabila mabegani mwake; akienda pamoja na damu ya mbuzi katika patakatifu pa patakatifu. Mara tu alipoingia ndani ya pazia la pili, akichukua chetezo cha dhahabu kilichojaa makaa ya moto kutoka kwenye madhabahu [ya uvumba] mbele za Bwana, na mkono wake ukiwa umejaa uvumba, akauweka ule uvumba juu ya makaa ndani ya chetezo; uvumba wenye harufu nzuri ungeweza kumfunika alipokuwa akipita mbele ya uwepo wa Mungu unaoonekana, kama ilivyodhihirishwa kati ya makerubi juu ya kiti cha rehema. Kwa vidole vyake alinyunyiza damu juu ya kiti cha rehema juu ya sheria iliyovunjwa ya Mungu. Kisha*

[62] J.H. Waggoner, The atonement, page 200

*akatoka kwenda katika chumba cha kwanza, akazigusa pembe za madhabahu ya dhahabu [ya uvumba] kwa damu.*

*Alipokwisha "kumaliza kupatanisha patakatifu, na hema ya kukutania, na madhabahu," alitoka nje hadi kwenye ua. Kwa mfano kuhani mkuu sasa alibeba nafsini mwake dhambi zote za wana wa Israeli ambazo zilikuwa zimeungamwa na kuhamishiwa patakatifu. Kisha akaweka mikono yake juu ya kichwa cha yule mbuzi wa Azazeli, na kuungama "juu yake maovu yote ya wana wa Israeli, na makosa yao yote katika dhambi zao zote, na kuyaweka juu ya kichwa cha yule mbuzi," na yule mbuzi akapelekwa mbali, "kwa mkono wa mtu anayefaa huko jangwani." Yule mbuzi alibeba juu yake maovu yote mpaka nchi "isiyokaliwa na watu," "nchi iliyotengwa."*

*Anaporudi ndani ya hema ya kukutania, kuhani mkuu huweka kando mavazi yake ya kifahali ya kikuhani, anavaa mavazi yake mengine; kisha anaingia tena ndani ya ua, anaisafisha ule ua kutokana na unajisi wake wa dhambi. Miili ya wale wanyama ambao damu yao ilichukuliwa ndani ya patakatifu, ilitolewa nje ya kambi na kuchomwa moto. Jua lilipotua siku ya upatanisho, dhambi zote zilikuwa zimeingia kwenye "nchi ya iliyotengwa," na hakuna kilichobaki isipokuwa majivu kuwa ukumbusho wao.*[63]

Baada ya kueleza kwa undani ishara ya mifano, Mzee Haskell sasa anawasilisha maana zake katika utimilifu wa kitu halisi.

*Hivyo ndivyo ilivyofanyika kwa mfano wa kazi hiyo ya mbinguni ambayo ni kuamua hatima ya milele ya kila nafsi ambayo imewahi kuishi duniani. Kwa mfano na kivuli dhambi za Israeli zilizoungamwa zilikuwa zimehamishwa hadi patakatifu wakati wa mwaka mzima; utakaso wa patakatifu ulikuwa ni kuondolewa kwa dhambi hizo. "Basi ilikuwa sharti mifano ya mambo yaliyo mbinguni isafishwe kwa hizo [damu ya wanyama]; bali mambo ya mbinguni yenyewe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo."*

[63] Stephen Haskell, The Cross and Its Shadow, (Review and Herald,1914), pages 210-211

*Kila dhambi imewekwa alama mbele za Bwana mbinguni. Dhambi zinapoungamwa na kusamehewa, zinafunikwa. Hilo lilifananishwa na kuhamishwa kwazo hadi patakatifu, ambapo hakuna macho ya kibinadamu isipokuwa yale ya kuhani yaliyowahi kuona madoa ya damu ya dhabihu ya dhambi kwenye pembe za madhabahu ya dhahabu mbele ya pazia.*

*Isingewezekana kwamba vitabu vya mbinguni vitakuwa na kumbukumbu za dhambi daima, au kwamba Kristo daima atabeba dhambi za ulimwengu. Kama vile ambavyo kazi ya mfano ilivyofanywa mwishoni mwa mwaka, ndivyo utakaso wa patakatifu pa mbinguni utatukia karibu na mwisho wa kazi ya ukuhani ya Kristo. Kutakaswa kwa patakatifu pa mbinguni kunahitaji kupitia kumbukumbu - hukumu ya upelelezi.*[64]

Kazi ya Kuhani Mkuu katika kuweka mikono yake juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli inahusisha uhamisho wa dhambi kwa mbuzi wa Azazeli. Uhamisho huu wa dhambi unahusisha uchunguzi wa vitabu vya kumbukumbu vya mbinguni kwa uhamisho huu kutokea. Hiki ni kipengele muhimu sana cha ufahamu wa Waadventista cha upatanisho; upitiaji wa kumbukumbu mbinguni ili kuhifadhi majina ya wale ambao wameungama na kuziacha dhambi zao na kufuta majina ya wale wanaoita jina la Kristo lakini wanakataa kunyenyekea na kutubu. Je, tunapata uthibitisho gani wa kumbukumbu hizo mbinguni?

*Naam, nataka na wewe pia, mjoli wa kweli, uwasaidie wanawake hao; kwa maana waliishindania Injili pamoja nami, na Klementi naye, na wale wengine waliotenda kazi pamoja nami,* ***ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima.*** *Wafilipi 4:3*

*Wote wakaao juu ya nchi watamsujudu,* ***ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima*** *cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ufunuo 13:8*

[64] Ibid, page212

*Ndipo wale waliomcha BWANA waliposemezana wao kwa wao. Naye BWANA akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha BWANA, na kulitafakari jina lake. Malaki 3:16*

*Umehesabu kutanga-tanga kwangu; uyatie machozi yangu katika chupa yako;* ***hayamo katika kitabu chako?*** *Zaburi 56:8*

Biblia inazungumza juu ya Kitabu cha Uzima ambacho ndani yake majina ya wale wanaomkubali Kristo kama Mwokozi wao yameandikwa. Pia kuna Kitabu cha Kumbukumbu ambapo wale wanaomwabudu Mungu maisha yao yameandikwa mbele za Mungu.

Kama tulivyotangulia kusema, kutakaswa kwa Patakatifu katika Danieli 8 kuna ulinganifu wake na kazi ya kuvichunguza vitabu vya kumbukumbu vilivyoelezewa katika Danieli 7. Hapa matendo ya wanadamu yameandikwa. Mbele kidogo, Haskell anaelezea hukumu inayopatikana katika Danieli 7.

*Tazama tukio. Baba ameketi juu ya kiti cha hukumu. Malaika, ambao wamekuwa "roho zitumikazo" kwa wale ambao kesi zao zitakaguliwa mbele za Mungu, wako tayari kutii amri. Vitabu vinafunguliwa. Lakini kuna kitu kinakosekana bado. Umakini wa Danieli sasa unavutwa kwenye "mawingu ya mbinguni" - maelfu ya malaika - wakimchukua Mwokozi mbele ya Baba kwa ushindi .... Wakati umefika ambapo Kristo atapokea ufalme Wake, na kudai raia Wake; na malaika hupenda kumbeba Amiri wao mkuu kwa ushindi mbele ya kiti cha hukumu, ambapo, vile vitabu vinafunua kumbukumbu moja ya maisha baada ya nyingine, Kristo anakiri jina la kila mshindi mbele ya Baba na mbele ya kundi lisilohesabika la malaika.*[65]

Mzee Haskell sasa anaeleza kazi ya maombezi ya Yesu Kuhani wetu Mkuu, akisihi wema wa damu yake mbele za Baba kwa niaba ya wale ambao wameungama jina lake na kutubu dhambi zao.

[65] Ibid, page 213

*Kuhani mkuu wa duniani aliwasilisha damu ili kulipia dhambi za watu; Kuhani wetu Mkuu anasihi damu yake mwenyewe. "Baba, Damu Yangu, Damu Yangu, Damu Yangu." Kuhani mkuu wa duniani alibeba chetezo pamoja na ule uvumba wenye harufu nzuri; Kristo anatoa haki yenye manukato mazuri ya tabia yake mwenyewe, ambayo Yeye huweka kwa kila mtu ambaye dhambi zake zote zimeungamwa na kufunikwa kwa damu yake wakati majina yao yanapotajwa mbele ya Hakimu mkuu.*

*Katika patakatifu pa kidunia kuhani mkuu alisimama katika chumba cha kwanza ili kugusa pembe za madhabahu ya dhahabu na kuitakasa na dhambi zote zilizohamishiwa humo; (Law. 16:18,19) kwa kuwa huduma za Siku ya Upatanisho zilipokuwa zikiendelea, kama mtu angekumbuka dhambi ambazo hazijaungamwa, bado angeweza kuleta sadaka yake ya dhambi na kusamehewa. (Hes. 29:7-11). Kwa hiyo wakati Kuhani wetu Mkuu akihudumu mbele ya Baba katika hukumu ya upelelezi, yeyote anayetambua kwamba yeye ni mwenye dhambi anaweza kuja akiungama dhambi zake na kusamehewa kwa njia ya wema wa Kristo, Mchukua-dhambi mkuu.*

*Kuhani wetu Mkuu, kazi yake itakapomalizika katika chumba cha ndani cha patakatifu pa mbinguni, atakaa kwa muda katika chumba cha nje, ili dhambi zilizoungamwa alipokuwa katika patakatifu pa patakatifu zichukuliwe, pamoja na dhambi za wenye haki wa vizazi vyote, na kuchukuliwa nje ya patakatifu.*

*Ingawa Yesu anasihi kama Kuhani wetu Mkuu, kuna tumaini kwa kila mtenda dhambi anayetubu; lakini hatimaye atakapokuja kutoka patakatifu pa patakatifu, mlango wa rehema utafungwa milele. Hakutakuwa na mwombezi tena. (Isa. 59:16). Katika mfano huo, kuhani mkuu alipotoka katika patakatifu, alikuwa "amekwisha kufanya upatanisho." Kuhani wetu Mkuu atakapokuja kutoka patakatifu pa patakatifu, atatangaza,"Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu, na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; naye aliye mtakatifu na azidi kutakaswa."(Ufu. 22:11). Kila kesi huamuliwa kwa umilele. Rehema imekamilika milele. Wote wanaongoja hadi*

*wakati huo, wakitumaini kuokolewa, hawatapata mtu wa kuwatetea mbele za Baba; watakuwa wamepotea milele.*[66]

Kwa kufuata mfano wa Siku ya Upatanisho pamoja na Maandiko mengine, wanafunzi wa Biblia Waadventista walibainisha kwa umuhimu mkubwa kwamba kazi ya Yesu akiwa mwombezi itakoma kabla Kristo hajaja tena duniani. Hili lina maana kwamba watu wa Mungu watakuwa wameacha kufanya dhambi kabla ya kuja kwa Kristo. Wanapumzika kikamilifu katika neema ya Kristo na Kristo amepewa udhibiti kamili wa maisha ya waliookolewa walio hai duniani.

Mafundisho ya Biblia kwamba maombezi ya Yesu kwa niaba ya wanadamu yanaweza kuwaongoza kwenye ukamilifu wa tabia kabla ya kuja kwake Kristo ni suala la msingi linalogawanya huduma ya Kristo katika Patakatifu na Patakatifu Zaidi. Ndani ya Patakatifu, wale wanaoomba msamaha wa dhambi kwa njia ya damu ya Kristo hawana mawazo ya kupokea kutoka Kwake tabia kamilifu kabla ya kuja kwa Kristo.

Wale walioishi kabla ya wakati wa hukumu katika 1844 waliamini kwamba Kristo alifunika dhambi zao na wangekamilishwa wakati wa kuja kwake Kristo. Kuingia huku mbinguni kupitia huduma ya Kristo katika Mahali Patakatifu kulikuwa halali kabisa. Lakini Kristo alipoingia Patakatifu pa Patakatifu, asili ya kazi yake ilikuwa kukamilisha tabia zao.

Kuna masuala manne muhimu yanayozingatiwa hapa.

1. Danieli 7 inatoa tukio la hukumu mbinguni kabla ya kuja kwa Kristo.
2. Mandhari hii ya hukumu ndipo matukio ya Siku ya Upatanisho yanafanyika mbinguni kupitia kazi ya Kristo Kuhani wetu Mkuu.

[66] Ibid, pages 214-216

3. Mandhari ya Hukumu yanafanyika katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni na ina maana kwamba kazi ya Kristo imebadilika kutoka wakati wa Oktoba 1844 na kuendelea.
4. Watu wote wa Mungu wanapaswa kujinyenyekeza na kutubu dhambi zao huku vitabu vya kumbukumbu vikichunguzwa. Imani yao inamshikilia Yesu kwa njia ambayo wanaamini kwamba Kristo atawapa ushindi kamili juu ya dhambi zao.

Tukijenga juu ya mafundisho ya waanzilishi wa Kiadventista sasa tunahitimisha kwamba uadui uliofichika mioyoni mwao ingebidi ufichuliwe kabisa, ukiriwe na kuponywa kwa huduma ya Kristo. Lengo la hukumu hii si ghadhabu ya Mungu bali dhambi ya mwanadamu na hitaji la mabadiliko ya tabia katika kufanana na Kristo. Makanisa ya Kikatoliki na Kiprotestanti yanakataa kwa nguvu wazo kwamba watu wanaweza kushinda dhambi kabisa katika maisha yao. Hii ni kwa sababu msisitizo hauko juu ya kugeuzwa kwa mwenye dhambi bali ni kufunikwa na kulindwa kwa mwenye dhambi kutokana na ghadhabu ya Mungu. Mwenye dhambi hutafuta kujiboresha kwa usaidizi wa Kristo lakini hakuna msukumo wa haraka wa kukabiliana na kila jambo la maisha ya mwenye dhambi kwa sababu hilo halina maana. Msisitizo ni kwamba mambo yote yalikamilika pale Msalabani na hakuna la kufanya isipokuwa kuamini. Ni kweli kwamba kuna hofu ya kuungua motoni ikiwa humkiri Kristo lakini mara tu unapomkubali Kristo hofu yote inatiishwa.

Mafundisho ya Kiprotestanti ya Mbadala wa Adhabu pamoja na upatanisho uliokamilika Msalabani hayampi mwanadamu nafasi ya kukabiliana na uadui uliojificha ndani ya moyo wake. Yanahakikisha kwamba mizizi iliyo ndani ya moyo wake haiwezi kamwe kuponywa na kuondolewa. Mbadala wa Adhabu hufungua mlango kwa mwanadamu kuanza kuamini kwamba Mungu anayedai kifo kama haki kwa ajili ya dhambi, anaweza kumsamehe.

*Mafundisho ya Kiprotestanti ya Mbadala wa Adhabu pamoja na upatanisho uliokamilika Msalabani hayampi mwanadamu nafasi ya kukabiliana na uadui uliojificha ndani ya moyo wake.*

Ni kuupiga mwamba na ni mwanzo wa safari katika Patakatifu lakini haiwezi kuwapa watu mlango wa Patakatifu pa Patakatifu ambapo Kristo anaweza kumfundisha kuzungumza na mwamba na kuponywa dhambi zake zote kabla ya mwisho wa maisha yake.

Ni fundisho la Waadventista la Hukumu ya Upelelezi na kazi ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu kukamilisha tabia za watu wake kabla ya kurudi duniani ambalo linampa mwanadamu fursa ya kukabiliana na uadui uliofichika unaokaa ndani ya nafsi yake dhidi ya Mungu. Uadui huu kama tulivyotaja hapo awali unadhihirika katika uelekezaji wa haki ya uwongo kwa Mungu. Ni haki inayodai kifo na kwa hiyo lazima itulizwe.

Chuki hii iliyoimarishwa lazima iondolewe kabla ya upatanisho kutekelezwa. Mtazamo wa Kikristo wa upatanisho hauna uwezo wa kufichua hali ya kutoamini iliyofichika ndani ya mwanadamu. Kama tutakavyogundua, ni fundisho la Waadventista pekee la upatanisho lenye uwezo wa kukabiliana na hali yetu ya kweli ya kibinadamu. Mada ya hukumu kabla ya Kristo kuja ni muhimu ili kutusaidia kujichunguza wenyewe ili kuona ukubwa wa tatizo letu.

Kama tulivyokwisha onyesha hapo awali, kutokana na ukweli kwamba mfumo wa mafundisho ya Waadventista haukuepuka mfumo wa haki wa uongo unaodai utulizaji, hauwezi kweli kuponya uadui uliomo ndani yetu. Si Mungu anayemkasirikia mwanadamu, anayehitaji kusuluhishwa kwa damu ya Kristo. Ni mwanadamu anayehitaji kufahamu hukumu ya adhabu iliyo ndani yake mwenyewe. Adamu alimhukumu Mwana wa Mungu katika uadui na kisha akauweka kwa Mungu kama yule ambaye haki yake ilidai kifo. Uongo huu lazima usalimishwe ili upatanisho ukamilike. Ni lazima tuache uwongo wa kwamba Mungu anahukumu na kuwaua watu kabla hatujaweza kuwa huru kweli kweli kutoka kwenye uadui huu.

Mafundisho ya Waadventista ya hukumu na kufutwa kwa dhambi yanatoa kitu cha jambo hili kutokea. Ingawa waanzilishi wa Kiadventista waliweka msingi wa uhitaji wa dhabihu na sadaka kukomeshwa katika fikira za mwanadamu, ujumbe mwingine ulihitaji kuja kwa watu wa Mungu ili wajitayarishe kusimama mbele za Mungu bila uhitaji wa haraka wa Yesu kusihi "Damu Yangu, Damu Yangu" kama njia ya kutuliza haki ya Baba inayomlinda mwenye dhambi asiuawe mbele za Mungu.

Kama vile Ibrahimu, Mwanamke Mkanaani, walivyotenda chini ya wingu la kutokuelewa, vivyo hivyo Waadventista Wasabato, katika kupokea nuru ya hukumu, waliendelea kufanya kazi chini ya kutoielewa tabia ya Mungu kama mtu ambaye haki yake lazima itulizwe. Imani ya Ibrahimu, na Mwanamke Mkanaani kupitia kutokuelewa kwao iliwaleta hadi kwenye ushindi. Je, imani ya Waadventista pia itakuwa ya ushindi?

Waadventista walihubiri sheria mpaka ikawa kavu kama vilima vya Gilboa. Wazo la hitaji la kuishinda dhambi lililowekwa pamoja na wazo la kwamba Mungu atahukumu, kuwaadhibu na kuwaangamiza wale wanaoshindwa kupata ushindi liliongeza mizigo yao kwa kiasi kikubwa.

Waadventista walijiona kama kanisa la Filadelfia lililoitwa kupitia mlango wa Patakatifu hadi Patakatifu pa Patakatifu.

*Na kwa malaika wa kanisa la Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, yeye aliye na ufunguo wa Daudi;* ***yeye afunguaye wala hapana afungaye, na kufunga wala hapana afunguaye. "*** *Ufunuo 3:7*

Kwao, mlango wa kuingia Mahali Patakatifu, ambao uliwakilisha huduma isiyo na mwisho ya msamaha bila hitaji la kushinda ulimalizika. Mlango mpya ulifunguliwa kuwaalika katika Patakatifu pa Patakatifu kupokea muhuri wa Mungu.

Tatizo lao lilikuwa ni kwamba walijaribu kuingia Patakatifu pa Patakatifu wakiwa na mtazamo mbaya wa haki ambao ulidai kutuliza. Athari ya jambo hili ilikuwa ni kuwageuza Wafiladelfia waaminifu kuwa Walaodikia wasiojali.

*Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu. Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. Ufunuo 3:15-18*

Jumuiya ya Waadventista ilikuwa imetajirika katika kuelewa mambo mengi sana kuhusu injili, unabii, Patakatifu na mambo mengine mengi lakini bila mtazamo sahihi wa tabia ya Mungu, hawakuweza kuponywa hali yao mbaya, maskini na uchi. Walikuwa vipofu kwa hali yao ya kweli. Badala ya kutubu, walichagua kujitukuza katika mambo yote ya ajabu waliyokuwa wamejifunza na kutulia katika hali ya kujiamini ambayo ingesababisha kifo.

Kama Waisraeli waliotoka Misri, walikuwa wameepuka Babeli ya mafundisho ya uwongo katika makanisa mengine. Pia, kama Israeli, waliahidi Bwana kushika njia zake zote; lakini kwa vile

hawakutambua hali yao halisi, hatimaye walishindwa kuingia katika nchi ya ahadi na kuingia jangwani katika uzoefu wao wa Kikristo.

Mungu alitamani kuwaleta kupitia ufahamu huu mbaya wa tabia yake na hukumu. Mungu alitaka kanisa lake hatimaye, baada ya maelfu ya miaka, liingie katika ahadi ya amani ya kweli na pumziko.

Mungu alituma ujumbe kwa watu wake kupitia watu wawili, E.J. Waggoner na A.T. Jones ili kuanza kurekebisha kutokuelewa huku. Ujumbe wao ulikuja katika mwaka wa 1888 na ulihubiriwa ndani ya makanisa ya Waadventista kwa miaka 7 zaidi iliyofuata. Ujumbe huu, ambao ulijikita katika ufahamu wa Agano la Kale na Agano Jipya, ulikataliwa. Kwa hivyo, ni maagano ambayo lazima tuyachunguze baadaye, tukiweka ufahamu wake wa kweli kuhusiana na upatanisho.

SURA YA 21

# KUVUNJA NIRA YA MAAGANO MAWILI

Kusoma Agano la Kale kunasadikisha zaidi kwamba Mungu anaweza kuwa mkali, mwenye nguvu na wa mauti kupitia azimio lake la kudumisha utaratibu. Tunaposoma kisa cha gharika au Sodoma na Gomora, inaonekana dhahiri kwamba haki ya Mungu itawaangamiza wavunjaji wa sheria yake. Hili linatia nguvu hitimisho kwamba dhabihu na kafara zilihitajika ili kutuliza ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi. Dhabihu za wanyama zilielekeza kwenye kifo cha Kristo, ambaye anakidhi haki ya Mungu na kufanya kila kitu kuwa kizuri tena.

Maisha ya Kristo duniani yanaonekana kuwa tofauti kabisa na jinsi Mungu anavyoonekana katika Agano la Kale. Majaribio mengi yamefanywa ili kupatanisha tofauti kati ya mandhari hizo mbili. Katika sura ya 5 tuliangalia maisha ya Kristo kama ufunuo kamili wa tabia ya Mungu na sala ya kushangaza ambayo Yesu aliomba akionyesha kwamba kazi ambayo Baba yake alimwagiza kuifanya ilikamilishwa usiku kabla ya kusulubiwa kwake. Hili lazima litufanye tutilie shaka mfumo wa msingi wa Ukristo na maana ya Msalaba.

Moja ya sifa kuu za nira ambayo Ukristo umeweka juu ya mabega yake, ili kuzuia ukweli wa tabia ya Mungu kufunuliwa kikamilifu, inapatikana katika somo la maagano mawili.

Wakristo wanafundisha kwamba Agano la Kale lilikuwa mapatano kati ya Mungu na wana wa Israeli. Kiini chake kilikuwa agano la sheria. Mungu alitarajia wao kushika sheria na wakati ambapo Mungu angeweza kuwa na neema na subira, Asingesita kuwaadhibu na kuua nafsi zisizotubu zilizovunja sheria yake. Yesu alipokuja, Agano Jipya lilianzishwa na wenye dhambi sasa walikuwa chini ya neema na si chini ya sheria. Agano Jipya linasemekana kuchukua nafasi ya Agano la Kale. Hii inatenganisha milele Agano la Kale na Jipya.

Msalaba basi unaonekana kama mgawanyiko mkubwa wa wakati. Unatenganisha dini ya Israeli na Ukristo kwa sababu dini ya Kiyahudi inasemekana kuzingatia sheria lakini Ukristo juu ya neema. Pia unagawanya Biblia katika makundi mawili ya umuhimu. Agano Jipya linazungumza juu ya ukweli wakati Agano la Kale linazungumza katika vivuli.

Mfumo huu wa maagano uliogawanyika wakati ulipoimarishwa na mwanatheolojia mashuhuri wa Kirumi Mkatoliki, Augustine, na kupitishwa moja kwa moja hadi katika makanisa ya Kiprotestanti. Kisha ulirithiwa na harakati za Waadventista na kudhaniwa kuwa ni kweli, kwani hapakuwa na mtazamo mwingine wa kuelewa maagano.

> *Katika agano hilo, hata hivyo, ambalo kwa kwa namna inayofaa linaitwa lile la Kale, na lilitolewa kwenye Mlima Sinai, ni furaha ya kidunia pekee ndiyo iliyoahidiwa. Kwa hiyo nchi ile, ambayo taifa lile, baada ya kuongozwa katika jangwa, iliitwa, nchi ya ahadi, ambamo amani na mamlaka ya kifalme, na kupata ushindi juu ya adui, na wingi wa watoto na matunda ya nchi, na karama zinazoendana na*

*ahadi za Agano la Kale.* ***Na hizi, kwa hakika, ni mifano ya baraka za kiroho zinazohusika na Agano Jipya [agano];***[67]

Augustino anasema kwamba kile kilichoahidiwa kwa Wayahudi kilihusu maisha haya tu. Hutumika tu kama mfano mdogo wa baraka zinazopatikana katika Agano Jipya.

Msingi huu ulijengwa juu yake na Uprotestanti mwingi. Ingawa walifanya jitihada za kuvunja nira hii, wote walishindwa kuuacha. Hapa kuna nukuu kutoka kwenye ungamo la imani la Mbaptisti:

> *Madaraja mawili ya maagano, yaliyotatuliwa katika maagano mawili; asili yao, na utofauti;* ***agano la kale limetimizwa, na kubadilishwa na lile jipya****; maandalizi ya ulimwengu wa Mataifa kwa ajili ya kuja kwa Masihi; asili na ubora wa injili*.[68]

Ufahamu huu wa maagano ni mfano mwingine wa uadui ndani ya mwanadamu dhidi ya Mungu.

> *Kwa maana nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu; kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Warumi 8:7*

Unaharibu kazi ya sheria kama mwalimu wa shule ili kumleta kwa Kristo. (Wagalatia 3:24). Unapasua misingi ya kweli ambazo alipewa Musa na kuzipigilia misumari kwenye msalaba wa Kirumi.
Paulo anazungumza juu ya maagano mawili wakati matukio mawili ambayo Abrahamu anayapitia katika ndoa mbili alizofunga na Sara na Hajiri.

> *Kwa maana imeandikwa ya kuwa, Ibrahimu alikuwa na wana wawili mmoja kwa mjakazi, na mmoja kwa mwungwana. Lakini yule wa mjakazi alizaliwa kwa mwili, yule wa mwungwana kwa ahadi.* ***Mambo haya husemwa kwa mfano; kwa maana hawa ndio***

---

[67] Philip Schaff, "Augustine, Anti Pelagian Writings," Nicene and Post Nicene Father Series 1, Vol 5

[68] https://founders.org/covenants/the-covenants-chapter-viii/

> ***kama maagano mawili**: moja kutoka mlima Sinai, lizaalo kwa utumwa, ambalo ni Hajiri. Wagalatia 4:22-24*

Ibrahimu alimwoa Sara kwanza. Kutokuwa na imani kwa Ibrahimu kulifunuliwa na kupanuliwa katika ndoa yake na Hajiri. Uzoefu aliokuwa nao Ibrahimu kwa Hajiri ulimnyenyekeza na kumleta kwenye miguu ya Mwokozi wake. Jeraha la kumfukuza mwanawe, Ishmaeli lilimtesa na kumwonyesha ubatili wa kujaribu kutimiza ahadi za Mungu kupitia jitihada zake mwenyewe.

Kwa hiyo kazi ya Agano la Kale ni sehemu ya mpango wa wokovu. Paulo anauita utukufu.[69]

> *…Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha. Basi, ikiwa huduma ya mauti, iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika; je! Huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu? Kwa maana ikiwa huduma ya adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi. 2 Wakorintho 3:6-9*

Ni kweli kwamba Kristo alifunua ukweli juu ya Mungu kwa njia ambayo iligawanya historia ya ulimwengu, lakini kila kitu ambacho Kristo alikifunua kinapatikana katika umbo la mbegu katika Agano la Kale. Kristo daima alirejelea Agano la Kale kama mamlaka yake kwa yale aliyosema.

Katika nuru hii, maagano mawili yanawakilisha matukio mawili ndani ya maisha ya Kikristo ya kila mtu. Sio vipindi viwili vya wakati kabla na baada ya Msalaba. Ibrahimu, Musa na Daudi walihesabiwa haki kwa imani kama Wakristo wa leo. Kristo alisema kwamba Ibrahimu aliiona siku yake na alifurahi kuiona. (Yohana 8:56). Paulo anasema kwamba injili ilihubiriwa kwa Ibrahimu. (Wagalatia 3:8).

---

[69] Kwa maelezo zaidi juu ya hili angalia kijitabu Faith Journey kinachopatikana katika fatheroflove.info

Ukweli huu kuhusu maagano ulikuwa msingi wa ujumbe uliotolewa kwa wahudumu wawili vijana walioitwa E.J. Waggoner na A.T. Jones. Katika kuongelea suala hili, Waggoner aliandika mnamo 1888:

> *Kuhesabiwa haki kwa imani ni jambo ambalo kila mtu lazima ajionee mwenyewe. Maelfu walioishi wakati wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza hawakujua lolote kuhusu tukio hili, ilhali maelfu walioishi muda mrefu kabla ya kuja kwake, waliletwa kwa Kristo kwa ajili ya msamaha, nao wakaupokea. Habili alihesabiwa haki kwa imani; Nuhu alikuwa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani; na Ibrahimu kwa kweli aliiona siku ya Kristo, na akaifurahia, ingawa alikufa miaka 2,000 kabla ya ujio wa kwanza.* ***Na hii inathibitisha kabisa kwamba mtume, katika sura ya tatu ya Wagalatia, anazungumza juu ya uzoefu wa mtu binafsi, na sio mabadiliko ya kipindi****. Hakuwezi kuwa na uzoefu wa Kikristo, hakuna imani, hakuna kuhesabiwa haki, hakuna haki, hilo si suala la mtu binafsi. Watu wanaokolewa kama watu binafsi, na si kama mataifa*.[70]

Mfumo wa agano unaotumiwa na Wakristo ambao unagawanyikia Msalabani unaunda namna mbili ambazo watu husoma Maandiko. Namna hizi mbili huashiria upinzani wa pande mbili, kama vile tunavyoona katika vita kati ya wema na uovu. Enzi ya sheria ya Agano la Kale na enzi ya neema ya Agano Jipya inamtambulisha Mungu kama mpinzani katika tabia yake. Humfanya Mungu aonekane asiyelingana, mwenye sura mbili. Kabla ya Msalaba Mungu anafanya kazi zaidi kupitia sheria. Baada ya Msalaba anafanya kazi zaidi kwa njia ya neema. Hii inalingana na kanuni ya Yin/Yang ya mashariki ambapo nukta nyeupe iko ndani ya nusu nyeusi ya duara na nukta nyeusi iko ndani ya nusu nyeupe ya duara.

Tunaweza kutofautisha mitazamo hii mawili ya maagano kama ifuatavyo:

---

[70] E.J. Waggoner, The Gospel in Galatians, (1888), page 33




*Agano la kale kabla ya msalaba, Agano jipya baada ya Israeli kuokolewa kwa sheria na Wakristo kwa neema. Msamaha kwa mifano katika Agano la kale. Msamaha halisi baada ya Msalaba.*

2. UZOEFU WA AINA MBILI




*Agano la Kale huleta katika Agano Jipya. Wote hupita kutoka Agano la kale na kwenda katika Agano Jipya. Agano la Kale huifunua dhambi; Agano Jipya hutoa Neema.*

Mfumo huu unapokubaliwa, akili hugawanyika katika usomaji wake wa Biblia. Inakubali kilicho kinyume kama kitu cha kawaida. Chukua kwa mfano aya hii:

> *Kwa maana torati ilitolewa kwa mkono wa Musa, bali neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo. Yohana 1:17 (KJV)*

Kwa kutumia mfumo wa agano wa Augustino, sheria inarejelea kipindi cha kabla ya Msalaba na neema na ukweli inarejelea baada ya Msalaba. Sheria na Kristo zimetenganishwa katika mstari huu kupitia mfumo usio sahihi. Sasa na tuisome katika toleo lingine la Biblia bila neno "bali" ambalo liliongezwa.

> *Maana torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa njia ya Yesu Kristo. Yohana 1:17 (NIV)*

Neno "maana" pia linaweza kutafsiriwa kama "kwa sababu". Ni kwa sababu torati ilikuja kwa mkono wa Musa kwamba neema na kweli huja kwa njia ya Yesu Kristo. Sheria ni mwalimu wetu wa kutuleta kwa Kristo. Utaratibu huu ulikuwa uleule katika siku za Ibrahimu kama ilivyo leo; katika vipindi vyote vya historia sheria inatuonyesha hali yetu ya dhambi kwamba tungetambua hitaji letu la Mwokozi. Uelewa wako wa maagano huathiri sana jinsi unavyosoma Maandiko. Fikiria maandishi mengine. Tazama jinsi watafsiri wanavyoongeza neno la ziada ili kulifanya lilingane na mfumo pinzani wa maagano.

> *Kwa maana ile sheria haikukamilisha neno; na pamoja na hayo kuliingizwa tumaini bora, ambalo kwa hilo twamkaribia Mungu. Waebrania 7:19 (KJV)*

Sheria inatofautishwa na tumaini bora. Sheria haifanyi chochote kuwa kikamilifu hata kidogo. Ni tumaini bora ambalo hufanya hivi. Lakini tafsiri hii haiakisi ukweli kwamba ni sheria inayokuleta kwenye tumaini lililo bora zaidi. Kama vile Daudi katika Zaburi anavyosema:

> *Sheria ya BWANA ni kamilifu, huiburudisha nafsi; ushuhuda wa BWANA ni amini, humtia mjinga hekima.Zaburi 19:7*

Jinsi unavyoelewa maandiko haya inategemea unatumia mfumo gani wa maagano. Wakati maagano mawili yanapofanyika kuwa uzoefu wa kila mtu, sheria na neema zote hufanya kazi pamoja. Hayako katika upinzani bali yanafanya kazi pamoja.
Tukirejea tena kwenye tabia ya Mungu. Unapotumia mfumo wa mfano wa agano, kifo na uharibifu unaohusishwa na Mungu katika Agano la Kale unaweza kuonekana kuendana kwa upatanifu na nuru na rehema ya Mungu kupitia Yesu katika Agano Jipya. Kwa mfano, tunaoanisha vipi kauli hizi mbili; moja kutoka kwa Yoshua katika Agano la Kale na moja kutoka kwa Yesu katika Jipya.

> *Kisha ikawa hapo walipomletea Yoshua hao wafalme watano hapo nje, Yoshua akawaita wanaume wote wa Israeli, akawaambia majemadari wa watu wa vita waliokwenda naye,* ***Haya, jongeeni karibu, mweke nyayo za miguu yenu katika shingo za wafalme hawa.***

> ***Nao wakajongea karibu, wakatia nyayo zao katika shingo zao. Yoshua akawaambia, Msiche, wala msifadhaike; iweni hodari na wa mioyo ya ushujaa; kwa kuwa ndivyo BWANA atakavyowafanyia adui zenu wote ambao mwapigana nao.*** *Baadaye Yoshua akawapiga, na kuwaua, akawatundika katika miti mitano; nao wakawa wakitundikwa katika hiyo miti hata jioni. Yoshua 10:24-26 (KJV)*

> *Na tazama, mmoja wao waliokuwa pamoja na Yesu akanyosha mkono wake, akaufuta upanga wake, akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio. Ndipo Yesu akamwambia, Rudisha upanga wako mahali pake, maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga. Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? Mathayo 26:51-53*

Anachokisema Yoshua ni kinyume kabisa na kile Yesu anachokisema. Tunaweza kuoanisha hili kwa kusema kwamba Yoshua aliishi chini ya mfumo wa sheria, mfumo wa Agano la Kale. Yesu alikuwa katika Agano Jipya. Hivi ndivyo unavyoweza kufanya matukio yanayopingana yaendane pamoja na kukufanya usihoji zaidi kwa nini yako kinyume.

Tunapotumia mfumo sahihi wa agano kama ulivyofundishwa na Waggoner na Jones, tunaweza kuanza kuona kwamba Mungu anaruhusu uadui wa asili katika Yoshua na Israeli kuongezeka. Hii ni kwa kusudi la kusababisha neema kuwa nyingi zaidi. Hii italeta uthabiti wa ufahamu kwa tabia ya Mungu kupitia Biblia nzima. Mfumo mwingine unahimiza akili kufikiria kinyume.

> *Uwili ulionekana kwa mara ya kwanza kabisa katika imani za Kidini za Kimisri kwa tofauti ya Miungu Sethi (matatizo, kifo) na Osiris (utaratibu, maisha). Dhana ya kwanza ya wazi ya uwili ilitoka kwenye Dini ya Kale ya Uajemi ya Zoroastrianism karibu katikati ya karne ya tano K.K. Zoroastrianism ni dini ya Mungu mmoja inayoamini kwamba Ahura Mazda ndiye muumbaji wa milele wa mambo yote mazuri. Ukiukaji wowote wa amri ya Ahura Mazda*

*hutoka kwa druj, ambayo ni kila kitu ambacho hakijaumbwa. Kutokana na hili huja chaguo muhimu kwa wanadamu kulifanya. Ama wanashiriki kikamilifu katika maisha ya mwanadamu kwa ajili ya Ahura Mazda au hawashiriki na kuwapa druj nguvu. Uwili wa kibinafsi ni tofauti zaidi katika imani za dini za baadae*.[71]

Dini ya Misri ilikuza uwili ili kuunganisha mungu wa uhai na mungu wa kifo. Mfumo wa maagano mawili ya Ukristo unaruhusu Mungu wa Biblia kuwa Mungu wa uzima/neema na Mungu wa kifo/sheria kwa wakati mmoja.

Uwili huu wa agano ni mwendelezo wa asili wa uwili unaodhihirishwa katika Utatu. Mwana wa Mungu anaonyeshwa sawa na Baba na bado katika mchakato wa kuzaliwa na Baba. Umoja wa Mwana na Baba unampa sifa sawa na Baba ambaye hakuzaliwa. Wakati huo huo Mwana wa Mungu amezaliwa na Baba na bado yuko katika mchakato usio na mwisho wa kuzaliwa. Mawazo haya hayapatani kiasili isipokuwa utayaweka ndani ya uwili.

Ujumbe wa Waggoner na Jones ulivunja nira ya uwili ambao uliwekwa kwa hila ndani ya Maandiko kupitia kwa "mababa wa kanisa" wa awali ambao walikuwa wameathiriwa sana na mawazo ya falsafa ya Kigiriki.

Ikiwa maagano hayo mawili yanafanya kazi pamoja katika historia ya mwanadamu, basi lazima iwe hivyo kwamba Yesu anaposema Yeye ni ufufuo na uzima, kwamba kanuni hii inapatana katika Maandiko yote. Mungu anaposemwa kuwa ni Mungu wa walio hai na si wa wafu basi hili lazima liwe hivyo katika Maandiko yote. (Mathayo 22:32).

Kwa hiyo, ukweli kuhusu maagano yaliyoletwa na Waggoner na Jones ilikuwa ni hatua muhimu katika kufichua uwili huu uliowekwa kwenye Maandiko na ulimwengu wa Kikatoliki na wa Kiprotestanti ambao uliwezesha kufikiri kwa kupingana na kukubali migongano.

[71] https://slife.org/dualism/

Adamu ndiye aliyemhukumu Baba yetu aliye mbinguni kuwa Mungu wa kifo. Uadui huu moyoni mwake uliwezeshwa kubakia kuwa umefichika kupitia mafundisho ya uwili wa kimagano na Wakatoliki na Waprotestanti.

Katika kurejesha maagano kwenye ufahamu wake sahihi, nuru inaweza kufurika juu ya Maandiko ili kuthibitisha ukweli ufuatao:

> *Kwa maana mimi, BWANA, sina kigeugeu; kwa hiyo hamkuangamizwa, enyi wana wa Yakobo. Malaki 3:6*

> *Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Waebrania 13:8*

Kristo alituambia kwamba alikuwa amedhihirisha kikamilifu tabia ya Baba yake duniani kwa wanafunzi waliomfuata.

> ***Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu****; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika. Yohana 17:6*

Kama E.J. Waggoner alivyoanza kutumia mtazamo thabiti wa Maandiko kupitia mfumo wa agano uliosahihishwa, alianza kuona mambo kama haya:

> *"Lakini," mtu fulani atasema, "Mmefanya upatanisho wote kwa upande wa wanadamu; Nimefundishwa kila mara kwamba kifo cha Kristo kilimpatanisha Mungu na mwanadamu; kwamba Kristo alikufa ili kutimiza haki ya Mungu, na kumtuliza." Naam, tumeliacha suala la upatanisho pale tu ambapo Maandiko yameliweka; na ingawa wana mengi ya kusema kuhusu ulazima wa mwanadamu kupatanishwa na Mungu, kamwe hawaonyeshi hata mara moja umuhimu wa Mungu kupatanishwa na mwanadamu.* ***Kuweka wazi ulazima wa jambo kama hilo ni kuleta mashtaka makubwa dhidi ya tabia ya Mungu. Wazo hilo limekuja katika Kanisa la Kikristo kutoka kwenye Upapa, ambalo nalo lililileta kutoka kwenye Upagani****, ambapo wazo*

*pekee la Mungu lilikuwa ni kuwa ni lazima ghadhabu yake itulizwe kwa kafara*.[72]

Waggoner anabainisha kiini cha suala hilo. Kupendekeza kwamba Kristo alikufa ili kukidhi haki ya Mungu ni kuleta mashtaka makubwa dhidi ya tabia ya Mungu. Wazo hili lilitoka kwa Upapa ambao ulilipata kutoka kwa Upagani. Hizi ndizo mamlaka mbili zilizotajwa katika Danieli 8 kama kila siku na kosa la uharibifu. Ni kupitia mfumo huu wa kutuliza ndipo watu wa Mungu wanakandamizwa na nguvu hizi mbili za uharibifu. Waggoner alilifichua mnamo 1893. Mwaka uliofuata alienda mbali zaidi:

*Wazo la upatanisho au dhabihu ni kwamba kuna ghadhabu inayotakiwa kutulizwa. Lakini zingatia hasa kwamba ni sisi tunaohitaji dhabihu, na si Mungu. Yeye anatoa dhabihu. Wazo la kwamba ghadhabu ya Mungu inapaswa kusuluhishwa ili tupate msamaha halipati kibali chochote katika Biblia. Ni upuuzi wa hali ya juu kusema kwamba Mungu amewakasirikia sana wanadamu hata hatawasamehe isipokuwa kitu fulani kimetolewa ili kutuliza ghadhabu Yake, na kwamba kwa hiyo Yeye Mwenyewe hutoa zawadi Kwake Mwenyewe, ambayo Yeye hutulizwa kwayo...*

*Wazo la Kikristo la upatanisho ni lile lililoelezwa hapo juu. Wazo la kipagani, ambalo mara nyingi hushikiliwa na wale wanaodai kuwa Wakristo, ni kwamba lazima wanadamu watoe dhabihu ili kutuliza ghadhabu ya mungu wao. Ibada zote za kipagani ni za kuhonga tu miungu yao ili iwapendeze. Ikiwa walifikiri kwamba miungu yao imewakasirikia sana, wangetoa dhabihu kubwa zaidi, na hivyo dhabihu za wanadamu zilitolewa katika hali mbaya sana. Walifikiri, kama waabudu wa Siva katika India wanavyofanya leo, kwamba mungu wao alifurahishwa na kuona damu. Mateso ambayo yalifanywa katika zile zinazoitwa nchi za Kikristo nyakati zilizopita na ni kwa kiasi fulani hata sasa, ni kupunguzwa kwa wazo hili la kipagani la upatanisho.* ***Viongozi wa makanisa hufikiri kwamba***

---

[72] E.J. Waggoner, Present Truth UK, September 21, 1893, page 386.7

***wokovu ni kwa matendo na kwamba wanadamu kwa matendo wanaweza kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi, na hivyo wanamtolea yule wanayemdhania kuwa mwasi kuwa dhabihu kwa mungu wao*** *si kwa Mungu wa kweli, kwa sababu Yeye hapendezwi na dhabihu hizo.*[73]

Hizi ni kauli za kina sana katika muktadha wa Kikristo. Hii ingetoa zana zinazohitajika ili hatimaye kuuelewa upatanisho.

Waggoner alimpinga Luther, Calvin na Waprotestanti wote katika kauli hizi. Patakatifu sasa pangeweza kweli kuanza kutakaswa dhidi ya uadui wa mwanadamu, ambao umefichwa kwa milenia na upatanisho ungeweza hatimaye kuanza kufanyika.

Hebu tusimame ili kufupisha mambo haya ya jinsi utakaso wa Patakatifu unavyoweza kufanyika.

1. Adamu aliamini kimakosa kwamba Mungu alikusudia kumuua mke wake kwa kula tunda la mti.
2. Adamu alihukumu na kumshutumu Mungu moyoni mwake na kuchukua tunda kwa uasi. Kile alichofikiri Mungu alitaka kumfanyia mke wake, alitamani kumfanyia Mungu na Mwanawe.
3. Kaini alidhihirisha uadui huu, alipomwua Abeli ndugu yake kama udhihirisho wa uadui aliouhisi dhidi ya Mungu.
4. Mfumo wa dhabihu uliotolewa ili kumwonyesha mwanadamu uadui uliokuwa ndani yake ulipindishwa na wanadamu kuwa kitu ambacho wanadamu walikifanya ili kutuliza ghadhabu ya Mungu dhidi yao. Uadui wa wanadamu dhidi ya Mungu ulielekezwa kwa Mungu kama yeye ndiye ambaye alikuwa na uadui dhidi yao.

---

[73] E.J. Waggoner, Present Truth UK, August 30, 1894, page 550

5. Mataifa mengi ya kipagani yalitengeneza mifumo ya kutoa dhabihu za wanyama au watu ili kufurahisha miungu yao, na kupotosha mpango wa awali wa dhabihu katika Edeni.
6. Kanuni za kutuliza za dhabihu zilikuja katika kanisa la Kikristo kupitia fundisho kwamba Mungu alidai kifo cha Mwanawe ili kukidhi ghadhabu na haki yake.
7. Mafundisho ya Kikristo ya upatanisho yalifundisha kwamba haki ya Mungu ilithibitishwa katika kifo cha Mwanawe.
8. Waadventista Wasabato walianzisha fundisho la Hukumu ya Upelelezi kabla ya Ujio wa Pili wa Kristo. Viambatanisho viwili muhimu vinavyosimamia hili vilikuwa ni mlolongo wa kinabii wa falme katika Danieli pamoja na mfumo wa Patakatifu wa Agano la Kale.
9. Mfumo wa Waadventista ulihamisha mwelekeo wa upatanisho kwenye kazi ya Kristo Kuhani Mkuu mbinguni na hitaji la kuondolewa kwa dhambi ndani ya mwanadamu kabla ya kuja kwake Kristo.
10. Hukumu ya Upelelezi ilizidisha hukumu ya adhabu ya mwanadamu. Ilisababisha dhambi kuwa nyingi lakini haikuleta neema nyingi sana.
11. Ujumbe wa 1888 wa Waggoner na Jones ulivunja mfumo wa maagano ya uwili wa Ukristo na kurejesha umoja wa Maandiko.
12. Hili liliwaruhusu kuufichua mfumo wa kutuliza wa dhabihu na kwa hiyo wakaanza kubadilisha maana yote ya upatanisho.

Ni kwenye mageuzi haya ya upatanisho tunayoyageukia sasa.

SURA YA 22

# KUUFIKIA UTU UZIMA—MSALABA NI JAMBO LA SASA

*Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba. Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu. Wagalatia 4:1-7*

Paulo anazungumza juu ya maisha ya Kikristo katika muktadha wa mtoto ambaye ana hisia ya mtumwa katika nyumba ya baba yake.

Hajui moyo wa baba na hivyo maisha yaye huhisi kuwa magumu na yamedhibitiwa kupita kiasi. Mabadiliko hutokea anapokua na kumjua baba yake na jinsi alivyo hasa. Anakuja kuona mambo kwa njia tofauti kabisa.

Jumbe zilizotolewa kwa Waggoner na Jones zilitoa fursa kwa kanisa la Kikristo hatimaye kufikia utu uzima; kuuelewa moyo wa Baba bila mtazamo wa uwongo wa utulizaji.

Ukristo umeutazama Msalaba wa Kristo kwa namna ile ile kama Israeli walivyomtazama nyoka wa shaba juu ya mti. Kama tulivyoona katika sura ya 7, amri ya Mungu kwa Musa ya kutengeneza sanamu ya kitu kilichokuwa kikiwauma na kuwaua ilikuwa inaendana na mawazo ya kipagani ya upatanisho. Wazo la kwamba haki ya Mungu inatimizwa katika kifo cha Mwanawe ni la kipagani sawa na kuinuliwa kwa nyoka wa shaba; hutoa ulidhishwaji wa mitazamo ya kibinadamu ya haki.

Uelewaji wetu wa kiasili wa haki ya Mungu hutufanya tuyaone matendo ya Mungu bila kujua kama bwana anayemiliki watumwa ambaye ni mkali, katili na anayeadhibu inapohitajika. Chini ya mambo ya ulimwengu, tunafasiri matendo ya Baba kuwa ni Yule ambaye kwa nguvu anapiga uasi.

Baba amengoja kwa subira na kwa uchungu watoto Wake waanze kumwelewa kiukweli. Alijua kwamba imani za kibinadamu kuhusu kutuliza zingeendelea na kupanuka kutoka wakati wa Danieli mwaka wa 600 B.K. hadi karne ya 19. Nguvu mbili za uharibifu zinazoelezewa katika Danieli 8 zingeendelea kabla dirisha halijafunguliwa kwa ajili ya sehemu ndogo ya jamii ya binadamu, kabla ya nuru kupenya kikamilifu ndani ya mioyo na akili za wanadamu.

Je, Waadventista Wasabato wangekuwa na imani ya kuzungumza na mwamba au wangeupiga kama Musa mara mbili kwa hasira, na kuharibu nafasi kwa watu kuona njia mpya na iliyo hai ya kumkaribia Baba?

Waggoner na Jones walipoendelea kuyachunguza Maandiko bila kuzuiwa na pazia la mfumo wa agano la Augustino, ukweli wa thamani ulimwagika kutoka kwenye sauti na kalamu zao.

Katika kuandika juu ya somo la Msalaba, Waggoner alipenyeza ukweli wa Agano Jipya ambao ulikuwa umefichwa kwa milenia. Hapo awali ulionekana kwa kipindi kifupi cha wakati kama uking'aa kwa nuru katika ulimwengu wa giza.

> *"Ni nani aliyewaloga, ninyi ambao Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele ya macho yenu ya kuwa amesulubiwa?" Yesu aliwekwa mbele ya Wagalatia, wakati Paulo alipowahubiria, akiwa amesulubiwa waziwazi mbele ya macho yao. Uwasilishaji ulikuwa wazi sana hivi kwamba wangeweza kumwona Kristo akiwa amesulubiwa. Haikuwa uchoraji wa maneno kwa ustadi kwa upande wa Paulo, wala hayakuwa mawazo ya kufikirika kwa upande wa Wagalatia, kwani hapo ingekuwa ni udanganyifu tu. Hapana; ulikuwa ukweli halisi; Kristo alikuwa pale, amesulubiwa mbele ya macho yao, na Paulo kwa Roho aliwawezesha kumwona.*
>
> *Tunajua kwamba haukuwa ustadi wa Paulo katika kutengeneza mifano ya maneno yenye kupendeza ambayo uliwawezesha kufurahia kwamba waliuona kusulubishwa, kwa maana mahali pengine Paulo anasema kwamba alidhamiria kutojua chochote ila Yesu Kristo na Yeye aliyesulubiwa, na kwamba alijiepusha kwa makusudi na kwa uangalifu kutumia hekima ya maneno, kwa kuogopa kwamba asije akafanya msalaba wa Kristo kuwa bure. 1Kor.1:17,18; 2:1-4. Uzoefu wa Wagalatia katika jambo hili haukuwa wa kipekee kwao.* ***Msalaba wa Kristo ni kitu cha sasa. Usemi, "Njooni msalabani," si namna ya maneno matupu, bali ni mwaliko unaoweza kutimizwa kihalisia. Kristo amesulubishwa mbele yetu, na kila jani la majani, kila jani msituni, linaonyesha ukweli huu. Naam, tunao huo ushuhuda katika miili yetu wenyewe, kwamba ingawa sisi ni wenye dhambi na wa kuharibika, bado tunaishi. Sio mpaka mtu amuone Kristo amesulubishwa mbele***

***ya macho yake, na anaweza kuona msalaba wa Kristo kila kona, ndipo mtu atakapojua ukweli wa Injili.***[74]

Wazo la kushangaza kama hilo. Je, hili lingewezekanaje? Kristo akiteseka na akiwa katika uchungu kila siku?

"Msalaba ni kitu cha sasa!" Zaidi ya hayo, ni mpaka tulitambue hilo, vinginevyo "hatutajua uhalisi wa Injili!" Hii ni changamoto kwenye Ukristo wote. Maneno ya Waggoner yanaigusa akili kama nuru kubwa, yakiondoa mawazo ya kitoto ya upatanisho na kuchoma mfumo mzima wa Mbadala wa Adhabu kwa haraka.

Mahitaji ya adhabu yanayopatikana katika Mbadala wa Adhabu yanawasilisha Msalaba kama tukio la mara moja katika mkondo wa historia ya mwanadamu. Yanaondoa utambuzi wa uchungu wa Baba na Mwana katika kubeba hali yetu ya dhambi katika historia nzima ya jamii yetu.[75] Lakini zaidi ya hayo, inamtambulisha Mungu kuwa ndiye anayetafuta kisasi kwa ajili ya uovu. Waggoner anafungua ukweli mpya kabisa. Tukio la askari wa Kirumi wakimpiga Kristo, wakitemea mate usoni mwake, wakifunga taji ya miiba kichwani Mwake si matukio ya siku moja bali ya milenia. Kile ambacho Kristo alikidhihirisha katika mwili kwa hakika kilikuwa dirisha la kile ambacho Kristo alikipitia katika Roho kila siku kama wanadamu wao wenyewe wanavyomsulubisha upya Mwana wa Mungu (Waebrania 6:6).

Waggoner anapiga hatua katika utu uzima wa Kikristo; anaanza kuelewa moyo wa Baba na Mwana na uchungu wao kama wazazi katika kushughulika na watoto wao wenye mioyo migumu, wanaojidanganya.

Mwana mpotevu ambaye alichukua urithi wa baba yake hakuwa na mawazo au kuelewa uchungu wa baba yake alipokuwa ameenda.

---

[74] E.J. Waggoner, The Glad Tidings, (Pacific Press, 1900), pages 99-100

[75] Kwa maelezo zaidi angalia kitabu Cross Examined and Cross Encountered kinachopatikana katika fatheroflove.info

Akiwa amebaki nyumbani, baba alipiga magoti pembeni ya kitanda chake huku akibubujikwa na machozi huku akimsihi Mungu mwanae ahifadhiwe salama na arudi kifuani mwake. Mwana hakuwahi kushika upendo wa baba yake akiwa nyumbani kwa baba yake. Alitenda kama mtumwa na kubaki katika Ua wa nje wa shaba; wana masikio lakini hawasikii, wana macho lakini hawaoni.

Tangu wakati Adamu alipomhukumu na kumshutumu Baba yake wa mbinguni katika bustani, uchungu ulipenya moyo wa Baba na Mwana. Wazazi wote waliokataliwa na watoto wao hulionja hili. Adamu hakuwa na ufahamu wa kujinyima uliotakiwa kwa upande wa Mungu kuendelea kumbeba na kumpa pumzi. Mwana wa Mungu aliuawa au alichomwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu na uadui uliofichika wa Adamu. (Ufunuo 13:8).

Kama tulivyosema hapo awali katika kitabu, Kristo kamwe hakuzungumza juu ya Msalaba kama chombo cha kuridhisha haki ya Baba. Alizungumza tu juu yake kama kujinyima kunakoendelea mpaka sasa katikati ya kutokuwa na shukrani na ubinafsi wa kibinadamu. Tofauti hii ni muhimu ili kuelewa upatanisho.

*Kristo kamwe hakuzungumza juu ya Msalaba kama chombo cha kuridhisha haki ya Baba. Alizungumza tu juu yake kama kujinyima kunakoendelea mpaka sasa katikati ya kutokuwa na shukrani na ubinafsi wa kibinadamu*

> *Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. Mathayo 16:24*

Huu ndio Msalaba wa kweli na hivi ndivyo Mungu na Mwanawe wanavyofanya kila siku:

> *Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. Na mtu atakaye*

*kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili. Akuombaye, mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo. Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Mathayo 5:39-45*

Mtume Paulo alizungumza juu ya Msalaba kama ukweli wa sasa ambapo mfuasi anaingia katika uzoefu wa kusulubiwa wa kujikana nafsi pamoja na bwana wake.

*Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. Wagalatia 2:20*

*Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. 2Wakorintho 4:7-10*

Je, unaweza kufahamu athari zake? Uzoefu wa Msalaba ni kustahimili hasira na dharau ya mwanadamu bila kujibu kwa namna fulani. Ni kutoa upendo kwa malipo ya chuki; ni kuruhusu wewe mwenyewe kutoeleweka bila kujaribu kuwafichua wengine kwa uwongo na udanganyifu wao. Hivi ndivyo Yesu anavyoteseka kila siku. Tunapofanya kama Kristo, inazungumza na mioyo ya wale wanaotutesa, na kama tutakavyochunguza zaidi baadaye, inasababisha upatanisho kufanyika katika mioyo ya wale wanaotuchukia.

*Wapenzi wangu, msilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, kwa maana imeandikwa: "Kulipiza kisasi ni juu yangu; mimi*

*nitalipa, asema Bwana. Kinyume chake: "Adui yako akiwa na njaa, mpe chakula; akiwa na kiu, mpe kitu cha kunywa. Kwa kufanya hivyo, utampalia makaa ya moto juu ya kichwa chake." Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema. Warumi 12:19-21 ( NIV)*

Juu ya madhabahu ya shaba (inayowakilisha mtazamo wa mwanadamu) ya Ua wa nje iliwakilishwa dhabihu, inayowakilisha Msalaba, ikifanya utoshelevu wa haki ya Mungu. Lakini tunapokuwa katika Patakatifu pa Patakatifu panatambuliwa kama uchungu wa Kristo katika kubeba uasi na chuki ya watoto wake waovu; ni mwanzo katika akili ya mtoto ya kile ambacho Baba anateseka hasa kutokana na uovu wake. Hapo ndipo tu Mwana wa Mungu anaweza kusababisha hamu yetu ya dhabihu na matoleo kukoma na kuelewa pamoja na malaika wote kwamba Mungu hakuwahi kutaka dhabihu kwa ajili ya dhambi.

Kuuona Msalaba kama kitu cha sasa badala ya kuuona kama tukio la mara moja husaidia kueleza kwa nini Yesu aliomba kwamba aliikamilisha kazi aliyopewa na Baba kabla ya kufa kwenye Msalaba wa kimwili. Uchungu Alioupata katika Gethsemane ulikuwa mtihani Wake mkuu zaidi, ambapo damu Yake ilimwagwa au kutokwa na jasho katika pambano la nguvu zaidi ya ubinadamu akilini Mwake katika ama kuokoa ubinadamu au kuwaacha wakutane na matokeo yao wenyewe.

Baba yetu alijinyenyekeza kufanya upatanisho kwa njia ya shaba/giza ambayo tungeelewa ili kutuongoza hadi mahali ambapo hatimaye tungemjua Yeye, kutambua kutoelewa kwetu kwake, na kisha kupatanishwa na upatanisho ukamilike.

Msalaba wa Agano Jipya unavutia zaidi kuliko ule wa Agano la Kale, lakini yote mawili ni ya muhimu. Sio moja au lingine.

*Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale. Isaya 63:9*

Mateso ya Mwokozi yanajitokeza ndani ya nafsi kwa njia ya ndani zaidi. Uchungu wa Gethsemane unakuwa mlango wa kuingia katika miaka 6000 ya huzuni ya kujinyima. Ukuu wa upendo wa Mungu unakukumbatia na inakuwa haiwezekani kabisa kupinga mara tu unapofungua mlango huo.

Chini ya Msalaba huu, mwenye dhambi aliyepotea hajifikirii yeye mwenyewe bali Baba yake. Mtenda dhambi huugua kwa uchungu wa mateso aliyoyasababisha. Akiwa amevunjwa na kuondolewa, analia kwa kutojali kwake kwa ubinafsi hisia za Baba Yake. Moyo wa mawe huanza kubomoka na ahadi ya moyo mpya inamvuta mdhambi mbele. Mahali pale pale ambapo dhambi yake inazidi sasa, neema, neema tele inamvuta kwenye kifua cha upendo.

Kama mtu akivutwa katika uzoefu huu, George Fifield, mfanyakazi mwenza wa A.T. Jones aliandika maneno haya mazuri.

> *Neno "upatanisho" lina maana ya hali ya kuletwa pamoja. Dhambi ilikuwa imeleta taabu, na taabu ilikuwa imeleta kutoelewa tabia ya Mungu. Hivyo wanadamu walikuwa wakimchukia Mungu badala ya kumpenda; na kumchukia yeye, alie Baba mmoja, watu pia wakamchukia mwanadamu, ndugu yao. Hivyo, badala ya familia moja na Baba mmoja, wanadamu walitenganishwa na Mungu na kutoka kwa kila mmoja wao, na kuwekwa kando na chuki na ubinafsi. Lazima kuwe na upatanisho.*
>
> *Upatanisho unaweza kufanywa tu kwa jinsi Mungu anavyofunua upendo wake, licha ya dhambi na huzuni, kwamba mioyo ya wanadamu itaguswa kwa huruma; na wao, wakiwa wamekombolewa kutoka katika upotovu wa Shetani, wapate kuona jinsi walivyomwelewa Mungu vibaya, na hivyo kumdharau Roho wa neema yake. Hivyo waweza kuongozwa, kama ndugu wanaorudi, kurudi nyumbani kwa Baba katika umoja wenye furaha.*
>
> ***Upatanisho sio kutuliza ghadhabu ya Mungu, ili watu wathubutu kuja kwake, lakini ni kufunua upendo wake, ili waje kwake**. Hakuwa Kristo aliyekuwa akiupatanisha ulimwengu*

*na Mungu, bali ni Mungu katika Kristo akiupatanisha ulimwengu nayeye mwenyewe. Haijasemwa popote kwamba Mungu alihitaji kupatanishwa nasi; anasema: "Sikukuacha, lakini wewe umeniacha."*[76]

Asili ya kweli ya upatanisho katika Agano Jipya si jambo la kisheria bali ni suala la moyo, kwa maana mwenye hekima anasema:

*Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo, maana ndiko zitokako chemchemi za uzima. Mithali 4:23*

Fifield anaandika juu ya upatanisho kuwa unafunua upendo wa Mungu kwa kiasi kwamba unagusa mioyo ya watu na kuwavuta Kwake. Anasema si kuhusu kutuliza ghadhabu ya Mungu bali kujifunza kuhusu tabia yake na kugundua kuwa ni ghadhabu yetu ambayo ilipaswa kutulizwa.

Ningerekebisha kile ambacho Fifield alikisema kwa njia hii. Ni katika Agano la Kale kuutazama Msalaba ambapo haki inadai kutoshelezwa. Agano Jipya linatamani kuunganishwa tena kwa mioyo miwili katika upendo na maelewano. Ili hili litokee, kutoelewana ambako wanadamu wamekuwa nako kuhusu tabia ya Mungu lazima kuondolewe, vinginevyo upatanisho hauwezi kutokea.

Msalaba wa Agano la Kale hutuliza ghadhabu yetu na huturuhusu kumsamehe Mungu kwa magumu ambayo tumekumbana nayo maishani. Msalaba wa Agano Jipya hutupatia ufikiaji wa chumba kitakatifu cha moyo wa Mungu na huturuhusu kuhesabu gharama ya sisi kumtenda dhambi, ndani ya mahali pa usalama, bila laana.

Picha ya kutisha ya hakimu katika Danieli 7 ambaye anachunguza kila wazo na matendo yetu inabadilishwa kuwa picha ya Patakatifu ambayo haidai tena damu, ikiruhusu Patakatifu kutakaswa katika Danieli 8.

Hii ni njia nyembamba sana. Sheria ya Agano Jipya ni ya kiroho (Warumi 7:14). Ni suala la moyo sio kanuni ya kisheria iliyoandikwa

[76] George Fifield, God is Love, (1897), page 48

kwenye jiwe. Je, utachagua kuja katika Patakatifu Zaidi? Unapaswa kuachana na dhana zako za kitoto za Baba kama mtu anayetafuta kutulizwa kwa damu. Lazima ukubali kwamba wazo hili la uwongo lilionyeshwa kwa Mungu na Adamu na vizazi vyake vyote na lazima liachwe. Hakuna njia nyingine ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu na kusimama pale bila mpatanishi wa dhambi.

SURA YA 23

# MAANA YA DAMU KATIKA PATAKATIFU

Katika kuliondoa pazia la Agano la Kale, utukufu wa Agano la Kale unafunuliwa. Utukufu huu unaonyeshwa kwetu kupitia tabia ya Kristo.

> *Basi, kwa kuwa mna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi; nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika; ila fikira zao zilitiwa uzito.* ***Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo****; 2 Wakorintho 3:12-14*

Kumwaga damu hakueleweki tena kuwa kukidhi ghadhabu ya Mungu, lakini kwa kweli ni onyesho la ghadhabu ya mwanadamu.

> *......na kusema, Kama sisi tungalikuwako zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. Hivi mwajishuhudia wenyewe, ya kwamba ninyi ni wana wao waliowaua manabii. Kijazeni basi kipimo cha baba zenu. Enyi nyoka, wana wa*

*majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanum? Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. Amin, nawaambieni, Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki. Mathayo 23:30-36*

Damu ya Yesu haikumwagwa na wenye dhambi waliotubu bali na watu waliojawa na hasira dhidi yake. Viongozi wa Kiyahudi walisema ukweli wa kina waliposema:

*..."Sisi tunayo sheria, na kwa mujibu wa sheria hiyo inampasa kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu." Yohana 19:7*

Ukweli mzuri ni kwamba Kristo, nyikani, alishinda jaribu la Shetani la kutilia shaka uwana wetu kwa Mungu. Roho wa Yesu ametolewa kwetu bure kwamba sisi, katika Kristo, tunaweza pia kushinda majaribu ya Shetani ili kutilia shaka utambulisho wetu wa kweli.

> *Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu. Wagalatia 4:4-7*

Nguvu ya kuamini kuwa unaweza kupokea utambulisho wako kama mwana wa Mungu inaunganishwa moja kwa moja na imani yako kwamba Yesu kweli ni Mwana wa Mungu. Unapokubali ukweli huu ndipo unaweza kufahamu ukweli kwamba Mungu anakupenda kama vile anavyompenda Mwanawe. Kama Yesu alivyosema:

> *Yesu akamwambia, "Usinishike, kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba; lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu na Baba yenu na kwa Mungu wangu na Mungu wenu.'"— Yohana 20:17*

Unapojua kwamba Mungu ni Baba yako kama vile Yeye alivyo Baba wa Yesu basi maneno ya Baba, "Wewe ni Mwanangu mpendwa" yatachipuka katika nafsi yako pamoja na uzima kwa wingi. Haiwezekani kupata uzoefu kama huo ikiwa unaamini kwamba Yesu ni Mungu bila kuwa Mwana wa kweli wa Mungu. Mtu anaweza kufikiria kuwa haileti tofauti lakini Yesu anaiweka wazi kabisa aliposema:

> *Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea,* ***wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako,*** *wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Yohana 17:8 (KJV)*

Neno katika Kigiriki kwa ajili ya "nalitoka kwako" lina maana ya kutoka, *kutoka ndani ya.* Kuamini hili ndiyo nguvu ya siri ya uwana wetu kwa Mungu na hutupatia uwezo wa kupokea maneno ya Mungu, "Wewe ni mwanangu mpendwa" na hivyo kupokea upatanisho. Tunaposoma katika Wagalatia 4:6, hili linawezekana tu wakati Roho wa Mwana mzaliwa anapokaa ndani yetu na Roho huyu hawezi kukaa ndani yetu ikiwa hatumwamini Mwana mzaliwa pekee wa Baba.

Hii ndiyo njia ya Agano Jipya kuuelekea upatanisho. Haihitaji kifo cha Kristo ili kupokelewa. Lakini kama tulivyotangulia kusema, hatuwezi kuingia katika njia hii isipokuwa kupitia Agano la Kale; kwa kupigwa kwa mwamba na kumwaga damu. Hapo ndipo tu tunapoweza kutembea katika mikono ya Baba na kuzungumza na Mwamba kwa imani na kusema, "Ninaamini mimi ni mtoto wako kupitia Roho wa Mwana pekee."

Uhamisho huu kutoka kwenye ufalme wa kifo hadi ufalme wa nuru umewekwa katika kitabu *Identity Wars* kinachopatikana katika *fatheroflove.info*. kinazungumza juu ya vita katika nafsi zetu kuamini

kwamba sisi ni watoto wa Mungu kupitia Kristo. Hatupaswi kuthibitisha chochote au kutoa chochote ili kufikia ukweli huu; tunahitaji tu kuiamini kwa Roho wa Kristo.

Lakini ili kudumisha uana huu tunahitaji kuja katika uhalisia wa Mungu asiyechukua uhai. Ni hapo tu ndipo tunapoweza kuwa huru kutoka kwa Chronos na kuwa wana wa Mungu kweli bila kuogopa kifo.

Ni maisha ya Yesu duniani ambayo yalifunua tabia ya Baba Yake na kusababisha upatanisho. Ni kwa njia ya Uwana wake kwa Baba kwamba Kristo alituunganisha tena sisi ambao tuko tayari kupitishwa katika ufalme huu. Kama vile Kristo alivyotuvuta kwa Baba yake, ndivyo sisi katika siku hizi za mwisho tunaitwa katika huduma kama hiyo.

SURA YA 29

# HUDUMA YA UPATANISHO

*Lakini siku ya kumi ya mwezi huo wa saba ni siku ya upatanisho; itakuwa kusanyiko takatifu kwenu, nanyi mtazitesa nafsi zenu; nanyi mtasongeza sadaka kwa BWANA kwa njia ya moto. Nanyi msifanye kazi yo yote siku hiyo; kwa kuwa ni siku ya upatanisho, ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu mbele za BWANA, Mungu wenu. Kwa kuwa mtu awaye yote asiyejitesa mwenyewe siku iyo hiyo, atakatiliwa mbali na watu wake. Mambo ya Walawi 23:27-29*

Kwa mtu anayebaki kwenye madhabahu ya shaba, na kumhesabu Mungu kuwa anadai kifo juu ya wale ambao hawatubu, ili haki itimizwe, wanaweza tu kuwa na woga wanapotazamia hukumu.

Wale ambao hawakuhesabiwa kuwa wanastahili Siku ya Upatanisho wanakatiliwa mbali. Bado, kuna wengi ambao, ingawa bado hawana hekima kuhusu njia za Mungu, wataingia mbinguni kupitia imani yao kuu. Wamepokea msamaha wa upendo wa Mungu hivi kwamba, kama yule mwanamke ambaye alifikiri kwamba Yesu alikuwa

amemwita mbwa, imani yao inawaleta kupitia ufahamu wao mbaya kwenye uzima wa milele.

Lakini katika siku za mwisho za historia ya dunia, wale wanaopokea muhuri wa Mungu lazima waingie katika ujuzi wa kweli juu ya Baba ili kustahimili jaribu la mwisho la jamii ya kibinadamu, wakati majaribio ya wanadamu yanapofungwa na wale wanaoishi duniani wasimama mbele za Mungu bila mpatanishi.

> *Akaniambia, Usiyatie muhuri maneno ya unabii wa kitabu hiki, kwa maana wakati huo umekaribia. Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo. Ufunuo 22:10-12*

> *Akaona ya kuwa hakuna mtu, akastaajabu kwa kuwa hapana mwombezi; kwa hiyo mkono wake mwenyewe ulimletea wokovu; na haki yake mwenyewe ilimtegemeza. Isaya 59:16*

Tumejadili kwa undani sana tofauti kati ya kanuni za upatanisho za Ukristo wa kawaida na wale ambao wametembea njia ya harakati za wana Marejeo katika ufahamu wa ndani zaidi wa yote ambayo Maandiko yanasema juu ya somo hili.

Tumetaja jinsi Waadventista walivyoingia Mahali Patakatifu pa Patakatifu pamoja na Yesu katika Siku ya Upatanisho isiyo ya kawaida, na kuona umuhimu wa sheria yake, walivyoongeza hisia zao za woga kwa imani yao ya Mungu ambaye haki yake inadai kifo. Ni muhimu kuvuka kutoka katika giza hili kuingia kwenye nuru tukufu ya Mungu ambaye ni kama Yesu alipokuwa hapa duniani.

Hofu ya kuishi mbele ya Mungu bila mwombezi, ikiunganishwa na imani katika Mungu ambaye atamharibu mkosaji, hufanya iwe vigumu sana kushikilia imani. Wengine waliofanya kazi chini ya wazo potofu kwamba Mungu alidai kifo watashinda kwa imani kama Ibrahimu; lakini kuna njia iliyo bora zaidi ya kutembea na kwa wale

144,000 ambao watapata ushindi juu ya mnyama na sanamu yake, njia hii ndiyo iliyo salama zaidi kuipita.

> *Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu. Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo. Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza. 1 Yohana 4:17-19*

Kipengele kinachotupa ujasiri katika siku ya hukumu ni kwamba tumefikia hatua ya kumwona Baba kama jinsi Yesu anavyomwona. Sisi ni kama Yesu kwa kuwa tunamjua Baba kuwa kweli mwenye huruma, mwenye neema na mvumilivu katika tabia, na kwamba ni rahisi kutoa uhai wake kuliko kuwaza kuchukua uhai wa mwingine.

Sababu ambayo hatuwezi kuwa na upendo kamili kwa Mungu ni kwa sababu ya hofu yetu kwake kupitia tishio la kifo. Yohana anatuambia kwamba hofu huja kwa sababu ya mateso. Mateso kwa Kigiriki ina maana ya adhabu. Ikiwa tunashikilia imani kwamba Mungu atatuadhibu na kutukatilia mbali katika kifo, hatutaweza kuepuka woga na kwa hiyo hatuwezi kufanywa wakamilifu katika upendo.

Kama nilivyosema, kutakuwa na wengine ambao, kama Ibrahimu watafanya kazi chini ya mtazamo mbaya wa tabia ya Mungu na bado watashinda, lakini imani hii inaweza kutoshelezwa katika kifo cha kikatili. Wale 144,000 wanaopitia janga la mwisho bila kuona kifo lazima waache dhana potofu kwamba Mungu—kama anayeua—angeweza kutuacha na kututelekeza tufe katika dhambi zetu.

Ukweli kwetu sote ni kwamba, kama Kristo juu ya Msalaba, tutajaribiwa kufikiri kwamba Mungu ametuacha, wakati nguvu ambayo inaunda sanamu ya mnyama itawafanya wote kumwabudu mnyama au kufa.

> *Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza*

*mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona. Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.* Ufunuo 13:11-15

Mamlaka inayowakilishwa hapa ni Marekani. Itafika mahali katika kazi yake ambapo italazimisha ibada ya mnyama wa kwanza, ambaye ni Upapa. Haya yote yamefafanuliwa kwa kina katika kitabu Danieli na Ufunuo cha Uriah Smith.

Kabla ya amri hii ya kifo kutekelezwa, ujumbe wa tabia ya upendo ya Baba yetu utaifunika dunia nzima.

*Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na* ***nchi ikaangazwa kwa utukufu wake****. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake. Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu,*

> Ni ukweli wa tabia ya upendo ya Mungu ambayo husababisha mateso ya roho, sio hofu kwamba Mungu atakuua ikiwa hautatubu. Tofauti kati ya nafasi hizi mbili ni kubwa sana; ni tofauti kati ya uzima na kifo

*msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Ufunuo wa Yohana 18:1-4*

Mungu ataonyeshwa kama asiye na vurugu kabisa na asiye na hatia katika tabia. Nguvu za Roho Mtakatifu zitawajaza wale wanaotoa ujumbe huu kwa kiasi kwamba wataakisi tabia hii kabisa. Watajazwa na upendo wake hivi kwamba, kama harufu nzuri katika sanduku la alabasta la Mariamu, hauwezi kufichwa kutoka kwenye ulimwengu.

Wale wanaokubali ujumbe huo watazitesa nafsi zao kwa majuto kwa sababu walikuwa wamemwamini Mungu kuwa mharibifu. Wataungama uadui wao usiojulikana dhidi ya Mungu na Mwanawe. **Ni ukweli wa tabia ya upendo ya Mungu ambayo husababisha mateso ya roho, sio hofu kwamba Mungu atakuua ikiwa hautatubu**. Tofauti kati ya nafasi hizi mbili ni kubwa sana; ni tofauti kati ya uzima na kifo.

Wale wasiokubali ujumbe wa tabia ya Mungu ya upendo na huruma watajitenga wenyewe. Kama walivyohukumu na kuwashutumu wengine, ndivyo watakavyojihukumu wenyewe sasa katika kukataa kwao kuikubali nuru angavu inayoifunika dunia.

*Hata imekuwa, sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili. Ingawa sisi tumemtambua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena. Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao;* ***naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.*** *2 Wakorintho 5:16-19*

Kristo alikuja hapa duniani ili kutupatanisha na Mungu kupitia ufunuo wa tabia yake ya upendo, ambayo kwa hakika ni tabia ya Baba yake. Kazi hii ya upatanisho imekabidhiwa kwetu, kufanya kama alivyofanya.

Biblia inatuambia kwamba tumepatanishwa na Mungu kwa kifo cha Kristo (Warumi 5:10), lakini upatanisho huu unafanyika kwa sababu Kristo alitupenda sana hata alikuwa tayari kwa wanadamu kumkataa na kumwua huku bado akifunua tabia ya upendo unaosamehe. Katika mfumo wa Agano Jipya Kristo hakufa ili kuridhisha hasira ya Baba yake dhidi yetu bali alikufa kwa sababu ya hasira yetu ya kibinadamu dhidi yake. Anafunua hasira na chuki yetu kwa Mungu na wanadamu wenzetu na kisha, tunapoingia katika toba, anafunua jinsi tunavyopaswa kutenda chini ya majaribu - kuyastahimili kwa neema ya upendo, bila kumhukumu mtu yeyote. Hata tulipomfanyia hivi, upendo wake wa ajabu bado ulitusamehe na ulikuwa unafikiri jinsi ya kutufikia na kutufundisha. Upendo huo ni wa thamani na wa ajabu.

Katika siku hizi za mwisho, matukio yanayotokea katika maisha ya Kristo yatarudiwa kwa wafuasi wake:

> *Kisha nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; imetupwa chini.* ***Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao, na hawakupenda maisha yao hata kufa.*** *Ufunuo 12:10-11*

Upendo wa Mungu utakuwa mwingi sana ndani ya watu wa Mungu hivi kwamba watakuwa tayari kuyatoa maisha yao kwa ajili ya waliopotea; watakuwa tayari kuruhusu waovu wawaue na hawatakuwa na mawazo yoyote ya madhara kwao bali upendo tu.

Udhihirisho wa upendo huu katika mioyo ya wanadamu utaleta ulimwengu mzima kwenye uamuzi. Upendo kama huu hauruhusu mwitikio usio na maamuzi. Wale wanaoutazama ama watayeyuka chini ya uwezo wake au watajizatiti kuupinga.

Matukio haya yatafunga kipindi cha matazamio ya ulimwengu mzima kwa sababu wote watakuwa wamefanya uamuzi wao wenyewe.

Ni ufunuo wa upendo wa Mungu kwa ulimwengu ambao utakamilisha mchakato wa upatanisho. Wakati upendo wa Mungu

unaonyeshwa kikamilifu katika maisha ya watoto Wake, wote watafanya uamuzi wao wa kuingia katika upendo huu au kuukataa.

Si Mungu afungaye rehema ya waovu. Si Mungu anayewakatilia mbali. Waovu wenyewe ndio wanaofanya hivyo, kwa maana Mungu anasema "na mwenye kudhulumu aendelee kudhulumu." Mungu hatumii nguvu, bali huruhusu kila mtu kufanya uamuzi wake kuhusu tabia Yake.

Ndiyo maana saa ya hukumu ya Mungu imefika sasa. Hatimaye, baada ya mwisho wa ile miaka 2300, ujumbe ulikuja ulimwenguni ambao umefikia upeo katika ukweli kwamba Mungu hajeruhi wala kuangamiza.

> *Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; kwa maana dunia itajawa na kumjua BWANA kama maji yaifunikavyo bahari. Isaya 11:9*

Ujuzi wa Bwana ndio unaowafanya wasidhuru au kuharibu, kwa sababu tu Mungu hadhuru au kuharibu. Je, utapokea ukweli wa tabia ya Mungu na kuingia katika huduma ya upatanisho? Je, utamruhusu Baba yetu akuondolee uwongo kwamba haki ya Mungu inadai kifo? Je, utakubali kwamba ni chuki yako mwenyewe inayodai adhabu kwa ajili ya makosa; ugumu wa moyo wako unaodai dhabihu na matoleo?

Tafadhali ungana na wana na binti za nuru ambao wanapoteza hofu yao kwa sababu wanaacha uwongo wa adhabu ambayo hapo awali tulimhusisha Mungu.

SURA YA 30

# UJUMBE WA MALAIKA WA KWANZA

Kwa mara nyingine tena tuna deni kwa waanzilishi wa Kiadventista, kwa muunganiko waliofanya katika Maandiko, kwa ajili ya ujumbe ambao ungekuja duniani wakati ule unabii wa miaka 2300 kuhusu ghadhabu utakapokamilika. Tunarudi kwa J.H. Waggoner:

> *Danieli alisema alimsikia mtakatifu mmoja akiuliza mwingine kuhusu maono hayo kwamba yanapaswa kuwa ya muda gani, hata "kupakanyaga patakatifu na jeshi pia kukanyagwa chini ya miguu."Jibu lilitolewa kwa Danieli kwa maneno haya: "Hata siku elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa." Sasa imeonekana katika walawi 16 ya kwamba kutakaswa kwa patakatifu, na kufanya upatanisho, maana yake ni kitu kimoja; kwa maana upatanisho ulifanywa na kuhani mkuu kunyunyiza damu juu ya kiti cha rehema na madhabahu, na kuwatakasa na dhambi za watu. Kwa hiyo, usemi huu wa Dan. 8:14 ni sawa na kusema, "Hata siku elfu mbili na mia tatu, ndipo upatanisho utakapofanywa."* ***Na tena, kuelewa wakati huu ni kuelewa utimizo wa ujumbe wa Ufu. 14:6, 7, "saa ya hukumu yake imekuja," kwa maana Hukumu***

> ***inawekwa wakati upatanisho unapofanywa**. Hivyo tunaona kuwa muda uliwekwa na kutangazwa kwa ajili ya kufanya upatanisho.*[98]

Tunaona basi kwamba ujumbe wa Ufunuo 14:6-7 unatuletea ujumbe ambao upatanisho utafanyika. Ujumbe huu una vipengele 5 muhimu.

> *Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, [1] mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi kwa kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa, akisema kwa sauti kuu, [2] Mcheni Mungu na [3] kumtukuza, [4] kwa maana saa ya hukumu yake imekuja; [5] na kumwabudu yeye aliyezifanya mbingu na nchi, na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:6-7*

Neno malaika katika Kigiriki linaweza kurejelea ujumbe au mjumbe. Malaika huyu anatangaza hukumu ambayo ingekuja mwishoni mwa miaka 2300, na kuanza kazi ya mwisho ya upatanisho. Ujumbe huu uliwekwa katika muktadha wa injili ya milele.

**1. Injili ya Milele**

Injili ya Kikristo inaenea tu kutoka wakati wa Kristo hadi wakati huu. Kwa sababu ya mfumo wa maagano mawili uliotengenezwa na Augustine na wengine, injili iliyohubiriwa ilionekana kwamba imeanza wakati baada ya Msalaba wa Kristo. Wazo hili linapuuza ukweli kwamba injili ile ile ambayo ilihubiriwa kwa Ibrahimu na Israeli inahubiriwa kwetu. ( Wagalatia 3:8; Waebrania 4:1-2 ).

Kosa hili halikugunduliwa hadi E.J. Waggoner na A.T. Jones walipohubiri ujumbe wa haki kwa imani kuanzia 1888 na kuendelea. Ujumbe wa malaika wa kwanza uliwekwa katika muktadha wa injili ya milele. Tunaona kwa shauku kwamba malaika hatamki ujumbe huu bali ana ujumbe huu. Hili linaonyesha kwamba injili ya milele ingekua kutoka kwenye maneno ambayo malaika wa kwanza alizungumza.

---

[98] J.H. Waggoner, The atonement in Light of Nature and Revelation, (Review and Herald, 1884), pages 212-213

**2. Mcheni Mungu**

Sehemu ya kwanza ya ujumbe huo ni mwito wa kumwabudu Mungu wa kweli. Je, tunajuaje huyu ni Mungu? Sehemu ya 5 ya ujumbe huu inatuambia huyu ndiye Mungu aliyeziumba mbingu na nchi. Hili linatoa dokezo la kwanza, na la pili linapatikana katika aya ya kwanza ya sura ya 14:

> *Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, wenye jina lake na **jina la Baba yake limeandikwa** katika vipaji vya nyuso zao. Ufunuo wa Yohana 14:1*

Mungu huyu ni Baba; Baba aliye na Mwana pekee. Jumuiya ya Waadventista ilianzisha ujumbe wake juu ya ibada ya Mungu wa pekee wa kweli na Mwanawe pekee. Hii ni sehemu ya kwanza ya ujumbe ulionenwa na malaika. Ni jiwe kuu la msingi ambalo juu yake ujumbe uliosalia umejengwa. Paulo anathibitisha hili aliposema:

> *ili wafarijiwe mioyo yao, wakiunganishwa katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, **yaani, Kristo; ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika.** Wakolosai 2:2-3*

Tumeorodhesha baadhi ya sababu zinazofanya ibada ya Mungu wa kweli na Mwana Wake iwe muhimu kwa upatanisho katika sura ya 26. Kwa uchunguzi wa kina zaidi wa somo hili soma vitabu *Divine Risk, My Beloved na Escaping Pentagon of Lies* vinavyopatikana katika *fatheroflove.info.*

Ibada ya Mungu wa kweli hutoa njia pekee ya kuingia katika asili ya uhusiano wa upatanisho. Kwa hili tunamaanisha kwamba ukubali ambao Mwana wa Mungu anao kwa Baba unakuwa ukubali wetu kwa Baba, kwa sababu Baba ni Mungu wetu kwa njia sawa na ilivyo kwamba Baba ni Mungu wa Yesu. Ukweli wa hili unafafanuliwa na maombi ya Yesu katika Yohana 17:3.

*Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3*

Ni wawili tu ndio sehemu ya kanuni ya uzima wa milele. Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo Mwanawe.

**3. Kumtukuza**

Utukufu wa Mungu unafafanuliwa na maisha ya Yesu Kristo. Maombi yake katika Yohana 17 yanafafanua hasa utukufu wa Mungu ni nini.

*Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. Yohana 17:4*

Yesu anasema kwamba alimtukuza Baba yake duniani. Hii ina maana maisha ya duniani ya Yesu yanafafanua utukufu wa Baba. Yesu anaendelea baadaye kidogo katika maombi yake kufafanua muhuri ambao wale 144,000 wanatiwa muhuri nao kama ilivyotajwa katika Ufunuo 14:1.

***Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu;*** *walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika. Yohana 17:6*

Kwa hiyo, tabia ambayo imetiwa muhuri kwenye vipaji vya nyuso za watu wa Mungu ni tabia ileile ambayo Yesu alidhihirisha alipokuwa hapa duniani. Yesu aliwapenda adui zake na kuwasamehe wale waliokuwa wakimuua. Hakuwahi kuumiza au kuua mtu yeyote. Alionyesha rehema kwa watu wote na kuwatakia mema wote, akiwaonya juu ya hatari yao na kuonyesha dhambi zao ili kuwakomboa kutoka gizani.

Ujumbe huu ulianza kuhubiriwa na Waggoner na Jones pamoja na George Fifield lakini, kwa vile ujumbe huo ulikataliwa, ulitoweka hadi hivi majuzi. Sababu yakwa nini hili ni muhimu kwa ajili ya upatanisho imeelezwa katika sura ya 25 - Hakuna Chronos Tena. Tabia ya Mungu haina kifo ndani yake. Ikiwa tunaabudu Mungu anayeua watu basi hatuwezi kupokea tabia ya Mungu wa kweli ambaye Yesu alimfunua duniani. Huwezi kuunganishwa na Mungu

wa Biblia ikiwa unaamini kuwa Yeye ni Mungu anayeua. Huwezi kupokea upatanisho ili uwe sehemu ya 144,000. Kama nilivyoonyesha mapema, kuna wengi ambao wamekufa kabla ya kutolewa kwa ujumbe wa saa ya hukumu ya sasa ambao hawakujua mambo haya; bado watafufuliwa kwa upya wa maisha ingawa ufahamu wao haukuwa sahihi. Lakini wale ambao wametiwa muhuri katika pambano la mwisho la historia ya dunia wataepuka uwongo kwamba haki ya Mungu inadai kifo, na ni kupitia hilo watapata ushindi juu ya mnyama na sanamu yake. Hii ni kwa sababu mnyama na sanamu yake hutumia tishio la nguvu kupata kibali; na utumiaji wa nguvu wa mnyama unaweza kutetewa tu wakati wa kukabiliana na nguvu. Ikiwa hakuna kabisa vurugu au hukumu ya wengine ndani yetu kutokana na ufahamu wetu sahihi wa tabia ya Mungu, basi tofauti kati ya ukweli na makosa itakuwa wazi.

Kwa muhtasari, sala ya Yesu katika Yohana 17:3-4 inashughulikia sehemu ya 2 na 3 ya Ujumbe wa Malaika wa Kwanza.

**4. Saa ya Hukumu Yake Imekuja.**

Ili upatanisho ukamilike, kila mtu lazima ahukumu mwenyewe suala hilo. Katika mfumo wa Agano la Kale, kifungu hiki kinapendekeza kwamba Mungu anatuhukumu, lakini katika Agano Jipya, ni sisi tunaomhukumu Mungu na jinsi tabia yake ilivyo. Tunaamua kama tunataka kukaa milele pamoja na Mungu au la. Maandiko yako wazi ni nani anayehukumu.

> *Kwani ikiwa wengine hawakuamini? Je, kutokuamini kwao kutafanya uaminifu wa Mungu kuwa bure? Hakika sivyo! Hakika Mwenyezi Mungu awe mkweli na kila mtu ni mwongo. Kama ilivyoandikwa: "**Ili upate kuhesabiwa haki katika maneno yako, na kushinda uhukumiwapo.**" Warumi 3:3-4*

Mungu ndiye anayehukumiwa. Mungu hahukumu au kumshutumu mtu yeyote.

> *Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote; Yohana 5:22*

*Ninyi mwahukumu kwa jinsi ya mwili; Mimi [Yesu] simhukumu mtu yeyote. Yohana 8:15*

Mungu wala Mwana wake hawahukumu mtu yeyote kwa sababu hukumu inapelekea kwenye kifo cha mtu aliyehukumiwa. Kwa vile Mungu si Mungu wa kifo, yeye hahukumu. Sisi ndio tunajihukumu. Je, tunafanyaje hili? Ikiwa tutaamua kwamba Mungu anahukumu na kuwashutumu wenye dhambi, basi hii ndiyo hukumu ambayo tutajitolea sisi wenyewe tunapomwona katika utukufu wake wote. Kutambua kwamba mtu amemwelewa na kumhukumu Mungu vibaya, huku akiendelea kukataa kusikiliza Mungu alipojaribu kueleza, kutamfanya mtu kuiita miamba na milima imwangukie mara tu anapoijua ukweli.

*Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. Mathayo 7:1-2*

Ni kwa kuwahukumu wengine ndiko kunakovunja uhusiano wetu na Mungu kwa sababu Yeye kamwe hamhukumu mtu yeyote. Huwezi kupatanishwa na Mungu na kupokea muhuri wa tabia yake wakati unaamini kwamba Mungu atawaua adui zako. Hukumu ilianzia kwa Adamu kwa jinsi ulimwengu huu unavyohusika. Kwa zaidi kuhusu hili tazama kitabu *As You Judge* kinachopatikana katika *fatheroflove.info.*

**5. Mwabuduni Yeye Aliyezifanya Mbingu na Nchi.**

Sehemu hii ya Ujumbe wa Malaika wa Kwanza ni wito wa kuheshimu amri zote za Mungu. Neno hili karibia ni nukuu ya moja kwa moja kutoka kwenye amri ya nne inayotangaza kumwabudu Mungu katika siku ya saba.

*Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako,….Maana, kwa siku sita* ***BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo,*** *akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa. Kutoka 20:8-11*

Sabato ni uzoefu wa wale wote wanaoishi katika kifua cha Baba pamoja na Kristo. (Yohana 1:18). Pumziko kamili linaweza tu kupatikana kwa wale wanaomjua Mungu kuwa upendo kamili. Pumziko la Sabato ni matokeo yasiyoepukika ya kuamini kwamba Mungu si Mungu wa kifo na wala hahukumu. Wakati huo huo, tunaweza tu kupata pumziko hili tunapoacha asili zetu za kuhukumu kupitia neema ya Kristo.

*Uwepo wa Mungu unapatikana katika Sabato kwa wingi zaidi kuliko siku nyingine yoyote kwa sababu Yesu, Bwana wa Sabato, anapata pumziko kamilifu mikononi mwa Baba yake siku hii. Pumziko hili Kristo anashiriki na wote wanaomwamini na kupumzika pamoja Naye.*

Sabato ya siku ya Saba na Sabato za uzao wake zinazopatikana katika sikukuu huleta Roho Mtakatifu kwa watu wa Mungu ili kutia muhuri tabia ya Baba ndani ya mioyo yetu. Uwepo wa Mungu unapatikana katika Sabato kwa wingi zaidi kuliko siku nyingine yoyote kwa sababu Yesu, Bwana wa Sabato, anapata pumziko kamilifu mikononi mwa Baba yake siku hii. Pumziko hili Kristo anashiriki na wote wanaomwamini na kupumzika pamoja Naye. Uzoefu wa Sabato huja kwa wote wanaoacha juhudi zozote za kumpendeza Mungu kwa matendo yao. Uzoefu wa Sabato kila siku ya saba ni tunda la haki kwa imani. Kwa zaidi kuhusu hili tazama kitabu Fountain of Blessing na sura ya 12 ya kitabu Comforter kinachopatikana katika fatheroflove.info.

Kwa muhtasari basi hizi ni jumbe zinazoungana ili kukamilisha mchakato wa mwisho wa upatanisho:

1. Injili ya milele iliyojengwa juu ya ufahamu wa kweli wa maagano mawili.

2. Ibada ya Mungu wa pekee wa kweli na Mwana wake wa pekee. Hii inamaanisha kukataliwa kwa Utatu au mungu mwingine yeyote wa uwongo.

3. Utukufu wa tabia ya Mungu kama ilivyofunuliwa katika Mwanawe duniani. Mungu hamhukumu wala kumuua mtu yeyote.

4. Sote tuko katika mchakato wa hukumu ili kuamua tabia ya Mungu ni ipi. Je, Yeye kweli ni mwenye upendo na mwenye huruma daima, au je, Anawahukumu na kuwaangamiza wale ambao hawakubaliani Naye?

5. Ibada ya Mungu kwa nyakati zake alizoziweka kama ilivyofunuliwa katika Mambo ya Walawi 23. Huu ndio wakati Roho wa Mungu anamiminwa kwa kiwango kikubwa zaidi na kutoa nguvu ya kutia muhuri ya Roho Mtakatifu ili kutufanya kama Yesu.

Tunapokubali kweli hizi zote kwa imani ndipo malaika wa pili anayemfuata yule wa kwanza atazungumza nasi juu ya uhuru wetu kutoka kwa Babeli na divai yake. Kipindi kimoja cha nyakati zilizowekwa na Baba, Roho atadhihirisha katika maisha ya watakatifu wa Mungu na watalia kwa furaha kuu kwamba Babeli imeanguka kutoka mioyoni mwao na hatimaye wako huru.

SURA YA 31

# UMEANGUKA BABELI

> *Na malaika mwingine akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule mkubwa, maana ndio umewanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake. Ufunuo 14:8*

Malaika wa pili anamfuata malaika wa kwanza, kumaanisha kwamba kile ambacho malaika wa pili anakitangaza ni matokeo ya ujumbe wa kwanza. Je, marejeleo haya ya Babeli yanamaanisha nini na divai yake ni nini?

Neno *Babeli* umeanguka limechukuliwa kutoka katika kitabu cha Yeremia.

> *Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa BWANA; kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa na wazimu. Babeli umeanguka na kuangamia ghafula; mpigieni yowe; twaeni zeri kwa maumivu yake; ili labda apate kuponywa. Yeremia 51:7-8*

Babeli ilikuwa imeathiri ulimwengu mzima kupitia mafundisho yake ya uwongo kuhusu maisha, kifo na maisha baada ya kifo. Israeli, watu wa Mungu, walikuwa wamedanganywa na mafundisho ya Babeli na hatimaye utekaji wake wa kiroho ukawa halisia.

*Sauti yao wakimbiao na kuokoka, Kutoka katika nchi ya Babeli, Ili kutangaza Sayuni kisasi cha BWANA, Mungu wetu, Kisasi cha hekalu lake. Waiteni wapiga mishale juu ya Babeli, Naam, wote waupindao upinde; Pangeni hema kumzunguka pande zote; Ili asiokoke hata mtu mmoja wao; Mlipeni kwa kadiri ya kazi yake; Mtendeni sawasawa na yote aliyoyatenda; Kwa sababu amefanya kiburi juu ya BWANA, Juu yake aliye Mtakatifu wa Israeli. BWANA wa majeshi asema hivi, Wana wa Israeli, na wana wa Yuda, wameonewa pamoja; na wote waliowachukua mateka wanawashika sana; wanakataa kuwaacha. Mkombozi wao ni hodari; BWANA wa majeshi ndilo jina lake; yeye atawatetea kwa bidii, apate kuistarehesha nchi, na kuwasumbua wakaao katika Babeli. Yeremia 50:28-29,33-34*

Babeli inawakilisha mfumo unaopigana na watu wa Mungu, unaotaka kuwafanya watumwa. Babeli ina kiburi juu ya Bwana. Katika kitabu cha Ufunuo mji huu unawakilishwa kama mwanamke wa ajabu ambaye huwatesa na kuwaangamiza watu wa Mungu.

*Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake. Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI. Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu. Nami nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu. Ufunuo 17:4-6*

Mfumo wake wa kuabudu pamoja na dhabihu na matoleo yake ulikumbatiwa na mataifa na hatimaye mfumo huu wa Upagani ukainuliwa na kuingizwa katika mfumo wa ibada ya upapa.

Mungu anayemwabudu ni Utatu. Tabia ya Mungu anayemwabudu ni yule ambaye haki yake inadai kifo. Mungu huyu ni Mungu wa nguvu na Mungu wa hukumu, akionyesha rehema kwa wale tu wanaohesabiwa kuwa wanastahili kupitia wema wao au kupitia utegemezo wa kanisa. Siku yake ya ibada ni siku ya jua- Jumapili-na

anakaa kama hakimu tayari kuamua na kusuluhisha masuala yote ya uzima na kifo.

Babeli ni pingamizi kamili la ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14. Mafundisho yake ya ajabu yanawatia wafuasi wake utumwa wa hofu ya kifo, kuwaweka bila usalama milele na kamwe hawaruhusu kuingia katika pumziko ambalo Kristo aliahidi. Binti zake wa Kiprotestanti wanaoabudu Utatu uleule na kutunza Jumapili kwa heshima ya amri zake, wanatoa injili yenye kupendeza zaidi kuliko Rumi lakini matokeo ni yale yale; injili yao haina uwezo wa kuikomboa nafsi kutoka Babeli na mvinyo wake.

Mtu anapogundua kwamba Mungu wa Yesu Kristo hamhukumu mtu yeyote wala hawatishii kuwaua; wanapoelewa kwamba Uana wa Yesu kwa Baba ni wao wenyewe bila adhabu yoyote inayohitajika; wanapoona kwamba Mungu ndiye anayehukumiwa na wao ndio mahakimu, nafsi inaweza kupata yale ambayo Mariamu aliyapata usiku alipoosha miguu ya Yesu kwa manukato ya thamani.

> *Naye Yesu alipokuwapo Bethania katika nyumba ya Simoni mkoma, mwanamke mwenye kibweta cha marhamu ya thamani kubwa alimkaribia akaimimina kichwani pake alipoketi chakulani. Wanafunzi wake walipoona, wakachukiwa, wakasema, Ni wa nini upotevu huu?Maana marhamu hii ingaliweza kuuzwa kwa fedha nyingi wakapewa maskini. Yesu akatambua akawaambia, Mbona mnamtaabisha mwanamke? Maana ni kazi njema aliyonitendea mimi. Kwa maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi; lakini mimi hamnami siku zote. Maana kwa kunimwagia mwili wangu marhamu hiyo, ametenda hivyo ili kuniweka tayari kwa maziko yangu. Amin, nawaambieni, Kila patakapohubiriwa Injili hii katika ulimwengu wote, tendo hilo alilolitenda huyu litatajwa pia kwa kumbukumbu lake. Mathayo 26:6-13*

Mariamu anaonyesha uhuru unaokuja kwa wale wanaojua kuwa wamesamehewa na ni watoto wa Mungu wanaotunzwa. Moyo wake ulikuwa umejaa shukrani kwa Mwokozi wake kwa kurejesha hisia

zake za thamani na kusafisha akili yake kutokana na hatia yake ya zamani.

Shukrani ya nafsi yake ilionyeshwa kwa njia ya ajabu na manukato aliyokuwa amenunua na kuyamwaga kwa upendo kwa Mwokozi. Matendo yake hayakuwafurahisha wafuasi wengine wa Yesu. Kitendo hiki kilijenga chuki. Ni aina ile ile ya ghadhabu iliyoanzia moyoni mwa Adamu na kutumiwa na Pembe Ndogo hadi mwisho wa unabii wa miaka 2300.

Hasira ya wafuasi wengine wa Kristo ilikuwa ni chuki yao kwa Mungu na tabia yake bila wao kujua. Shukrani za Mariamu ziliwafichua wote, ijapokuwa hakuwa na lengo la kuwafichua. Alikuwa ametamani tu kutoa shukrani zake za dhati kwa Bwana wake kipenzi. Alikuwa ameshuhudia tabia yake nzuri; Rehema Zake nyororo, na namna yake ya upole na kujali wanaume, wanawake na watoto wote. Alionyesha tabia yake nzuri kwa kuwa alitoa kila kitu alichokuwa nacho.

*Katika siku hizi za mwisho za historia ya dunia, kikundi cha watu kitatambua uzuri wa kweli wa tabia ya Mungu. Watatambua kwamba hajawahi kuwahukumu wala kuwatishia kuwadhuru kwa sababu ya dhambi zao.*

Hiki kilikuwa kioo kamili cha kile ambacho Kristo alikuwa karibu kukifanya katika kutoa kila kitu alichokuwa nacho kwa ajili yetu sote.

Katika siku hizi za mwisho za historia ya dunia, kikundi cha watu kitatambua uzuri wa kweli wa tabia ya Mungu. Watatambua kwamba hajawahi kuwahukumu wala kuwatishia kuwadhuru kwa sababu ya dhambi zao. Matokeo ya kweli hizi yatasababisha nafsi kupata uhuru wa kweli kutoka kwa Babeli na mvinyo wake.

Kama Mariamu, lengo lao si kuwahukumu wengine kwa makosa yao, bali ni kuonyesha tu shukrani kwa ajili ya wokovu wao, wakijua kwamba wao wenyewe hawastahili kabisa, hata hivyo

watashikamana na ukweli kwamba Baba yao wa mbinguni hawahukumu.

Manukato ya shukrani yao haiwezi kusahaulika na wafuasi wengine wa Kristo watakuwa na hasira dhidi yao na kuwashtaki mbele ya ulimwengu. Wakati huo Yesu atasimama kuwatetea kama vile alivyomtetea Mariamu na matukio ya mwisho ya ulimwengu yataonekana.

> *Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye juu ya wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa, hata wakati huo. Na wakati huo watu wako wataokolewa, kila mtu atakayeonekana ameandikwa katika kitabu. Danieli 12:1*

Kisha kutakuwa na wakati wa taabu ambao haujawahi kutokea hapo awali. Shetani na malaika zake wataonekana kuchukua udhibiti kamili wa ulimwengu kwa sababu makanisa yaliyoanguka yamekataa kuja kwenye nuru ya malaika wa kwanza wa Ufunuo 14.

Kama Mariamu, lengo lao si kuwahukumu wengine kwa makosa yao, bali kuonyesha tu shukrani kwa ajili ya wokovu wao, wakijua kwamba, ingawa wao wenyewe hawastahili kabisa, Baba yao wa mbinguni hawahukumu. Haijalishi nini kitatokea wanashikilia ukweli huu.

Kama Kristo Msalabani watajaribiwa kufikiri kwamba Mungu amewaacha. Ndipo imani ya Yesu itadhihirika kikamilifu ndani yao, watamshika Mwokozi wao na kushikilia kungoja baraka ya amani iwajie kama vile Yakobo alivyoshindana mweleka na malaika usiku kucha. Wanawezeshwa kushindana na Mungu kwa sababu Shetani hawezi kuwasadikisha kwamba Mungu amewaacha kweli. Imani yao katika tabia Yake ya rehema daima inawategemeza kupitia mtihani wao na mabaki ya mwisho ya giza ndani yao yanatoweka pamoja na Agano la Kale.

Upatanisho wa mwisho umekamilika. Sisi ni wamoja na Mungu katika tabia na tuna furaha mbele yetu ya uzima wa milele. Ni safari

iliyoje! Mungu ametuongoza kutoka kwenye madhabahu ya shaba katika Ua. Alitosheleza mitazamo yetu ya kibinadamu ya haki na kuturuhusu kuamini kwamba Mchungaji alipigwa na Mungu ili rehema iweze kutushukia.

Lakini basi tunapoendelea na safari, ukweli wa tabia ya Mungu huangaza kwa wale walio tayari kuupokea. Ua umeachwa nje na tunatambua maana ya maneno ya Yesu kwamba alikuwa amemaliza yote ambayo Baba yake alimpa kufanya usiku kabla ya kufa kwake Msalabani. Ni furaha iliyoje kujua kwamba Mungu hakutamani kamwe dhabihu au matoleo, bali alifanya hivyo kwa ajili yetu, ili hitaji letu la damu kumwagika.

Sasa tunaona ukweli wa tabia ya Baba. Tunaona vivuli vyeusi vikiondolewa na tunapiga magoti mbele zake kwa machozi ya furaha tukitambua kwamba hapo awali tulimwelewa vibaya kabisa. Tunasimama kwa mshangao kutambua kwamba Kristo alichukua asili yetu ili kuua uadui wetu wa asili dhidi yake. Aliteseka kwa zaidi ya miaka 6000, siku baada ya siku akivumilia hasira yetu, akingojea wakati ambapo kundi la watu lingeamini ushuhuda Alioutoa alipokuwa duniani.

Hatimaye, sisi ni wamoja na Mungu na tunatoa shukrani kwa Mwana mzaliwa-pekee kwa kuja kutuokoa kutoka katika giza la Shetani na mfumo wake wa haki wa uwongo.

Upatanisho wa thamani kiasi gani; Ni ajabu sana kuwa katika upatanifu kamili na Mungu. Jina la Bwana lihimidiwe.

SURA YA 32

# MOYO WA SHUKRANI

Hakuna maneno ambayo yanaweza kuwasilisha shukrani ninayohisi kwa Baba yetu aliye mbinguni kwa kunisaidia kupita njia hii kuelekea upatanisho uliokamilika. Katika ujana wangu wa mwisho, niliungama dhambi zangu kwa machozi kwa Mwokozi wangu na kumshukuru Mungu kwa imani kwamba nilisamehewa.

Huu ulikuwa uzoefu wangu wa madhabahu ya shaba. Niliamini kwamba sasa nisingeangamizwa na Mungu kwa ajili ya dhambi zangu. Yesu, Yesu mpendwa, alikuwa nami daima. Nilihisi huzuni ikiwa mawazo yangu yangekengeushwa kutoka Kwake hata kwa saa chache. Kuanzia nyakati hizo hadi sasa, miaka 36 imepita kama kwa dakika moja.

Kila ukweli mpya ulipotolewa kwangu, shauku ya maarifa ya kina ilinisogeza mbele. Jinsi ya kuweka vipande vyote pamoja ilikuwa daima akilini mwangu, pamoja na huzuni yangu kwamba zaidi ya 80% ya makanisa yoyote niliyohudhuria kwa kweli hawakutaka kwenda zaidi ya ukweli wa juu juu na kujitolea kujua ukweli.

Mlango wa ukweli ulifunguliwa kwa ajili yangu miaka 20 iliyopita wakati Mwokozi wangu aliponiongoza kutambua kwamba maneno ya Baba kwa Mwanawe wakati wa ubatizo wa Kristo yalikuwa ni

maneno ambayo ningeweza kudai kuwa yangu katika Kristo. Uzoefu huu umeandikwa katika kitabu *Identity Wars* kinachopatikana katika *fatheroflove.info.*

Tangu wakati huo, kupitia shida na huzuni nyingi, ukweli umesisitizwa kupitia maombi, kujifunza Biblia na ushirikiano na watafuta ukweli wengine kote ulimwenguni.

Sasa ninasimama juu ya vilele vya juu vya milima ya injili. Ninatafakari juu ya neema ya Mungu wetu na Mwanawe na ninaridhika. Ninamhukumu Baba yangu kuwa mtu mwenye upendo zaidi, mwema, anayejali zaidi ulimwenguni. Mtu ambaye hatumii nguvu yoyote kwa watoto Wake na kamwe hawahukumu. Yeye ni mvumilivu na msitahimilivu, rehema zake ni za milele kwa wale wanaoziamini na ninamhukumu kuwa anastahiki ibada yangu milele.

Kwa Mwokozi wangu, Bwana Yesu… maneno yananikosa. Wewe ni kila kitu changu, umenibeba njia nzima na kufungua ukweli mzuri sana kwa roho yangu. Umenionyesha Baba na ninajisikia amani sana. Ninaamini kuwa nimesamehewa uwongo wangu wa giza wa hapo awali ambao nilijikongoja chini yake. Ninaomboleza kwa ajili ya uadui ambao nimeudhihirisha Kwako katika hukumu yangu na hukumu ya wengine. Lakini sasa nimebarikiwa na najua hakika utanitoa gizani.

Haya yote yanafifia sasa na furaha kamili ya upatanisho wangu iko mikononi mwangu. Bwana Yesu, ninaamini utajidhihirisha kikamilifu moyoni mwangu. Najua utamimina Roho wako juu yangu kwa nyakati zako zilizowekwa. Ninaona tabia yako nzuri; Nimeshikwa nayo kabisa. Nitasubiri kwa subira nitakavyowezeshwa na najua hivi karibuni tutaonana uso kwa uso na utaniweka mbele ya Baba yetu na nitajua kama ninavyojulikana mimi.

Kwako Bwana Yesu na kwako Baba mpendwa una uwezo na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka!

> *Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia,*

*vikisema, "Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo wa Yohana 5:13*

Ni hatua gani zinazohusika ili kupata upatano kamili na Mungu?

Je, Mungu anataka damu imwagike kabla ya kutusamehe?

Je, Mungu alisababisha Mwanawe auliwe ili kulipa deni letu la dhambi?

Kwa nini Yesu alijilinganisha na kuinuliwa kama nyoka wa shaba?

Je, kuna umuhimu gani wa Musa kuupiga Mwamba pale alipoamriwa kuusemesha?

Ikiwa wanadamu walichukuliwa mateka na Shetani, ni nani anayeweka bei ya fidia ili tuachiliwe?

Je, Ubadilishaji wa Adhabu unahitajika kwa ajili ya Wokovu?

Je, kifo cha Msalaba ni Upatanisho mbadala kwa ajili ya dhambi zetu?

Je, makanisa ya Kikristo yanafundisha ukweli kamili wa Upatanisho?

FATHER OF LOVE
fatheroflove.info